# CONSTITUTION OF KENYA REVIEW COMMISSION

# (CKRC)

## VERBATIM REPORT OF

## CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GANZE CONSTIUENCY, HELD AT VITENGENI SCHOOL

ON

6TH MAY 2001

**CONSTITUENCY PUBLIC HEARINGS, GANZE CONSTITUENCY, HELD AT VITENGENI BAPTIST SECONDARY SCHOOL ON 06/050/02**

**Present:**

1. Com. Ibrahim Lethome
2. Com. Isaac Lenaola

**Absent with apology**

1. Com. Hon. Phoebe Asiyo

**Secretariat in Attendance:**

1. Joash Aminga - Programme Officer
2. Patricia Mwangi - Verbatim Recorder
3. Rachael S. Kitonyo - Asst. Programme Officer
4. Eunice Kasisi - Sign Language Interpreter
5. Daniel Mwaringa - District Coordinator

Meeting was called to order at 9.30 a.m.

**Com. Lethome**:……Mila ikiwa inawazuia, mkae nyuma. Hii nchi sasa inategemea mstakubali ambao unategemea kina mama. Nafikiri tutaanza kikao chetu ijapo watu wengi hawajafika, tutaendelea. Na wale watakaokuja, tutaweza kuwasikiza. Najua kina mama wengine mnataka kwenda shambani kulima mihogo na nini, mpate nafasi ya kwenda. Ama sivyo? *(in dialect*). Sasa nafikiri, naona kuna Sheikh hapa hivi, hebu tuongoze kwa Dua halafu tuweze kuanza kikao hiki. Mama, wewe ni Mkristo? Hebu tuongoze kwa maombi tuanze.

**Prayer**: Asante Baba mtakatifu wa watakatifu,tunakutolea shukrani,ni asante kwa asubuhi njema hii ya leo Baba uliyetulinda kwa njia mbali mbali…hata tazama wageni wapendwa tulikuwa tukiwatarajia waingie mahali hapa. Tazama wametembea na chombo ambacho kimeumbwa na mikono ya binadamu. Lakini tazama umewalinda hata wakafika mahali hapa wakiwa salama na tunakutolea shukrani na asante. Tazama katika mkutano huu, katika njia zote tunazikabidhi mikononi mwako. Baba naomba ukapate kuvuta watu majumbani ili kila mmoja akaseme maoni yake. Mungu nenda ukapate kusafisha kila mmoja roho yake Bwana. Ukapate uonekana wewe katika mkutano huu, asionekana mwanadamu. Mungu wangu wa Rehema tumejua kwamba umesikia na utatenda hayo, maana kutenda na kutimiza ni ahadi yako Jehovah. Kwa hayo sisi bado tunakuomba na kuamini. Amen.

**Com. Lethome**: Haya, asante sana mama kwa hayo maombi. Hivi tumekuja hapa kama Tume ya marekebisho ya Katiba ya Kenya, na tumekuja kuwasikiza, hatukuja kuwazungumuzia. Leo tumekuja kusikiza maoni ya watu wa hapa, ili tuweze kuyachukua maoni hayo na tuyaweke katika Katiba mpya ambayo itakuwa ni muongozo mpya kwa nchi hii. Nafikiri

nitawajulisha kwanza wale ambao nimekuja nao hapa. Ma-commissioners. Upande wangu wa kushoto tunaye Commissioner Isaac Lenaola, ni mwanatume, Kisha karibu na yeye, kuna Rachael, yeye kazi yake ni kusajili kwa maandishi yale yote mtakayozungumuza. Pale nina Programme Officer kutoka katika makao yetu makuu Nairobi, yeye ni msimamizi wa idara, anaitwa Joash Aminga. Upande wangu wa kulia, kuna Mrs. Patricia Mwangi, kazi yake ni kunasa sauti za wazungumuzaji kwa kupitia katika hichi chombo. Hatutaki neno lolote lipotee. Kila kitu kihifadhiwe. Halafu tuna muakilishi wetu katika wilaya hii ambaye anaitwa Daniel Mwaringa, nafikiri mshamuona, si mara ya kwanza. Mwamjua huyu? Haya. Yule pale, anaitwa Esther, ikiwa kuna mama yeyote anataka kutuzungumuzia Ki-giriama ama Kichoni ama kiribe ama Kimiji-kenda, yeye ata-tafsiri, kwa hivyo usiwe na wasiwasi. Na tuna mwenzetu ambaye anaweza kutufasiria kama kuna mtu ambaye ni kiziwi, hawezi kuzungumuza au bubu, basi kunamufasiri, wana lugha yao wanaitumia ishara. Kuna mufasiri. Yaani hatutaki kumuacha Mkenya yeyote.

Na sisi kuna sheria ambazo tunafuata wakati wa kusikiza maoni. Ikiwa mtu ana maoni yake kwa maandishi, tutampa dakika tano aje aeleze yale maandishi yake, kisha atakabidhi yale maandishi. Ikiwa hana, tutampa dakika kumi, aeleze, na tunasema hivi, tuheshimu maoni ya wengine. Unajua hata nyumbani wakati mwingine, baba ana maoni tofauti na mama. Lakini haina maana nyumba ivunjike, tunaheshimiana. Una heshimu maoni ya mwingine. Kwa hivyo tuta-heshimu maoni ya kila mtu. Yale yatakayo zungumuzwa hayo ni maoni yake, kila mmoja angoje nafasi yake, atatoa maoni yake. Baada ya hapo, ikiwa commissioners wana swali lolote la kuuliza, wanaweza kuuliza. Yaani ufafanuzi, siyo swali. Ufafanuzi. Kisha tutaendelea. Kwa hivyo, huo ndio mpangilio ambao tuko nao. Tutakuwa hapa vile watu watakavyo kuja, mpaka jioni ikiwezekana, kama kutakuwa na watu wengi. Kwa hiyo tutaanza na hawa walioko hapa, baada ya kutoa maoni yako, una uhuru wa kuketi kuwasikiza wengine, au kama una kazi ya kwenda kulimia mihogo na kazi ya kuangalilia mzee chakula na watoto, unaweza kwenda.

Kwa hivyo tutaanza, na mimi ninaitwa Ibrahim Lethome, mimi ni Commissioner pia. Tunawashukuru wale wote ambao wametukaribisha hapa, headmaster tulikuwa naye hapa, tukazungumuza naye, na pia tunamshukuru bwana chief wa sehemu hii, kwa sababu ya pia kutusaidia katika kuandaa mkutano huu. Tunajua watu watakuja baadaye, Kwa hivyo tutaanza moja kwa moja, na huyu wa kwanza anasema yeye hatazungumuza. Festus? Yuko? Amesema hazungumuzi yeye. Tutaanza na Mwalimu Ponda. Mwalimu Ponda? Haya, karibia pale, useme jina lako, kisha uanze.

**Mwalimu Ponda:** Mimi naitwa Mwalimu Ponda. Mimi ni mkaaji wa Vitengeni na ningali na maoni yangu, shida za hapa Vitengeni. Mwanzo ni barabara. Pili, (interjection). Kuhusu barabara, barabara inataka urekebishaji mzuri Kwa sababu wakati wa mvua, huwa magari yana shida sana na hata kama ni mtu mwenye mali yake ya shamba anapeleka sokoni, huwa mali inaoza. Pengine ni mtu hasikii vizuri, ni mgonjwa, kupata transport ya haraka kukuja hospitali pia ni ngumu maanake hata gari zinazolala huku ni kidogo kwa vile wanajua mvua yaweza kuja wakati wowote halafu gari lika-baki huku ikawa haina kazi.

Pili, ni hospitali. Hospitali ziko sehemu mbali mbali sana. Ninapendekeza tupate hospitali nyingine ya karibu kama hapa

Vitengeni,na hapa Matanomane centre. Pili ni mambo ya school. Hiyo nayo ningependelea iwe na urekebishaji Kuhusu malipo. (interjection). Malipo hata kama haitaondolewa lakini kuwe na kiwango maalum cha chini kulingana na uwezo wetu. (interjection.) Skuli ya Msingi. Zile zingine, siwezi nikazizungumuzia sana maanake sina mtoto wangu ambaye yuko Secondary, sasa sijui ubaya wa huko wala uzuri wake.

Jambo lingine, ni kuhusu mambo ya kama ma-councillor. Ma-councillor huwa wanachaguliwa na wananchi, na wale wanaochaguliwa, kuna wengine hata hawakusoma. Kiswahili chenyewe, barua hawezi kusoma. Na kuna wengine, mtu amesoma hadi pengine Form six ama Form four, yeye anakosa kazi,. anapata yule ambaye hakuwa na gharama zozote. Pili, kuna mikutano mingine ambayo kunazungumuzwa kizungu ama kiswahili. Ikizungumuzwa kizungu, yeye bado akiondoka hapo na akaulizwa, “Pale mwisho kulizungumuzwa nini?”, hakusikia chochote. Aje akidanganya. Si pia sisi wananchi atakuja kutudanganya? Kwa hivyo inatakikana awe ana kiwango kizuri cha elimu. (interjection) Kuanzia Kidato cha Nne kuendelea. (interjection). Mtindo ungekuwa wakuchaguliwa na wananchi. Maanake wale ni wachache, ni hao ma-councilors peke yao, sasa wanaweza wakachaguana kiubaguzi kwa kuwa pengine hao ma-councilors kuna watano ambao ni ukoo moja, sasa watachagua kiukoo. Lakini ikiwa ni
wananchi, kutakuwa hakuna ubaguzi wowote. (interjection). Wabunge pia wangeanzia kama kidato cha sita, maanake yeye ako juu zaidi. (interjection). 8-4-4- ya zamani. (interjection) Hiyo form four, maanake akitoka hapo ndiyo anaenda university. (interjection). Mimi ningependekeza ibaki tu hivyo,hatuwezi kumtoa MP au councillor kabla siku zake hazijaisha. (interjection.) Mashamba? Ardhi? Kuna sehemu nyingi sana huku, zinaandikishwa na title deed zinakwama hivo hivo. Sasa hatujui zinakwamishwa na nini ama - - zinakuaje. Hiyo ndiyo tunataka nayo irekebishwe. (interjection). Eh, hatujapata.vyeti vya kumiliki mashamba Haya, naona hiyo inatosha. (interjection).

**Com. Lethome:** Haya, sema jina lako. Sema na sauti. (interjection). Sasa, unataka sheria iwe aje? Pendekeza.

**Kachi Kazungu:**

*(Dialogue between Com. Lethome and Kachi very faint)*

Free health services.

Free education upto secondary school.

**Com. Lethome**: Unajua mambo ya urithi? Urithi? Mwanamke akishaolewa ana haki ya kurithi mali ya baba yake ama unaonaje?

..

**Kachi Kazungu:** *(In Giriama dialect)*

**Translator:** Anasema hataki huo urithi (inaudible)

**Com. Lethome:** Na mashamba? Ana cheti cha shamba lake?

**Translator:** *(in Giriama dialect)*

**Kachi Kazungu:** *(in Giriama dialect)*

**Translator:** Yuasema,ana shamba lakini hana title deed.Sasa yuapendekeza hizo title deed ziwe issued

(Dialouge between Com Lethome and Kachi very faint)

Com.Lethome:Asante mama.Tumpate Sidi Naumbao.Sema jina lako.

**Sidi Naumbao**: Naitwa Sidi Naumbao

**Com. Lethome**: Haya, eleza mapendekezo yako.

**Sidi Naumbao*: (****In Giriama dialect*)

**Translator:** (inaudible)

**Sidi Naumbao:**

**Translator**: Na hospitali pia. The hospitals are far, so they would like hospitals constructed around.

**Sidi Naumbao**: *(In Giriama dialect)*

**Translator:** So, she is asking for free education because the fee is too high and they can't afford that. Primary and secondary education according to her,should be free.

**Sidi Naumbao**: *(In Giriama dialect)*

**Com. Lethome:** Na kuna mila za Wagirima ambazo pengine zinamgandamiza (inaudible)?

**Translator:** *(translates in Giriama dialect)*

**Sidi Naumbao**: *(In Giriama dialect)*

**Translator:** She doesn't like that idea of wife inheritance.

**Com. Lethome**: (inaudible)

**Translator:** *(translates in Giriama dialect)*

**Sidi Naumbao**: *(In Giriama dialect)*

**Translator:** She doesn't want that. O.K. She is asking for piped water. Kuna yingine? She doesn't have any more.

**Com. Lethome**: Christine Baya? Haya, endelea. Taja jina lako halafu unaendelea.

**Christine Baya**: Mimi naitwa Christine Baya. Matatizo yangu ni kama ifuatavyo: Kuhusu hizo karo za shule, huo ni mzigo kwa kina mama. Kwa kusema ukweli, utakuwa pengine una mtoto hapa secondary na kule primary. Sasa mzigo huu,utakuta huo ni mzigo wa kina mama, maanake tukisema ule ukweli, hata mzee pia hutoroka, ukabaki na ule mzigo tu wewe peke yako. Sasa uangalie primary unatakikana huko ulipe kama shilingi elfu moja, una watoto watatu. Haya ikiwa ni mia tatu tatu, hawa watoto watatu si ni mia tisa, hiyo elfu moja imebaki nini? Na huku unatakikana shillingi elfu nne,upeleke huku secondary. Unakuta hata manyumba yanaporomoka kwa sababu huna la kufanya. Sasa tunagandamizwa kabisa sisi kina mama, sisi huku, yaani Wagiriama tunagandamizwa sana, kwa vile ukizungumuza unaambiwa kwamba wewe umeolewa, huna mamlaka. Kwa hivyo tunapendekeza angalau huko shuleni, kama inawezekana, tusaidike. Kama bure, kama hivyo, hata kama watachukua kiwango cha chini angalau.Kama shilingi mia moja na hamsini, (Interjection). Form four, hapo siwezi kuwaingilia sana, sababu wanajua wenyewe..

Na kuhusu mambo ya barabara, nitapendekeza hivyo hivyo. Kina mama tunaumia, hapa hakuna mahospitali ya kutosha. Hivyo ukitoka hapo ukienda Dida, una-changewa pesa ndio upatiwe madawa. Kutoka hapa kwenda Vitengeni, ukifika kule ni pesa ndio upate hizo dawa. Sasa kina mama, wengi tunazalia hapa barabarani hapa. Pengine unakaa, umekesha, umeshindwa, unazalia hapa barabarani kwa sababu ndipo upande gari, ni asubuhi ya kesho ndio na ukifika hapa barabarani, unatingishwa, unazalia hapa hapa. Aibu! Tunasikia kusikitika sana sisi kina mama, kwa mpango kama huu.

Tunaomba kama inawezekana,tuwe na hospitali hapa,tupate matibabu ya bure ili tujisaidie sisi kina mama. Na lingine ni hivi, nitafuatiza vile mzee yule, sijui ni Ponda, vile alivyo- zungumuza kuhusu hawa wachaguliwa. Ikiwa ni kuchaguliwa, tunawachagua kweli, wakitoka hapo uchaguliwani, wanaenda. Wakati ule kabla hawajachaguliwa, wanatubembeleza. Lakini wakati tukiwachagua, ndio basi, unakuta mtu una mzigo kama huu wa shule, unafuata mtu ambaye umemchagua mwenyewe kwa sababu unasema baadaye atakuja kunisaidia kwa mzigo kama huu. Ukifika, anakwambia " Ho! Mimi nina hili, ngoja,". Unampatia zile kama ni fee structure hiyo, basi zinabaki kwenye mfuko mpaka wewe ni kwenda tu. Kesho, kesho kutwa, kesho, ama ana hamia huko Kilifi kwa county council huko, anasema "Kuna mikutano mingi". Wakati ukitaka kura, unakuja

hapa, wakati ukiwa umechaguliwa, kuna mikutano mingi. Kwa hivyo tunakuta sisi tunaumia wananchi. Tunapendekeza mtu anayechaguliwa ashugulikie zile masilahi ya wale waliomuchagua maanake umechaguliwa kwa sababu ujue shida za hao watu. (interjection). Ningependa mtu kama huyo tumtoe na tuchague mwingine.

**Com. Lethome:** Na kiwango chao cha elimu unaona kinatosha au?

**Christine Baya**: Kiwango chao cha elimu ni kama vile kufuatiza vile alivyosema yule wa kwanza. (interjection). Yeye, mtu kama huyo, kwa mfano awe kama ni wa Form four. Huyo ni councillor. (interjection). MP, huyo awe ni kama wa form six hivi.

**Com. Lethome**: ulipoanza kuzungumza ,ulisema kina mama,haswa wanamama wa kigiriama munagandamizwa sana.Hebu tueleze hayo magandamizo na pendekezo lako.

**Christine Baya:** Magandamizo yetu ni kama hivi. Pengine umeolewa na huyo bwana hana shamba, mumetengeneza shamba nyote, mumepata. Mumetafuta pesa mumepata, mumenunua shamba, munakaa pale na family yenu. Halafu baadaye huyo bwana kufa,, kunatokezea ndungu zake wengine kule. Wanakuja wanasema huu ni urithi wa kaka yetu, lazima tuuchukue. Sasa unasemekana kwamba wewe huna sauti maanake wewe ni muolewa, umefanya kuja kununuliwa. (interjection) Eeh! Ndiyo hivyo, tunaambiwa hivyo. (interjection). Ikiwa mume wangu amekufa, ninapendekeza kwamba nikae pale mahali, nirithi mimi na wale watoto wangu.

**Com. Lethome**:umezungumzia kuhusu habari ya wanawake kununuliwa.Hebu fafanua halafu utupe pendekezo

**Christine Baya:** Wanawake kununuliwa, yaani ndivyo wanavyosema, kwamba wewe huna sauti kwa sababu wewe umefanya kununuliwa kuja hapa, huna sauti kabisa! (interjection). Ni mali, si ametoa mali! Kwa sababu ametoa mali akampatia babako ndio sasa wewe huna sauti, maanake umefanya kununuliwa kuja hapa.

**Com. Lethome:** sasa ninyi kina mama wa kigiriama munaridhika na hayo?

**Christine Baya:** Haturidhiki! Ndiyo hivyo. tulikuwa tunaumia hivyo. Ninapendekeza jambo kama hilo liachike, la kusema ati tumenunuliwa.

**Com. Lethome:** Na kwa mfano unapoolewa ,mkiachana na mume wako na pengine mumekosana kabisa, mambo ya mahali inakuwaje?

**Christine Baya:** Tunarudisha, ndiyo. hata kama umezaa watoto ishirini, unarudisha tena hiyo mahari ndio unarudi kwenyu.

**Com. Lethome:** Ungependa hiyo mila ibaki vile.

**Christine Baya:** Ah, Ah! Hiyo mila na iachike. Kama imekuwa kama hivyo tumekosana, natuna watoto, kama inawezekana, yaani mimi ninapendekeza kama inawezekana, watoto hawa wagawe katikati, na mimi nipate. Na habari ya mahari iachike, kwa sababu sasa mimi naenda kwetu nikiwa niko hivi hivi. Na kubakishia hivyo wamesoma, pengine hata mimi ndiye nimefanya bidii.

**Com. Lethome:** Sasa hawa watoto,siutatenganisha hawa watoto na ndugu zao.

**Christine Baya:** Ndiyo, lakini hata pamoja na hivyo, napenda hilo kama litawezekana.

**Com. Lethome** Hebu tuambie kugandamizwa kwingine.

**Christine Baya:** Eh, ndiyo, kugandamizwa kwingine ni kama huo, na unaingia pale pale kwa urithi. Pengine mtu kama huyo, umetafuata pesa hizo na ukanunua hilo shamba si ndiyo? Wale watakaotoka kule, utaambiwa ukitaka uolewe na usipotaka utaolewa hivyo hivyo. Sasa unakuta shemeji wako mkubwa, yule ambaye ulikuwa ukimuita kama babako, yeye ndiye anakuoa. Unapenda uolewe, usipopenda uolewe. Ukikataa unaambiwa "Wewe fanya nini, ondoka hapa". Sasa jambo kama hilo, mimi naona lingeachika. Maanake ni aibu.

**Com. Lethome:** Kuna kugandamizwa kwingine?

**Christine Baya:** Kugandamizwa kwingine ni kama hivi, Kina baba, wametuacha nyuma sana. Yaani unakuta kugandamizwa huko, unakuta sasa wewe, kila jambo litakuwa ni lako. Kama ni nyumba, kama ni nini, yaani unagandamizwa kiasi cha kwamba, sasa sijui nieleze kivipi. Kwa sababu mambo mengi yanakuwa sana. Kwa mfano, bwana huyu ameoa bibi mwingine. Unaona, pengine anafanya kazi huko town. Anachukua huyu mama wanaenda huko. Unabaki wewe ambaye ndiye bibi mkubwa hapo. Pengine huyo bibi mwingine anakuja bila kushauriana kabisa. Eti "Wewe, huna mamlaka. Vile nataka mimi, vile nitafanya hivyo. Sababu wewe umekuja hapa kwa mahari, na huyu pia nitamuoa - - ninamuoa vivyo hivyo kwa mahari". Kwa hivyo unakuta unagandamizwa kwamba yeye anakaa kule, wewe unakaa hapa na kila kitu ni chako. Utatengeneza mji, utafanya nini, hiyo ni shauri yako na watoto wako. Sasa unakuta unagandamizwa hivyo. Huna njia ya kwamba unaweza kupitia angalau ukapate usaidizi wa kuotsha. Ukienda kule kwa chief, anaanza kukuambia, "Umenishtaki kwa nini? Sasa ndio utakwenda kwenyu kabisa". Mambo kama hayo yaachike! Hapo, kufikia hapo, nimefikia kikomo.

**Com. Lethome:** Asante sana kwa maoni yako,jiandikishe pale.Sasa tupate Harrry K Jefa.

**Harry K. Jefa:** Harry K. Jefa. Mimi, jambo la kwanza ambalo nitalizungumuzia ni juu ya wale madiwani. Nataka madiwani watakao-gombea udiwani, wawe wana kiwango cha elimu cha kufikia form four. Na ikiwa diwani amechaguliwa lakini hafanyi kazi yake sawa sawa, asiketi mpaka miaka mitano iishe ndio achaguliwe tena. Wananchi waweze kupewa mamlaka ya kuwachagua wengine ambao watafanya kazi nzuri.

Upande wa Bunge, mbunge akiwa na kiwango cha chuo kikuu, huwa ni bora zaidi, na yeye pia, ile miaka mitano ikiwa hafanyi kazi vizuri, wananchi waulizwe, ili wawe wanaweza kuchagua mwingine. Kuna jambo lingine juu ya President. Sijui kama nitakosea lakini nasikia President yuko above the law. Nafikiri hii above the law katika upresident, kama inawezekana, pia kifungu hicho `cha above the law, kiwe kinaweza kubadilishwa. (interjection). Kingine ni upande wa wazee wa sheria, Attorney General. Kuna sheria fulani ambayo watu huwa wanakosa kosa katika Kenya, basi kuna kifungu kiasema mpaka Attorney General's chamber iwe inaweza kukubali kama anaweza kushtakiwa yule mtu. Kile kifungu, kile ninaona kina hali ambayo mtu akiwa amekosa, iko court. Si court wanaweza tu wakaweza kuzungumuza kuliko kungoja mpaka yule atoe idhini? Siku nyingine akikataa kutoa idhini, basi wale watu hawatashtakiwa. Kwa hivyo, hicho kifungu hicho, kiondolewe.

Upande wa urithi hasa wa mashamba, wajua mila hizi za kienyeji mara nyingine huziona hazipendezi- lakini mimi napendekeza ikiwa mtu ameselewa,ni mumewe na yule mke yuko pale na watoto wake. Mila ya Kigiriama mara nyingine wanasema kuwa achukue yule ambaye ashauchukua ufa, ufa ikiwa inawezekana pia utoke. Na ile ardhi ambayo ni shamba ya yule aliyefariki, iandikishwe yule mke, si wale watoto, Kwa sababu ukianadiksha watoto watasumbuana. andikishwe yule mke. Mimi yangu nilikuwa nimebeba ni hayo.

**Com. Lenaola:** Ungependa serikali ya aina gani?serikali ilioko ama serikali ya mikoa ya majimbo?

**Harry K. Jefa:** Mimi kwa sababu sijachunguza chunguza sana, lakini serikali ilioko, mimi kwangu si mbaya. Na hii multiparty ijapokuwa wengine wanazungumuza hivi na hivi, lakini hiyo pia lazima iweko kwa sababu itakuwa kidogo, anayekosea huambiwa. Lakini ikiwa ni yeye ni yeye, basi hatujui kuwa yanaendeshwa namna gani. Basi multiparty pia iko.

**Com. Lenaola:** Sasa tuna vyama 48 katika nchi ya kenya ungependa zibaki hizo nyingi au zipunguzwe?

**Harry K. Jefa:** Mimi ningependa ile ambayo ikiandikishwa, tuangalie watafanya nini lakini hatuwezi kusema kiwango ni lazima huwa vyama vya upinzani, ama vyama visipewe vyeti tuseme hapa ndio imetosha. Wale watakao kubali ku-register, wawe registered. Wananchi wenyewe wataangalia kama hii ya faa, haifai, watachagua.

**Com. Lethome:** Asante bwana Jefa.Jiandikishe pale.Tumpate Fracis Garama.

**Francis Garama:** Jina ni Francis Garama. Mimi nazungumuzia kwanza upande wa Rais. Ningeomba Rais kutawala muda wa miaka kumi na pia naomba Rais awe above the law. Na standard of education ile naomba at least ikiwezekana kuwa Form six. (interjection). Mimi nasema ile standard isiwe juu sana. Anaweza kuwa Form six ama form four. Na upande mwingine, narukia upande wa barabara. Barabara nataka au naomba ikiwezekana, kuwekwe lami. Tuna taabu sana sisi .Wakati wa mvua, tuna shida sana. Na hospitali tunazitaka hapa Matanomane. Nashukuru ni hayo.

Com. Lethome:Asante.Jiandikishe pale.TumpateKatana Kazungu Kiti

**Katana Kazungu Kiti:** Mimi sina mengi ya kusema isipokuwa …(interjection). Katana Kazungu Kiti. Mengi sina sana isipokuwa ulalamishi ni kuhusu hizi hospitali. Hospitali zetu ndizo ambazo kwamba zinafanya hatuendelei sana kwa sababu ukienda hosptali, lazima mpaka uwe na pesa. ikiwa huna pesa, wewe utabaki nyumbani. Mimi ningependa hizo hospitali ziwe za bure. (interjection). Hospitali hazitoshi. Napenda ziwe nyingi. Ziko mbali,naomba ziwe karibu. Na upande mwingine ni upande wa shule. Watoto wetu unafunza kutoka darasa la kwanza mpaka darasa la nane, na mtoto aki-pass, hapo basi, mbele mzazi aweza kushindwa. Ningependelea huko mbele tusaidiwe, ziwe za bure. (interjection). Akimaliza darasa la nane.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo secondary iwe ya bure?

**Katana Kazungu Kiti:** Eh, iwe ni bure.

**Com. Lethome:** Na chuo kikuu?

**Katana Kazungu Kiti:** Na chuo kikuu pia. Kwa maana hapo basi ndio mzazi hushindwa hapo. Na kwa hapo, hii serikali tuliyo nayo ni sawa. Hii ya KANU. (interjection). Ni sawa. Yenyewe, hapo ni makosa kwa maana hata ma-sub-chiefs yafaa wachaguliwe Wale, kwa maana vile wao ni wa sehemu za juu kule, si sana lakini hao viongozi walio hapa, wachaguliwe.

**Com. Lethome:Na** mfumo wa serikali uliopo sasa huwa tuna serikali ya umoja wa kitaifa ambayo iko Nairobi.Mambo yote yako Nairobi. Sijui ungependelea mfumo huo ubaki hivyo hivyo au serikali itawaze na ije karibu na wananchi.

**Katana Kazungu Kiti:** Ningependa iwe karibu karibu.

**Com. Lethome**:sasa ungependekeza mfumo gani ?unajua kuna mifumo tofauti ambayo inaweza kuwa na serikali tofauti , labda serikali ndogo na serikali kuu ,nyengine ni majimbo.ungependekeza nini

**Katana Kazungu Kiti:** Huo wa majimbo mimi haunipendezi, isipokuwa huu wa KANU ndio mzuri.

**Com. Lethome:**Na sasa kuna vyama vingi. Ungependelea kuwe na vyama vingi ama tuwe na chama kimoja.
**katana Kazungu Kiti:** Chama kimoja. Cha KANU.

**Com. Lethome:**Asante sana bwana kiti. Tumpate Henry Karabu . Anzia jina lako na uendele.

**Henry Karabu:** Jina langu naitwa Henry Karabu Mulewa. Pendeleo langu, ninapenda baada ya ikiwa mashamba yetu yameshapimwa na watu wa land, iwe wale ambao kuwa huwa wana kesi zao za mashamba, wawachwe lakini sisi ambao kuwa tulishatumiwa kabla kesi, tuwe tunaweza kupata karatasi zetu za title deed.

**Com. Lethome:** Ulisema mashamba yakisha pimwa.Yashapimwa?

**Henry Karabu:** Eh. Yalipimwa tayari.

**Com. Lethome:** Sasa tatizolinatoka wapi?mbona hamjapata title deeds?

**Henry Karabu:** Tatizo ni kuwa hatupati zile karatasi zetu za title deed, ni kwa sababu cases zilikuwa nyingi, sasa wale wenye kesi …

**Com. Lethome:** Endelea

**Henry Karabu:** Na pili, hili nikusema kwamba tunataka ule mkahawa wetu ambao kuwa tunaita kwetu ni pombe, iweze kuruhurusiwa kama zamani kwa sababu imekuwa ya kwamba, hata askari hawawezi kufanya kazi nyingine. Hata wezi wakiingia hawawezi kushika wale wezi, kwa sababu wao wanapata kazi ya pombe tu. Mtu akionekana na pombe anashikwa aende. Kwa hivyo mwizi anaiba.

**Com. Lethome:** Pombe ya aina gani?

**Henry Karabu:** Pombe ya mnazi. Na ule ndio mkahawa wetu ambao kuwa tuki –uza uza. Kama tunaweza kufunguliwa vile vilabu kama zamani, ndio tuweze kupata pesa tukapeleke watoto wetu mashule waendelee .

Tatu nikusema kwamba tunataka Rais wetu awe wa Pwani. Sio tuwe tu na Rais wa mbali, bara huko. Tunataka tupate Rais wetu wa Pwani. ili ikiwa tuna matatizo, tuwe tunaweza kutatua haraka.

**Com. Lethome**:Una kusudia kusema nini kuhusu huyu Rais wa Pwani?Unapendekeza mfumo wowote wa serikali?kukiwa na Rais wa pwani,sehemu zingine zitatawaliwa na nani?

**Henry Karabu:** Sisi, ninavyo pendekeza mimi, tunataka KANU kama sehemu zingine hizo huko, wawe wataweza kupata Rais wao lakini hapa Pwani, tuwe tuna Rais wetu kabisa.

**Com. Lethome:** Sasa hiyo sehemu itakuwa ni kama jimbo, ama itakuwa ni mkoa ama vipi?

**Henry Karabu:** Itakuwa ni Mkoa wa Pwani.

**Com. Lethome:** ... Na je,tutakuwa na Rais wa Kenya nzima baada ya kuwa na marais wa kila eneo? Unapendekeza tuwe na Rais wa Kenya nzima ama vipi?

**Henry Karabu:** Tunapendekeza tuwe na Rais wa Kenya nzima. Mambo mengine ni kama yale yamezungumuziwa na mwenzangu lakini ni kama kuongezea, katika sehemu za upande wa mashule. Tunasomesha watoto wetu, wanaenda mpaka wanakwama. Wakifikia darasa la nane, mbele huwa tunashindwa kwa sababu ya uhasifu wetu wa pesa. Tungeliomba angalau

kama tunaweza tukaletewa kampuni karibuni, huku kwetu, iwe wale watoto wetu wanaweza kujitolea wakapata kazi za kampuni, ili wawe wataweza kusaidia wale wenzao ambao wako mashule maanake kuna wengine wanasoma, wanashindwa na pesa,na kampuni za kufanya kazi hakuna. Mpaka waondoke hapa mpaka Mombasa, ama wapi. Ukazunguke, tena ukipata pahali kuna- andikwa kazi, mpaka uwe na pesa mfukoni ndio uwe na uwezo wa kuchukuliwa kwa kazi. Ukiwa huna pesa, una –achwa, anachukuliwa mwenye pesa. Lakini tukiwa tuna kampuni nyingi huku kwetu, zitaweza kutusaidia.

**Com. Lethome:** Ungependa makampuni ya aina gani?

**Henry Karabu:** Ziko kampuni kama za mbata tukiletewa tunaweza kutengenezea mafuta mnazi tuko nayo nyingi huku. Kuna kampuni za korosho, korosho tunapata, tukifunguliwa tunaweza kuendelea.

**Com. Lethome:** kitu kingine ni elimu.sasa elimu hii inawashinda wazazi kwa sababu ya malipo ya juu .ungependekeza nini juu ya malipo?

**Henry Karabu:** Ningelipendekeza ile malipo kama ya kwenda secondary, iwe inaweza kupunguzwa ikawa kiwango cha chini ili tuwe tunaweza kuendeleza watoto wetu kimasomo.

**Com. Lethome:** Haupendelei ya bure?

**Henry Karabu: T**ukisema kwamba tutaweka bure kabisa, tutakuwa hatuwezi kujenga mashule yetu lakini hiki kiwango kikipunguzwa, tunaweza kumalizia wale watoto wa form four, wakienda university, huko tunataka serikali iweze kutusaidia wakamalizia huko. Hapo - - nitakomea hapo.

**Com. Lenaola:** sikuelewa sawa yale mambo ya President kwa kila region. Ungetaka kuwe na serikali ya mkoa au serikali ibaki vile ilivyo,ya serikali kuu kule Nairobi.

**Henry Karabu**: Serikali yetu tunataka iwe ya Mkoa wa Pwani.

**Com. Lethome:** Tupate sasa Katana Mulewa:

**Katana Mulewa:** Mimi sina maoni mengi lakini maoni yangu ni kwamba, ningetaka kwamba wakati tunakuja uchaguzi, tuchague yule mtu ambaye tunamuona anafaa

**Com. Lethome:** (inaudible)

**Katana Mulewa:** Ambaye anaendelea tayari, penginetusichague mtoto tuanze kupanda tuanze tena. kile kitu ambacho tumepanda bado tunataka kuvuna, tuendelee na ile ,ndivyo nitakavyo.

**Com. Lethome:** Ngoja kidogo Wasema tuchague mtu ambaye ni sawasawa na mwenye sifa gani Kwa mfano kwa elimu

amefikisha kiwango gani? Unataka aje?

**Com. Lenaola:** Umesema akisha chaguliwa kama councillor, MP,President,unataka achaguliwe na kiwango gani cha elimu.

**Katana Mulewa:** Councilor, tunataka tupate kama mtu ambaye angalau amefika form four. Na mbunge, tupate yule ambaye anatufaa, tukichagua kitoto ambacho kitatuharibia …

**Com. Lethome:** Umri gani?

**Katana Mulewa:** Kama amefikisha miaka thelathini ama arobanne.

**Com. Lethome:** Na umri wa juu kabisa? Uwe kiwango gani?

**Katana Mulewa:** Umri wa juu kabisa, uende mpaka hamsini.

**Com. Lenaola:**miaka hamsini?kwa hivyo akipitisha miaka 50 anafaa asichaguliwe?

**Katana Mulewa: A**nafaa, maanake ni mzee ule ambaye ana maoni mazuri.

**Com. Lenaola:** umri wa juu zaidi uwe ni umri gani?

**Katana Mulewa:** Kama hamsini, sitini, sabini basi hiyo inaweza kuwa inafaa.

**Com. Lenaola:** Unataka sabini, sabini mwisho? Mtu wa miaka sabini na moja asichaguliwe?

**Katana Mulewa:** Anachaguliwa maanake tumeanza hii …

**Com. Lethome:** Tuambie kiwango cha juu, tuambie kutoka miaka thelathini mpaka miaka tisini, miaka arobanne mpaka miaka sabini, tuambie kiwango hicho.

**Katana Mulewa:** Kiwango hicho? Mpaka tisaini na tisa.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo kama mamanguana miaka 90 na akitaka kura,tunampigia kura? Na kiwango cha elimu cha MP, kwa sababu kiwango cha elimu cha councilor umesema form four. MP awe na kiwango gani cha elimu?

**Katana Mulewa:** Kama form 6

**Com. Lethome:** Na President je?

**Katana Mulewa:** Hii miaka yake?

**Com. Lethome:** Ya kuanziaPresident ungependa awe na miaka mingapi?

**Katana Mulewa:** Hata kama tisaini na tisa pia. Ya chini, tunaweza kuanzia hamsini mpaka tisaini na tisa.

**Com. Lethome:** Na kiwango chake cha elimu?

**Katana Mulewa:** Elimu itakuwa kama form four.

**Com. Lethome:** Aendelee kwa muda gani?Tumchague kwa kipindi gani?au vipindi vingapi?

**Katana Mulewa: A**endelee kama ile miaka mitano, ikiwa anatufaa tutamuwekea tena nyingine(interjection by Com. Lenaola). Eh, MP.

**Com. Lethome:** Hata kama ni mara 3,4,5 au…

**Katana Mulewa:** Hata kama ni mara kumi. Na jambo la pili, huku kwetuwakati wa kuandikishwa mashamba, huwa mashamba mengine yana case, na yale mengine ambayo hayana zingine ambazo hazina case, tunataka, tupatiwe,vyeti vyetu wale waendelee mpaka wamalize. Naona nimefikia hapo.

**Com. Lethome:** Asante bwana Katana.Jiandikishe pale.Kazungu Baya .Sema jina lako

**Kazungu Baya**: Kazungu Baya. Mimi ningependelea sub-chief yeye apate kura, apigiwe kura.

**Com. Lethome:** Na chief?

**Kazungu Baya**: Chief vile vile tumpigie kura. Na hawa askari hawa, mimi nimeumia bure, tena yeye anataka pesa kwangu, na mimi nimeibiwa Hawa asakari wanatuumiza. Mimi nimeibiwa, tena yeye anakuja kutafuta pesa ndio atafute wale watu. Yeye ni mtumishi, si anitumikie vile ambavyo? Ndivyo vilivyo? Kwa hivyo, wale askari wanatuumiza.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini?

**Kazungu Baya**: Ninge- pendekeza hivi, wale wapigiwe kura, hawa ma-chief na ma-subchief, na hawa askari waache vile wafanyavyo.

**Com. Lethome:** Kwa mfano askari akikuitisha pesa ndio akuhudumie ,unaweza kumshtakiwapi?

**Kazungu Baya**: Huyo police? Nitakwenda kule kwa chief.

**Com. Lethome:** Unaweza kumshtaki kule kwa chief? Na ukimshtaki, kuna hatua yeyote atachukuliwa?

**Kazungu Baya**: Atachukuliwa na chief.

**Com. Lethome:** Hivi sasa hali ilivyo, umedhulumimwa na askari polisi, si ndiyo? Badala ya kukuhudumia anataka pesa. hongo kutoka kwako. Kawaida ukienda kulalamika kwa chief, chief huchukuwa hatua yeyote?

**Kazungu Baya**: Chief atachukua hatua. Mimi sina mengi ni hayo tu.

**Com. Lenaola:** Umesema kwamba chief na naibu wake wachaguliwe na wananchi? Na je DO, na DC, na PC? Wale wengine wakubwa,wachaguliwe?

**Kazungu Baya**: Wale vile vile wachaguliwe.

**Com. Lethome:** Asante .jiandikishe pale.Tumpate Kahindi Yeri.

k**ahindi Yeri:** Mimi naitwa Kahindi Yeri. Mimi maoni yangu, ninasema hivi. Kwanza, utawala wa chief, sub-chief, DO, DC, PC, hawa wote sisi tunataka wawe wanachaguliwa. Pili, katika skuli, sisi tunataka skuli, hata serikali yenyewe imesema juzi kuwa watoto kutoka class cha kwanza mpaka class cha nane, wawe wanasoma bure. Na hata mimi pia napendekeza hivyo, maanake maskini wengi wale watoto wao hawasomi kwa sababu ya karo ya skuli. Lakini ikiwa ni bure, hata wale watoto wa maskini watasoma. Kwa hivyo napendekeza hivyo.

Tatu, ni hali ya afya. Afya, hospitali, sasa hata bila pesa wewe huangaliwi. Kama sisi maskini, tunakufa tu katika hospitalini kwa sababu ukifika pale, wewe huangaliwi mpaka utoe pesa, na sisi maskini hatuna pesa. Ikiwa inawezekana, hospitali iwe bure kabisa, iwe free. Hata maskini naye anataka kuokolewa.

Nne, kuna mjadala ambao hata sasa uko Bunge. Mjadala huo ni shauri ya huduma ya nyumbani ya wanawake. Ikiwezekana, tunataka ile huduma iwe inachukuliwa na serikali tu peke yake sio kuingiliwa na watu wa siasa. Mtu na bibi yake, vita vya bibi na bwanake, viwe ni vya mtu na bibi yake na mwisho wake ni katika huduma ya serikali. Wenyewe wakifikishwa kortini iwe huduma ile inakwisha, siyo kama vile ichukuliwe na watu wa siasa. Mimi nitakomea hapo.

**Com. Lethome:** Asante sana. Jiandikishe pale. Kadenge Menza?

**Kadenge Menza**: Mimi naitwa Kadenge Menza, na ningetaka watu wa KANU wapate nguo zao pamoja na tie zake. Wapate nguo zao, uniform zao pamoja na tie zake. Na napendelea hivi, mimi niko na licence yangu, na nilikwenda kwa company moja ambayo inaitwa Glana Range. Nilipofika hapo, tulikuwa watu wawili. Mimi, Mgiriama na Mbaluyha mmoja. Kuangalia kwa driving licence yangu kwamba nina-qualify nilipatiwa gari hapo ambayo niliendesha.Na nikaipeleka vizuri sana,

nikaja nikaiweka. Nilipoiweka, akachukua Mbaluya, hakwenda nayo vizuri na baadaye wakati wa kuchukuliwa, akachukuliwa yule Mbaluyha ambaye hakuendesha vizuri ile gari. (interjection). Kwa hivyo juu ya
Wajri ingependekeza watu wa bara wawe wanafanya kazi kwao, Mkoa wa Pwani, wawachie watu wa Pwani wafanye pwani. Hiyo ndiyo nilikuwa na pendekeza.

Ya pili, ningependekeza mpango wa hospitali. Ikiwa ni hospitali ya government, hospitali hiyo ukienda una-charg-iwa senti na wengine hawana pesa. Hata hivi niko na ndungu yangu ambaye kwamba inatakikana niende nikamtoe kwa shilingi elfu moja hospitali kwa sababu ya gharama ya kitanda. Kwa hivyo sina mengi isipokuwa ni hayo tu.

**Com. Lenaola:** Sasa ungependa malipo ya hospitali yawe aje?
**Kadenge Menza**: Nataka hospitali iwe hatulipi pesa.

**Com. Lethome:** Christine Charo?

**Christine Charo**: Christine Charo. Jambo la kwanza kabisa ni kuhusu barabara zetu kutoka Kilifi mpaka huku. Barabara ni ovyo, chafu kabisa, na tena hospitali si za karibu hivyo.

**Com. Lethome:** Mambo ya barabara unapendekezaje?

**Christine Charo**: Ningependa zitengenezwe, ziwe nzuri za kupitika. Jambo lingine ni kuhusu hospitali. Hospitali zetu ziko mbali. Ningependa ziwe za karibu, tena ambazo hazina malipo, sababu mimi nitakuwa pengine sina pesa na mtoto wangu anangojeka, sijui nifanyeje. Na nikifika kule ni mapeni, Kwa hivyo hospitali zetu jameni.

Jambo lingine ni ubaguzi wa wasichana, hata wale watoto wadogo wasichana ambao wanaanza kukua vile. Hawapelekwi shuleni kuelimika. Yaani wanabaguliwa hivi na wazazi wao

**Com. Lethome: Unapendakeza nini?**

**Christine Charo:** Ningependa hiyo elimu iwe ya kila mmoja, mvulana na msichana. Jambo lingine ni kuhusu mashamba yetu. Imekuwa ni wimbo kuhusu title deed, kugawanywa kwa mashamba. Hatugawanyiwi kabisa, tukapata zile title zetu, nambari zetu hatuzipati. Ningependa hiki kilio kifike huko, kisikike.

Jambo lingine ni kuhusu walimu wa nursery. Waalimu wa nursery, ningependelea walipwe na serikali si wazazi. Jambo lingine ni kuhusu pombe. Wazee wetu wakishaenda kulewa, huwa wanasahau hata familia zao nyumbani. Ningependa pombe kama

inawezekana, ipigwe marufuku.

**Com. Lethome:** Hii ya mnazi hii?.

**Christine Charo:** Hii ya mnzazi

**Com. Lethome:** Sikizeni, tukubaliane asubuhi kwamba, ni lazima kuyaheshimu maoni ya kila mtu**. S**asa sheria zetu hapa ni kuwa mtu ana uhuru wa kutoa maoni yake bila kusomewa, bila lolote. Hayo ni maoni yake, ni mapendekezo yako, na ni haki yake ya kikatiba. Nafasi yako ikifika, na wewe sema utakavyo. Yeye ameona pombe ipigwe marufuku. Wewe ukipata nafasi njoo hapa (interjection). Yote tunachukua, yote yanasajiliwa, hayo ni maoni ya mama, yaheshimiwe.

**Christine Charo:** Jambo lingine ni kuhusu viongozi wetu. Pengine kuna weza tokea kazi sehemu za huko nje, sisi tuko huku tayari tunangojea tu hiyo nafasi tusikie basi huko kuna kazi yetu. Hutasikia mpaka utafanya kusikia basi kuliingia tayari mtu mwingine, na si mtu wa kuwa ati ni wa hukuwa area hizi za huku kwetu. Pengine ni wa kutoka bara huko, pengine ni wa kutoka Ukikuyuni huko. Utamkuta tayari anafanya kazi. Wewe hapa unangoja unangoja na ni mtu pengine hata una elimu zako na tena ushaachwa. Kwa hivyo, jambo hili, litiwe maanani. Ningependa kama ni kazi imetoka, wachukuliwe. Hakuna cha ubaguzi. Kila mmoja ni binadamu.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo ungependa pia kazi za hapa hapa zisipewe watu wa kutoka bara.

**Christine Charo:** Eh, zipewe hapa hapa. Jambo lingine ni kuhusu chiefs, assistant chiefs na wale viongozi wengine kama councillors. Hao councillors, tayari hawa wanapigiwa kura lakini tungependa hawa chiefs na assistant chiefs wawe wa kupigiwa kura.

**Com. Lethome: C**ouncillors umesema wanapigiwa kura tayari kama wengine. Na kiwango chao cha elimu unaridhika nacho?

**Christine Charo:** Kiwango chao cha elimu siridhiki. Ningependa iwe kama ni form four kuendelea juu.

**Com. Lethome:** Na MPs, elimu yao unaniudhi nayo?

**Christine Charo:** Wabunge nao, hao nariudhika.

**Com. Lethome:** Elimu yao unanidhika hata kama amefika standard eight ama standard four au hayasoma kabisa?

**Christine Charo:** Ah, huyo wa kutosoma kabisa, basi siridhiki naye. Ningependa hata kama ni form four, hiyo ni afadhali.. Jambo lingine ni kuhusu hivi vikundi hivi. Kuna vikundi vingi na vingi, hasa za vijana, vya wakina mama, hivyo vyote

vimezoroteka, hakuna maendeleo yeyote huko kwetu ambayo yako kuanzia sasa. Kwa hivyo ningependa hivyo vikundi vifufuliwe.

**Com. Lethome:** Nani ativifufua hivyo hivyo vikundi? Si vikundi hutengezwa na watu wenyewe. Nani wamevivia na nani wavifufue.

**Christine Charo:** Hivyo vikundi, kuna wengine hao tayari wako ngazi za juu halafu kukurika huku na huku, huku na huku. Ili kama ni pesa hizo zimetolewa, hao tayari ndio wanakazi tena, wanachukuwa tayari hizi pesa ambazo wakina mama wanachangia, wao wao tena watafaidika.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo ni viongozi ndio wameviua si ndiyo? Viongozi ndio wamevivua, kwa hivyo wapendekeza wafanye nini?

**Christine Charo:** Virudi, vifufuliwe.

**Com. Lethome:** Halafu viongozi wale pesa

**Christine Charo:** Hao viongozi basi watafutiliwa mbali.

**Com. Lethome:** Una pendekezo lingine?

**Christine Charo:** Sina lingine.

**Com. Lethome:** Umezungumzia maneno ya watoto wanawake kubaguliwa Na je, wanawake, kwa sababu hawa watoto wa kike ndio baadaye wanawake wanakuwa wanawake wanaonewa. Kuna ubaguzi wowote kuhusu wanawake? Wanabaguliwa katika sehemu hii.

**Christine Charo:** Wako, wanabaguliwa.

**Com. Lethome:** Munabaguliwa nyinyi kina mama?

**Christine Charo:** Kubaguliwa na hao wazee wenyewe? Wako wanaobaguwa.

**Com. Lethome:** Wanabagua kivipi? Tupe mfano.

**Christine Charo:** Kwa mfano hivi umekosana na huyu Bwanako, atakupiga. Pengine akupige mpaka aseme "Nenda, kwanza wewe ulikuja kitupu hapa, ishia kwenu uende zako". Na wewe utabakia tu hapo.

**Com. Lenaola:** Na unaweza humchukulia hatua?

**Christine Charo:** Eeh, unachukua hatua. Sasa ukifika kule kwa chifu, jambo la kwanza utoe pesa pale, umpe chief ndio aanze kushughulikia yale maneno maneno, na wale wazee wa kijiji pia.

**Com. Lethome:** Ungendekeza nini? Ungependekeza case za magogoni?

**Christine Charo:** Mimi ninependekeza hizo case za magogoni kama zitakuweko, lakini nikifika kule na kilio changu, kichukuliwe kile kilio, si kuwa kichukuliwe kilio hakina maana.

**Com. Lethome:** Ungependa vikao vya magogoni viendelee au vaichwe?

**Christine Charo:** Viendelee.

**Com. Lethome:** Wawe wakiasikiza tu?

**Christine Charo:** Eh, wanasikiza tu kilio cha mtu binafsi. Sina mambo mengine.

**Com. Lethome:** Asante Christine Charo. Jiandishe pale. Grace Sanga.

**Grace Sanga:** Kwa majina yangu naitwa Grace Sanga. Maoni yangu ya kwanza nitatoa juu ya watoto, yaani wanafunzi na ninapenda kwamba kuwe na Tume ambayo ingeweza kutetea wanafunzi, yaani watoto wanaosoma shuleni, Tume hii iwatete kwa njia ya, kutafuta njia ya kuwa na maktaba shuleni, ili watoto wambao wazazi wao hawana uwezo wa kuwanunulia vitabu, waweze kupata kufahamu kupitia kwa vitabu vile, na baadaye wakimaliza class cha nane, wale wenye ufahamu wa kadiri, (maana najua wale wenye ufahamu wa juu, pengine husaidika baada ya kumaliza class cha nane), lakini wale wenye ufahamu wa kadiri, waweze kuchukuliwa maanane pia, kwa kujengewa vyuo vya ufundi. Serikali ione ya kwamba kuna vyuo vya ufundi kwanza huku mashambani zaidi. Maana wako watoto wengi wanaomaliza class cha nane, na inakuwa vigumu kwao kwenda secondary kwa hali ya udhaifu wa pesa.

Na oni langu lingine ni serikali itafute njia ya kuletea watu wa mashambani wanunuzi wa vitu vyao. Yaani kuwe na soko lakini tuletewe matajiri wa kutununulia vitu vyetu, kama vile mifugo, au vitu ambavyo vingeweza kutengenezwa na akina mama wa maendeleo, kama ushonaji wa vitambaa, vikapu, hata majamvi, ili kutafuta njia ya wakina mama waweze kupata pato kutoka humu humu. Katika soko hiyo, itawawezesha hata wazazi wengine waweze pia kufundisha watoto wao katika hivyo vyuo

vitakavyojengwa kama serikali itapendekeza.

Upande wa afya ningependa ya kwamba, pia kama ingewezekana kuwe na Tume ya kuchunguza, kutoka huku ndani ndani zaidi. Wakati jamii inapoingia katika hosptiali za kawaida na kupatikana pengine wana ungojwa ambao unahitaji pesa zaidi ndiyo watibiwe, serikali iwachukulie maanani kwa ajili ya kuwatibu wale wananchi

**Com. Lethome:** Kwa hivyo ungependa hayo matibabu yawe ya kulipwa ama.

**Grace Sanga:** Yawe ya malipo lakini kwa ugonjwa ambao huwa unajulikana huo, basi mtu akichunguzwa na kupatikana na ugwonjwa kama, nitasema labda T.B., au cancer, yaani ugonjwa ambao unajulikana huo kwa njia yeyote mtu anahitaji matibabu. Serikali angalau igharamikie zaidi kwa yule mwananchi atakayekuwa pengine hana uwezo ili apate tiba.

Upande wa vile tunavyo ongozwa na viongozi wetu, ningesema ya kwamba uongozi hauna neno lakini tunaombi. Ombi letu ni kwamba kama kungelikuwa na party fulani, ya mtu fulani ambaye atawasukuma wale viongozi ya kwamba, waweze kuhudumia jamii vilivyo, yaani kama ni mfano tu kama sub-chief vile, mamlaka yake jinsi yalivyo. Basi kuwe na mwenzake ambaye ni mkubwa wake, atakayeweza kumskuma mpaka aweze kupenya katika jamii kule ndani na kuwasaidia vilivyo. Kwa mfano, kama kuwaita katika mikutano na kuwapatia mawazo katika jinsi ya kujisaidia mpaka kujimudu. Mawazo, yaani kuhamasishwa katika kimaisha ijapokuwa nchi hii iko hivi. Lakini mnaweza kufanya hivi mkajiinua. Sasa, wale viongozi wetu wawe na mtu wa kuwasukuma ili waingie sana kule ndani. Maana hawaingii, tunawatamani kule, waje wakizungumuza nasi lakini si umfuate ukiwa na shida, tena ikugharimu ili uhudumiwe.

**Com. Lethome: U**napenda vile hawa machifu wanavyoteuliwa?

**Grace Sanga:** Mimi naridhika, kama kutatokea hiyo Tume ya kuwasukuma watuhudumie, watupatie haki zetu ambazo zinatustahili tupate kutoka kwao.

**Com. Lethome:** Hupendekezi wachaguliwe?

**Grace Sanga:** La, ina wazo hilo kwa wakati huu. Haya. Upande wa kuajiriwa, yaani uwajiri upo, na unaendelea hata huko mijini lakini sisi tuna kilio kama watu wamashambani. Kuna wapendwa wengine wana hata ujuzi wakujenga, wengine hata hiyo capentry wakijifundisha jifundisha wana ujuzi kidogo na wakina mama wengine hata ujuzi ujuzi wa ofisini kama vile kupiga chapa, lakini ile hali ya wanaume zao wakinunua mashamba huku, shambani ama vijana wakimaliza kujifunza hiyo capentry au masonry wakirudi huku nyumbani ndani ndani hawana uwezo au nafasi ya kupata kuajiriwa. Maana uajiri ni mgumu siku hizi, ninavyo zungumza ni kwamba ni lazima mpaka ujulikane, tena ugharimike sehemu fulani ndiyo uajiriwe. Sasa hivi, tunataka tu - - wapate haki zao. Aliye na ujuzi nao uweza kumpa kazi, serikali iweze kuchunguza hapo, hata huyo naye apate kazi.

Sasa upande wa haki za watoto wa kike, tunaomba ikiwezekana kuwe na Tume ambayo itakuwa inatetea wale watoto wa kike katika elimu. Watoto wa kike hutolewa shule, wakaozwa hata kwa siri. Ikitokea dhahiri ni kweli, viongozi hutoa hatamu zao na kuendelea. Lakini hata kwa siri wanaozwa na kutolewa shuleni na wanaozwa kwa watu wazima ambao si marika yao kabisa au nyumba ya pili. Mtoto mdogo aozwe nyumba ya pili au ya tatu. Azalishwe, tena yeye alime kipande, ajilishe yeye na yule mtoto. Maisha magumu, kutoka mwanzo aendelee mpaka either mwisho afe, amkimbie yule mzee akaolewe na mwingine alipe mali, yaani wanatumiwa kama biashara. Yaani mtoto wa kike ni kama biasahara, auzwe huku, kama hawezi kuishi huku, atafutiwe mume ajiuze kule, alipe huku namna hali, hawana haki watoto wa kike. Na wakina mama katika nyumba zao, wapatiwe haki yaani hata kwa makosa yanapotokea, kuwe kuna njia ya kuweza kuwatetea kosa lile lisuluhiswe kwa njia nzuri, kuliko kupigwa hata mama wa mimba apigwe hata akijulikana, basi aende hospitali mimba itoke. Halafu tena wanapatanishwa wanarudiana na yule mumewe, ijapo labda alikosa. Lakini kuwe na njia nzuri ya kusuluhisha makosa, yaani kuwe na kamati ya kuweza kusaidia jamii, yaani mama na baba kwa wakati kukitokea makosano fulani.

**Com. Lethome:** kuhusu huku kuozwa mapema, ungependekeza nini?

**Grace Sanga:** Mimi ningependekeza waozwe wakati wamefika umri wa angalau zaidi ya miaka kumi na nane, wawe wana nafsi ya kuweza kuwaza na kujiamulia.

**Com. Lethome:** kwa hivyo unapenda kuozwa mapena kuypigwe marufuku?

**Grace Sanga:** Ndiyo

**Com. Lethome:** Kuhusu wanawake kipigwa na mumewe, ungependekeza nini?

**Grace Sanga:** Mimi? Yaani asipigwe hata kama kuna kosa gani amefanya, kuwe kuna mahali ambapo wanaweza wakazungumuza wakasuluhisha juu ya hilo tatizo ambalo lingemfanya apigwe.

**Com. Lethome:** Na mambo ya mume kupigwa na mkewe?

**Grace Sanga:** Si saana haitokie sana.

**Com. Lethome:** (inaudible)

**Grace Sanga:** Na ikiweko pia huyu mume awekewe haki zake ili asije akaumizwa sana.

**Com. Lethome:** (inaudible)

**Grace Sanga:** -- asimpige mume, kuwe na haki.

**Com. Lethome:** Lingine?

**Grace Sanga:** Lingine ni upande wa vikundi. Yaani kama ingewezekana, serikali ikatafuta njia ya kusaidia vikundi vya huku ndani ndani ili ule uongozi wake uwe unastahili maana uaminifu ni kidogo, ndiposa hata tukichanga, tunataka tufanye jambo fulani kidogo vile wale wenzetu ambao wako mbele, wanaanza kuingiwa na hali, halafu ile hazina hivi inaharibika. Kuwe na kamati ambayo ingeweza kusimamia vile vikundu kwa wale viongozi kuona ya kwamba ni waaminifu ili chochote kitakacho changiwa na jamii kiwe katika hali ya usalama. Namna kama hiyo.

Na ijapokuwa kuna uhuru wa kuabudu hivyo, lakini serikali ichunguze kidogo juu ya hayo madhehebu kwa sababu kume kuwa kuna vitisho. Mtu akitoka mashamba pia waambiwa vitisho, waambiwa ukienda mjini basi ujijue kwa sababu kuna madhehebu mengine yana mambo magumu, yanatumia hivi na hivi, na ukiwaangalia wanatumia Biblia bila kujua wala kujitambua usije ukajiingiza katika kundi ambalo pengine lingekudhuru ama na wewe ukawa ndiyo chanzo cha kudhuru familia yako. Maana wanamakatiba fulani ambayo ukiwa mwanakikundi pale katika ibada hizo zao, mpaka utoe mtu wako aliwe, ama mwanao, ili uwe wa kuabudu pale, na uwe saa nyingine mtu haingii kwa hiyari. Unaambiwa tu nikuabudu halafu unafika mahali fulani unashikiwa ngumu, sasa kurudi nyuma huwezi. Unasukumwa pale, mpaka unakuwa mwana kikundi basi.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo kwa uhuru wa ibada unapendekeza vipi?

**Grace Sanga:** Kuweko uhuru wa ibada lakini kuwe nasema tu kuwe na Tume kama inawezekana, kichunguze kindani kama kuna madhehebu fulani ambayo yana madhara na wanadamu, basi ikiwezekana, yaweze kukataliwa katika kusajaliwa.

**Com. Lethome:** Endelea, una dakika moja.

**Grace Sanga:** Na upande wa walioajiriwa, kutokee njia yeyote ya kwamba muajiriwa aweze kuwa na nafasi ya kupata msaada wa kiafya na jamii yake katika siku za usoni.

**Com. Lethome:** Asante Grace. Jiandikishe pale. Tumpate Grace Tsuma.

**Grace Tsuma**: Jina langu naitwa Grace Tsuma. Nitazungumza Ki-giriama. Pendeleo langu nataka, mimi ni mkulima, ninalima vitu lakini pa kupeleka, ni mpaka Kilifi, Malindi. Nina shida. Mimi nalima mali yangu Wundanyi. Mali yangu inaoza. (*in Kigiriama dialect)*

**Translator**: When it rains, there is a problem with transport so the produce is left rotting in the shamba, they can't take it to the market because of the poor roads.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini kuhusu barabara mbovu?

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator**: She wants the roads constructed, nicely tamarcked so that they can ease transport.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator**: She wants leaders who will lead them well in their country so that the country can be good.

**Com. Lethome:** Tell her to give us the quailities of a good leader?

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K. She wants good leaders with upright morals who can come and see them when they have problems and all that and good them good directions.

**Com. Lethome:** Educated or not educated?

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Educated. They should have education.

**Com. Lethome:** Can she be able to say what level of education?

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Upto university level.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. She keeps cattle but she doesn't have anywhere to take the milk.

**Com. Lethome:** So what does she suggest?

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She is suggesting that maybe they construct something like a dairy firm somewhere they can take their produce there, so that they can benefit

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. Another problem is shops, they have a problem with shopping. The commodities here are very expensive.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Another problem is that you have to go working in somebody elses shamba for you to get some money to come and buy food so that you can eat.

**Com. Lethome:** So what does she suggest.

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She would like the prices of the commodities to be lowered.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Another problem is, that they do not have the hospital facilities here like for example when somebody is expectant

and wants to deliver, they have to go all the way to Kilifi.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** So she is suggesting that hospitals be built for them around here so that they do not have that problem of travelling all the way Kilifi for treatment.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. she is saying that it is so expensive to educate children she can try to educate her children as far as the primary level but when they get to the secondary level, it becomes very hard because she doesn't get any aid or help so she is asking for that help.

**Com. Lethome:** What kind of help?

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. She is asking that free education even at the secondary level because that is where it is too expensive.

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Even the primary

**Com. Lethome:**

**Translator:** *(In Kigirima dialect)*

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She is saying that even after they are educated upto the university level, they still do not get employment. So she is asking that their children be employed here so that they can also benefit.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She is asking that their children be employed around this place because they do not even have the money to go travelling all the way upto Nairobi.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Com. Lethome:** Nyingine?

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She doesn't have anymore that is all.

**Grace Tsuma**: (*in Kigiriama dialect)*

**Com. Lethome:** Asante mama. Tumpate Sidi Charo.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: Anasema ako na homa.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K. She is saying that her major problem is the road, the transport is not very good.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K, her other problem is the fact that education has become expensive. She can afford upto the primary level, after that when they get to secondary school, she cannot afford the school fees so she is asking if there can be free education.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K, even after that, when maybe you try to struggle upto the college level, after that there is no employment, so they end up hanging around.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K, She suggests free education.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K. free education from primary level upto secondary level.

**Sidi Charo**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator**: O.K. She is still emphazing the fact about the transport, that is a major problem. She doesn't have any more.

**Com. Lethome:** Asante mama. Tumpate Patience Muya? Halafu afuatwe na Julius Kasembe. Julius Kasembe yuko? Haya utafuata huyo mama.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** My name is Patience.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Our major problem is the road.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** There is a problem with transport because of the state of the road.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** Secondly, at the hospital, when you are not feeling well, you have to have money to get any treatment.

**Com. Lethome:** So what does she suggest?

**Translator:** *(in Kigiriama dialect)*

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** So, she is suggesting that there should be free treatment at the hospitals. Even as she talks, she is sick and she doesn't have money to go to hospital.

**Com. Lethome:**
**Translator:** *(in Kigiriama dialect)Na hizo hospitali ziko mbali na hapa?*

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. There are no hospitals around, the hospitals are far away.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. She suggests that they have hospitals around.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K, she can afford fees at the primary level but when it gets to the secondary level she cannot afford the school fees because it is too high.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. She is suggesting that at the secondary level, it should be free education because she cannot afford.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. The forth point is that. She has a child who finished forth form, four years ago but since there is no employment she is just at home.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She wants them to get employed, those who finished forth form.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** O.K. She says that those who are already employed are the same people who keep on getting better and better jobs while those who are not even employed cannot get jobs at all. So the jobs which are coming up are still being given to those who are already employed.

**Comm. Lethome:** So, what has she suggested? Amependekeza nini?

**Translator:** (In Kigiriama dialect).

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** So she is suggesting that those who are already employed be satisfied with whatever they have so that the other jobs which are coming up can be given to those who are not employed.

**Com. Lethome:** One person one job?

**Translator:** O.K.

**Patience Muya**: *(in Kigiriama dialect)*

**Translator:** She doesn't have any more, that is all.

**Com. Lethome**: Jiandikishe pale, asante. Julius Kasembe?

**Julius Kasembe**: Kwa jina ni Julius Kasembe. Maoni yangu hasa naanzia pale juu, kuanzia kwa Rais. Maoni yangu ninasema kungekuwa vizuri kama kungekuwa na mfumo wa majimbo. Yaani kila mkoa uwe na Rais wake, mwisho wake tupate Waziri Mkuu.

Upande mwingine wa maoni, kutoka kwa minister mpaka kwa Rais
kuwe kuna kiwango cha elimu cha kutosha.

**Com. Lethome:** Ungependekeza kiwango gani cha elimu kwa Rais?

**Julius Kasembe**: Elimu ya Rais, kuanzia Minister iwe form six

**Com. Lethome:** Ah, Ah! Utaratibu, mmoja mmoja minster na President.

**Julius Kasembe**: Rais, form six. Rais form six.

**Com. Lethome:** Form Six na kwenda juu? Haya, na Waziri?

**Julius Kasembe**: Form six.

**Com. Lethome:** Iwe sawa tu Rais.

**James Kasembe:** Iwe tu Rais, kwa vile kutakuwa na Rais na Waziri Mkuu. Njingine.

**Com. Lethome:** Na wabunge? Elimu yao?

**James Kasembe:** Form six pia

**Com. Lethome:** Kwa hivyo wote wawe form six? Haya, Councillor?

**James Kasembe:** Councillor form four. Upande mwingine ni upande wa magereza. Kwa Mwenyezi Mungu hakuna kosa ndogo, lakini kwa mwanadamu yako makosa madogo madogo. Katika maoni yangu ingekuwa vizuri kuwa wale huwa wana nenda mahakamani na kupata makosa yale madogo madogo kama ya miezi mitatu, miezi sita, ingekuwa vizuri badala ya wapelekwe jela, warudishwe kwa ma-chiefs au kwa Dos, waje wafanye kazi na kurudishwa nyumbani ili waendelee na shughuli zao. Badala ya kukaa huko na kuteseka tu, wakifa tu bila kujulikana vifo vyao vilitokea namna gani.

Tatu. Chief awe ni mtu ameanzia form four na umri wake wa arobanne na mitano kuendelea juu. (interjection). Kuchaguliwa kwake huyu Bwana, vile vilivyo viwe hivyo. Vile huwa wanachaguliwa. Si wanafanya interviews? Wabaki vivyo hivyo pamoja na assistant chief wake.

**Com.Lenaola:** Miaka arobaini mpaka miaka mingapi?

**James Kasembe:** Themanini. Nne, kuna hawa elders hawa. Elders huwa wanapata mateso makubwa sana kushinda chief or assistant chiefs. Kama mzee wa Kijiji, anafuatwa usiku wa saa nane, na anabishiwa na akifunguwa mlango hivyo anakuta pengine anaenda kuonyeshwa maiti na hana kithibitisho chochote cha kuenda kuona ili apatie ule msaada kama mtu kumukamata. Lakini utakuta anatembea hapa, zaidi ya Dida, au huko sehemu za Zanduni, bila kumpata chief kwa sababu

utawala uko mpana. Sasa napendekeza maoni yangu hawa wazee wa vijiji wangekuwa na power kushinda hao assistant chiefs.

Lingine ni kwamba, kuna huduma za kina mama hawa. Wanapata mateso sana. Mateso ni kwamba wataoana wako wadogo, waendelee mpaka wazae, kufikisha mimba nane, tisa hivi, wanakosana na bwana. Bibi anatoroshwa kule nyumbani anaenda kwao kutafuta mahari amurudishie bwana, na bibi anabaki tu pale anateseka. Ingekuwa vizuri kungetungwa sheria nzuri hata kama ni kugawanywa watoto wagawanyiwe watoto wakina mama.

Kama ni mahari, pengine kwa bahati mbaya mama pengine hakupata kizazi, iwe kuna kiwango fulani ambacho huwa bibi naye anaweza kutoa kiasi na bwana naye akabaki na kiasi fulani. Lakini kama wameza (interjection)

**Com. Lethome:** Yaani wagawane mali yao?
**James Kasembe:** Eh, kwa mfano mimi nimeolewa na bwana, nimekosana na yeye lakini sikupata mtoto, sasa ninaambiwa nirudi kwetu. Ingekuwa vizuri mimi bibi nitafute kama ni elfu tatu kwa sababu nimeolewa kwa elfu sita, elfu tatu nimpe yule bwana.

**Com. Lethome:** Yaani urundishe mahari nusu?

**James Kasembe:** Eh, nusu.

**Com. Lethome:** Kwa mfano wamechuma mali pamoja. Kijana umeowa na wamechuma mali. Baada ya miaka minane, mnakosana, na bibi anenda. Aende mikono mitupu ama ile mali pia ana haki sawa?

**James Kasembe:** Sawa, apate.

**Com. Lethome:** Haya, na kwa mfano umeoa mke mumekaa naye halafu umekufa na kuna mali pale. Hebu tuambie haki ya huyu mwanamke katika ile mali unapendekeza nini?

**James Kasembe:** Ningependekeza ingechukuliwa na bibi mwenyewe kwa sababu bibi na bwana ndio wametafuta hiyo mali.

**Com. Lethome:** Na kuhusu ufa?

**James Kasembe:** Urithi wa ndugu?.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini kuhusu ufa?

**James Kasembe:** Hii habari ya ufa huu, mimi hata sioni kuna maana yeyote kulingana na hili janga ambalo limeingia kwa wakati huu. Ni yule ambaye atakuwa amebaki na yule bibi, kama ni kumujengea pahali bibi ya ndigu yake, atafute maoni, ile ya kumsaidia tu vitu vidogo vidogo. Hakuna habari ya kumuingilia nyumbani ati huyu ni ndungu ya bibi yangu, ah ah!.

**Com. Lethome:** Na mali inayowachwa na ndugu yao, itakuwaje?

**James Kasembe:** Nafikiri nimetangulia ya kwamba ingekuwa ni vizuri bibi ndiye angetawala hiyo mali.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo unapendekeza mambo yu ufa yapigwe marufuku?

**James Kasembe:** Yapigwe marufuku.

**Com. Lethome:** Maoni yake,ni maoni yake. Lingine.

**James Kasembe:** Kuhusu mawasiliano hasa watu wa sehemu za mashambani kama sisi, kuanzia barabara. Barabara zetu huwa ni mbovu sana. Tuko na mali zetu huku, kama machungwa, maembe, nini, vitu namna hivyo. Lakini tunakosa kuelewa, sijui watu wa mashambani wamelaaniwa nama gani, wanakosa mawasiliano hata kupeleka mhogo hapa Kilifi unaona ni karibu, ni tikiti ya karibu mia mbili, kwenda hapo na kurudi. Yote inafanywa na hii barabara, lakini kama hizi barabara zingerudishwa na kutengenezwe kikamilifu, ingekuwa jambo mzuri sana

Lingine ni kuhusu hospitals. Hospitals sehemu za mashambani huwa zinawekwa mbali mbali. Huduma hizi ziko taabuni sana. Wananchi huwa tunalalamika sana. Nafikiri nitakomea hapo.

**Com. Lethome:** Asante Bwana Kasembe. Jiandikishe pale. Tumpate Omar Wanje.

**Omar Wanje:** Mimi kwa jina naitwa Omar Wanje. Kulingana na maoni yangu, mimi ningependelea kwanza hii Kenya igawanywe. Igawanywe, kila mkoa uwe na mambo yake. Yaani iwe na mambo yake kulingana na watu wake ambao wanahusiana na ule mkoa.

**Com. Lethome:** Igawanye kulingana na nini?

**Omar Wanje:** **I**le Mikoa. Na mkuu wa mkoa awe ni chief minister ambaye atasimamia mkoa huo, ambaye amechaguliwa na wananchi. Na huyo chief minister ambaye atakuwa amechaguliwa na mwananchi awe na mwanachini wake. Wakati wowote akiwa yule chief minister amekwenda kinyume kulingana na kazi yake, chief yule mwanachini wake ashikilie nafasi ile. Chief

minister anashikilia kwa muda fulani kama miaka mitano hivi halafu anaondoka, anawekwa mtu mwingine. Sio mtu abaki na uongozi mpaka kufa kwake, hiyo tunataka Katiba ibandilishe. Maoni yangu ni kuwa iwe ataondolewa baada ya miaka mitano. Akimaliza miaka mitano basi kazi yake imekwisha, awekwe mwingine. Na kunapotokea makosa- yeyote, kama yule mtanguliwa, yule aondolewa hata kama miaka mitano haijaisha, lakini yule chief minister anaonekana na kosa, basi yule deputy wake ashikilie nafasi ile kulingana na ule muda ambao utakuwa umebakia amalize, halafu kuchaguliwe, campaign iendelee kuchagua mwingine.

Na kusema hivyo si kwamba ati ndio tumegawanya Kenya iwe ndiyo kwamba kila moja ana mambo yake. Hii ni, kama nilivyo tangulia kusema, kuwe na Rais wa muungano. Yaani, majimbo kama nilivyotangulia kusema, kisha iwe kuna Rais wa muungano. Yaani headquarter kuwe kuna rais ambaye huyu ni wa Kenya nzima, ambaye huyo naye atachaguliwa na wananchi kama kawaida inavyoendelea kuchaguliwa. Na huyo awe anachukuwa nafasi ile kwa muda wa miaka kumi. Ikiisha miaka kumi, basi pachaguliwe mwingine na ikiwa tutakubaliana namna hivyo, basi kila mkoa iwe baada ya miaka kumi unatoa mtu wao anagombea kiti cha urais. Na izunguke hivyo hivyo mpaka mikoa yote ihakikishe kila mmoja ametabaruhu hichi kiti cha urais.

Sisi katika dhehebu la Waislamu, tunaomba, katika maoni yangu nataka kuwe na Kadhi Mkuu. Kadhi Mkuu ambaye atakuwa akisimamia kesi za Waisilamu, si yo kesi ya Muisilamu kwenda kuhukumiwa na Joseph ambaye hajui taratibu za Waislamu. Kwa hivyo kuwe na chief Kadhi ambaye huyu atakuwa akisimamia mambo ya Waisilamu,.

**Com. Lethome:** Achaguliwe na nani?

**Omar Wanje:** Huyo chifu anachaguliwa na huyu minister ambaye atakuwa anasimamia mkoa, ndiye anachaguwa huyu Kadhi Mkuu ambaye ndiye atasimamia mambo ya Waisilamu.

**Com. Lethome:** Ungependekeza kila mkoa na chifu Kadhi wake? Sasa, unasema kila mkoa una chifu Minister na chifu Minister ni kiongozi wa……

**Omar Wanje:** Wa jimbo.

**Com. Lethome:** Sasa itakuwa kila jimbo lina chifu Kadhi wake?

**Omar Wanje:** Yaani inawezekana kwa sababu tunasema hivi; Ikiwa katika ule mkoa kuna Waislamu kama hamsini elfu hivi, hapo ni lazima kuwe kuna chief Kadhi wake. Kwa hivyo katika mikoa mingine kama inaenda namna hiyo, lazima iwe namna hiyo.

**Com. Lethome:** Kuna chifu Kadhi na kuna Kadhi……

**Omar Wanje:** Na Kadhi, ndiyo, Kadhi Mkuu. Chief Kadhi ni chini wa Kadhi Mkuu. Eh.

**Com. Lethome:** sasa katika kila mkoa kuwe na Kadhi Mkuu? Au na Kadhi?

**Omar Wanje:** Yaani kila Mkoa uwe na Kadhi Mkuu.

**Com. Lethome:** Na kiwango chake cha elimu?

**Omar Wanje:** Kiwango chake cha elimu, awe na elimu ya form six ya Kizungu, awe amefaulu katika kusoma katika elimu ya dini, ana shahada ya kutosha, huyu achaguliwe. Mambo ya ardhi, nikienda kwa mambo ya ardhi, ni kwamba unataka mambo hii ya mashamba, wakati mwingi huwa yanasumbuwa lakini, kulingana na vile tulivyoona tukasikia hii maneno inawatatiza kwa sababu mara nyingi kesi ya mashamba inapelekwa Mombasa ambapo huko judge ambaye hajui Kilifi ama hajui Bamba kwamba kuna nini halafu ndiye anaamua ile kesi. Kwa hivyo tukaona, maoni yangu, mambo ya mashamba yaachiwe uamuzi wa wazee wenyewe wa miji, sio kuingiliwa na judge ambaye hajui sehemu inayotetewa ni sehemu gani. Kwa hivyo hili liachiwe wazee wa miji wenyewe waweze kuamua. Nafikiri nilikuwa sina mengi sana ya kuzungumza ni hayo, nilikuwa nimepanga nielezee na kwa hivyo, asanteni kwa hayo machache.

**Com. Lethome:** Mr. Steven Baya. Yuko? Steven Baya. Robert N. Gumbao. Robert yuko?

**Steven Baya:** Naitwa Steven Baya. Oni langu la kwanza ni kuhusu Rais. Kama atachaguliwa baada ya miaka mitano na kuendelea kama alikuwa anaendelea vizuri, itakuwa si shida.

**Com. Lethome:** Kwa vipindi vingapi?

**Steven Baya:** Vipindi kama viwili. Upande mwingine nasima kuhusu hii barabara yetu. Utakuta fare iko ghali kushinda barabara nyingine zile.

**Com. Lethome:** Pendekezo?

**Steven Baya:** Kama ingetengenezwa vizuri, hiyo transport fee ingerudi chini kidogo. Kitu kingine nataka kuongea ni kuhusu malipo. Tusema mzazi alikuwa anafanya kazi na serikali, halafu unakuta labda amefariki na hajamaliza miaka amefariki ghafla, yale malipo hayaji, mpaka sasa matatizo hutokea.

**Com. Lethome:** Una kusudia kusema marupurupu ama pension?

**Steven Baya:** Nilikuwa nasema hivi, tusema yuko kazini halafu afariki kwa ghafla labda. Kwa hivyo zile pesa zake.

**Com. Lethome:** Zinachelewa kulipwa?

**Steven Baya:** Zinachelewa, hazitoki haraka vile. Kuwe kuna njia ambayo kitu kama hicho cha ghafla, ziwe zinafuatiwa zitoke.

Kuhusu tuseme jela, nataka kuongea kuhusu jela. Tuseme mtu akifungwa huwa hafanyi kazi zake huwa anapelekwa mahali. Naona ni vizuri kama atakuwa kama pale mahali asiteswe sana vile, maanake sasa tuko hapa na pale aliko. Anateswa.

**Com. Lethome:** Pendekezo? Mtu alipatikana na hatia iwe aje?

**Steven Baya:** O.K. Akifungwa, asiteswe sana vile. Na kuhusu hizi hospitali, unakuta kweli kuingia hospitali lazima uwe na pesa. Kama hayo malipo ya hospitali yangekuwa hakuna, ingesaidia zaidi lakini.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo matibabu yawe ya bure

**Steven Baya:** Tena ziwe karibu karibu hizi hospitali. Kuhusu viongozi, tuseme hawa machief na kama hawa ma-councillors wangekuwa wanachaguliwa kutoka form four na kuendelea juu, ingekuwa vizuri.

**Com. Lethome:** Chief na nani?

**Steven Baya:** Ma-councillors. O.K. Upande wa ma-MP huwa ni sawa tu. O.K. MPs wawe ni form four na kuendelea.

**Com. Lethome:** Na rais naye?

**Steven Baya:** Tuseme form four, form six na kuendelea juu, mradi tu awe amesoma.

**Com. Lethome:** Awe amesoma hata kama ni kidogo tu?

**Steven Baya:** Ah Ah! Form four na kuendelea juu.

**Com. Lethome:** Umemaliza? Asante, jiandikishe pale . Robert Gumbao

**Robert Gumbao:** Mimi kwa jina naitwa Robert Gumbao Nuyaa kutoka Maera. Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu

ma-councillor wetu. Mimi ningependekeza councillor akichaguliwa, awe ana kiwango cha elimu kuanzia darasa la saba na kuendelea.

**Com. Lethome:** Mwisho wa elimu ya msingi ni darasa la nane. Unakusudia primary ama darasa la saba tu?

**Robert Gumbao:** Primary level.

**Com. Lethome:** O.K. Siku hizi inaishia darasa la nane.

**Robert Gumbao:** O.K. Kuanzia darasa la nane na kuendelea, kwa sababu unaweza kuta kuna kijana amemaliza darasa la nane, lakini ana ujuzi au ana hali ya kuwa anaweza kuwa kiongozi kushinda mwingine ambaye amemaliza darasa la kumi na mbili.

Oni langu la pili, ningependekeza kwamba, katika kila ofisi ya chief, tuwe tunaweza kupata ma-askari wawili wa utawala, pamoja na karani wake. Kwa sababu siku hizi unakuta katika ofisi ya chief, ukitaka msaada wa askari, hakuna mpaka utembee pengine mpaka kwa divisional level ambao ni kwa DO, ndio uweze kupata maaskari. Lakini chief akiwa na ma-askari na karani wake, itakuwa ni rahisi, hata ukienda ukimkosa chief, karani wake anaweza kukuhudumia, halafu wewe ukaondoka.

Oni langu la tatu, ningependekeza kwamba katika kila location, serikali iwe inaweza kutupatia shule moja ya upili, huduma, hospitali yaani, health centre na tuwe tunaweza tukapata chuo kimoja cha ufundi.

Oni langu la nne, kuna hizi shahada au karatasi za kuzaliwa na za vifo. Unakuta siku hizi mtoto hawezi pengine kuandikishwa au kuingia nursery bila karatasi kama hiyo. Karatasi hizi mara nyingi tunazipata katika sehemu za wilaya. Pendekezo langu ningeomba karatasi hizi tuwe tunaweza tukazipata katika maofisi ya machifu wetu. Kwa sababu yule mwananchi ambaye hawezi kutembea kwenda kwa DC kutafuta karatasi hizi, awe anaweza kutembea akafika kwa chifu, na akaandikiwa na akawa anaweza kupata karatasi kama hizi.

Oni langu la tano, ningependekeza hivi. Kwa mfano kwa wakati huu huku kwetu, nafikiri tulikuwa tuna Ganze, lakini sasa tumepata Bamba division na tumepata Vetengeni division. Ningependekeza katika kila tarafa, iwe inaweza kuwa na Mbunge wake kwa vile zimegawanywa. Na pia tuwe tunaweza tukapata kituo cha polisi kwa kila tarafa.

Pendekezo langu la sita, ningependekeza kwamba ma-chifu, ma-sub-chief na ma-councillors, wawe wanaweza kupata huduma za magari, au pikipiki au baiskeli, kuwawezesha kufanya kazi zao kwa urahisi.

Pendekezo langu la saba, ningependekeza kwamba, kila mwananchi, hata kama ana robo mkambaa, au ya sehemu ya ardhi,

awe anaweza akapata title deed.

Pendekezo langu la nane, ningependekeza serikali ya majimbo. Ningeomba kila mkoa uwe unaweza kujisimamia wenyewe, na ikiwezekana wafanyikazi, asili mia thamanini na tano, wawe wanaweza kuandikwa kutoka mkoa ule ule ambao wanatoka, na asilimia kumi na tano, wawe wanaweza kuandikwa kutoka kwa mikoa ile mingine. Ili kuwawezesha wakaaji wenyewe katika mkoa huo, wawe wanaweza kupata nafasi za kazi kama wengine.

Na pendekezo langu la tisa na la mwisho, ningependekeza barabara zetu au katika kila tarafa, angalau kuwe kuna barabara moja ambao ni ile barabara kubwa ya tarafa, serikali iwe inaweza kuiangalia, na hata kutuwekea lami kama sehemu zingine. Hayo ndio mapendekezo yangu, asanteni.

**Com. Lethome:** Asante, jiandikishe pale. Tumpate Tuva Nyala Kahindi.

**Tuva Ngala Kahindi:** Mimi naitwa Tuva Ngala Kahindi. Kwanza, mashaka yangu ni kuhusu Rais. Rais ningependelea vile akichaguliwa na wenyeji, lakini kuwe kuna mkataba wa miaka mitano halafu ajaribu kuachia mwenzake.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo awe na kipindi kimoja tu cha miaka mitano?

**Tuva Ngala Kahindi:** Eh, sasa hiyo iwe ni kipindi kimoja tu cha miaka mitano peke yake. Mwenzake naye ajaribu kuona utamu au ubaya, pale pale. Kama ni utamu, uonekana na mtu mwingine. Pili, kuhusu ma-chifu wetu na manaibu wao ningependelea wawe nao wao ni watu wa kufanya kuchaguliwa kama ma-councillor. Si kuchukuliwa tu huko kwa ofisi kubwa kumbe huku kuna vitendo ambavyo havistahili na wananchi. Kwa hivyo ningeomba kwamba nao wachaguliwe kama ma-councillor.

Haya, ya tatu ni kuhusu huduma za mahospitali. Huduma za ma-hospitali, watu wanaumia sana kwa huduma za mahospitali, kwamba ni lazima uwe na pesa. Ikiwa mimi ni mgonjwa na sina pesa, itakuwaje? Hospitali nataka ziwe za bure. Kuhusu elimu.

**Com. Lethome:** Hospitali zenyewe zipo?

**Tuva Ngala Kahindi:** Hospitali zenyewe ziko mbali mbali sana, huku kwetu ni kwamba hakuna. Napendekeza ziwe hospitali za karibu karibu na ziwe zina huduma bora. Kuhusu mambo ya barabara pia. Tunapata shida sana; kukinyesha mvua, hata hivi mmekuja na raha lakini kama ni wakati wa mvua, nafikiri: mngebaki huko Dida. Kwa hiyo huduma hivyo ionekane kwa kufanywa vizuri. Si mchanga tu peke yake, Mchanga peke yake ule utaenda na maji. Barabara iangaliwe vizuri. Kuhusu skuli. Watoto wetu ni kama ukizaa watoto wainne, watano, una maka sababu ya huduma za shule karo ya shule. Ningependekeza kwamba kuanzia mwanzo mpaka secondary, iwe bure. Ni pendekezo hilo.

Haya, kuhusu ma-councillor wetu. Pendekezo langu. Sisi tunapendekeza yule ambaye anafanya vizuri katika mtaa wake yule ambaye anapendekeza uzuri mahali aliko. Ikiwa ana elimu lakini, asiwe ana elimu, sababu wale waelimu, hata ukiwa una elimu, hutafanya lile ambalo ni nzuri kwa wananchi hufai kitu. Pendekezo langu ni kwamba, yeye ana elimu, hana elimu, lakini huduma ziwe nzuri. Natosheka mimi, pendekezo langu. Haya, kuna hawa wakina mama, wakina mama walichukua nafasi kubwa sana kwa sisi wazee. Nafasi kubwa ni kwamba, mtoto wako wewe atamaliza shule na amefika wakati wa kuolewa lakini basi unamuona tu, hataki kuolewa na wewe kwa vile sasa unaona si haki azalie pale, unataka aolewe. Na ukisikizana na mtu kwamba huyu aolewe, basi, wewe utaenda kifungoni wewe! Utaenda kufungwa. Sasa, wewe unanifunga, mamako ulimchukua kwa babu yako huyu? Wewe unanifunga kivipi? Anasema mpaka nitake mwenyewe bwana. Sasa utake mwenyewe bwana, na wewe unazaa. Kwa nini yule ambaye amekuzalisha, huwezi kuja naye hapa ukaja kunionyesha huyu ndiye bwana wako. Kwa hivyo, hiyo, nimepata siri kwamba, ni vile akikupeleka kwa chifu, unaenda kufungwa. Ndiyo sasa mamlaka hayo, nataka yaondolewa.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo unapendekeza nini? Mzee aweze kumulazimisha binti yake aolewe?

**Tuva Ngala Kahindi:** Si yo kulazimisha lakini yule anamudunga mimba yule, ningetaka aje naye pale kwangu aniambie, huyu ndiye mkwe wako huyu. Unaona?

**Com. Lethome:** Na akikataa kumuoa? Yule aliyemndunga mimba akikataa kumuoa?

**Tuva Ngala Kahindi:** Basi huyo tutapelekana mbele.

**Com. Lethome:** Unapendekeza achukuliwe hatua gani?

**Tuva Ngala Kahindi:** Huyo napendekeza kwamba, hata kama ni shilingi moja moja, lakini mahari yangu vile nitakavyo sema, anipatie shilingi moja moja mpaka ifike.

**Com. Lethome:** Hatafika mahari akubali kumuoa. Amekataa ameruka. Achukuliwe hatua gani?

**Tuva Ngala Kahindi:** Ikiwa hatanipatia mali, haya nataka afungwe, na asimurudie tena mtoto wake.

**Com. Lethome:** Kuna kitu nimekosa kukuelewa. Umesema wewe umemfuatia binti yako mtu,wewe unasema aolewe kwake na yeye hataki. Ungependekeza nini?

**Tuva Ngala Kahindi:** Hiyo kama hataki, aoelwe kule ninakosema mimi. Yule mwenye kumudunga mimba aje naye pale.

**Com. Lethome:** Hajamundunga mimba, hana mimba.

**Tuva Ngala Kahindi:** Hana mimba?.

**Com. Lethome:** Hana mimba, umekwenda ukamtafutia mtu kwa sababu unaogopa atazalia nyumbani. Ulivyosema wewe mwenyewe unaogopa atazalia nyumbani, unamtafutia mtu. Ungependa binti yako ukimtafutia mtu akubali?

**Tuva Ngala Kahindi:** Ningetaka hivyo.

**Com. Lethome:** Ampende, asimpende bora wewe umempenda huyo mtu, binti yako pia akubali?

**Tuva Ngala Kahindi:** Sababu mimi ni mzazi.

**Com. Lethome:** Na mamake ama haki ya kusema, " La, sitaki binti yangu aende kule?" Ana mamlaka?

**Tuva Ngala Kahindi:** Atakuwa anashindana na mimi, sitaki.

**Com. Lethome:** Anashindana na wewe? Endelea.

**Tuva Ngala Kahindi:** Kwa hivyo mimi naona nimekomea hapo.

**Com. Lethome:** Kidogo tu. Kuhusu mila ya ufa, unapendekeza nini?

**Tuva Ngala Kahindi:** Kuhusu mila ya ufa, hiyo napendelea ingeondolewa. Hiyo ingeondolewa isipokuwa sasa, yule mwenye kuchukuliwa ufa yule, akiwa yule mwenye kufa ameacha watoto na mama yao, mali ibaki na watoto na mama. Kuhusu ardhi zetu. Sisi ni kama tumeletewa msemo. Msemo ni kwamba bado hatujapata mashamba. Mashamba ni title deed. Bado hatujazipata na tunaona ni kama ni msemo, zachelewa. Pendekezo ni kwamba, wale wenye kutupatia zile title deed, wafanye haraka tuone kwamba tumemiliki vizuri kama wengine.

**Com. Lethome:** Asante, jiandikishe pale. Tupate Gasper Mwamuye.

**Gasper Mwamuye**: Gasper Mwamuye. Kuhusu ngazi ya juu, Rais, napendekeza awe na kiwango cha miaka mitano. Aishi katika urais wake kwa muda wa miako mitano, ukimalizika mwingine na yeye apate. Hivyo, hata councillors, hata wale wa umma wale PC ama manaibu wa ma-chief, wote hawa. Watu wote wa umma, wawe wanafanya kazi kwa miaka mitano.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo wote wachaguliwe kwa kipindi cha….

**Gasper Mwamuye**: Miaka mitano.

**Com. Lethome:** Pia ma-PC, na ma-DO na ma-PC wachaguliwe kwa kipindi cha miaka mitano?

**Gasper Mwamuye**: Vivyo. Sasa wachaguliwe. Eh, miaka mitano. Kwa upande wa elimu, mimi mwenyewe nimefanya kazi ya kuelimisha watoto wangu, mpaka sasa nishaelimisha. Mtoto wa kwanza amepata C+, mwanamke. Mtoto wa pili akapata C, mtoto wa tatu akapata D+, mtoto wa nne akapata D+, na mwingine yuko darasani bado, pale, hawajapata kazi. Na shaka langu, kazi za hapa, zinafanywa na watu ambao hata hawakusoma.

**Com. Lethome:** Pendekezo?

**Gasper Mwamuye**: Ningependekeza kwamba hawa watoto wapate kazi. Na lingine kuhusu mambo ya elimu, kuhusu mambo ya karo kutoka primary kwenda juu. Ningependekeza kwamba zile karo, ama mtoto kama ameshinda kwenda mbele zaidi, basi awe na mchango wa kuchangiwa aende shule. (interjection). Shule ya msingi mpaka kule secondary. Karo ya shule ikimshinda yule mtoto, Basi watu wa ile tarafa wachukuwe jukumu yule mtoto aende. (interjection). Mtoto asikose kwenda shule kwa sababu mimi ni masikini.

**Com. Lethome:** Huyu ni mtoto wa ufahamu wa hali ya juu…..

**Gasper Mwamuye**: Hali ya juu.

**Com. Lethome:** Na mtoto ambaye ni wa kawaida?

**Gasper Mwamuye**: Mtoto wa hali ya kawaida, ichukuliwe jukumu kuwa atapelekwa village polytechnic, na kulingana na kiasi chake vile ilivyo.

**Com. Lethome:** Tunaelewana? Nasema mtoot ambaye amepita vizuri na hawezi kulipa karo afanyiwe mchango kwa tarafa. Na huyu wa ufahamu wa hali ya kawaida?

**Gasper Mwamuye**: Yule atafutiwe college yeyote.

**Com. Lethome:** nasema huyu ambaye amepita kwenda secondary.

**Gasper Mwamuye**: Amepita kwenda secondary?

**Com. Lethome:** Ndiyo lakini si ati ana ufahamu wa kawaida.

**Gasper Mwamuye**: Huyu basi atafutiwe college yeyote ile kulingana na ile hali yake. Ili apate kazi. Basi maoni yangu ni hayo machache.

**Com. Lethome:** Asante \gasper, jiandikishe pale. Tumpate Moses Sofa

**Moses Sofa:** Kwa jina naitwa Moses Sofa. Ningependekeza kwamba wanfanyaji biashara ndogo ndogo, wapate mikopo. Kwa sababu tunaweza kufanya biashara lakini sasa utakuta pesa zikiingia kwa serikali, ukienda kule mpaka uambiwe kwamba uwe na guarantors, uwe na mdhamini, yule ambaye atakwambia "nakujua kwamba wewe unakaa sehemu hii".

**Com. Lethome:** Kwa hivyo ungependa mtu apewe loan bila guarantors?

**Moses Sofa:** Hata chifu pia anaweza kukudhamini, pia yeye ni kama anayekujua kule unapokaa. Kwa hivyo ningependekeza aruhusiwe bila kuambiwa mpaka uwe na title deed. Sasa mimi maskini tena naambiwa ni lazima niwe na title deed itakuaje iwe nitapata mkopo? Kwa hivyo ningependekeza nipewehuo mkopo bila kusumbuliwa.

Jambo jingine, kuna wakati mwingine mtu anaweza kukufanyia matatizo, kukisiwa kwamba umeiba ama muwe kama wawili. Sasa kabla hujapelekwa kortini, unapigwa kabla hujajulikana kwamba ni wewe uliyeiba. Unapigwa hata baadaye kuwa pengine kumechunguzwa kwamba si yo wewe, huwa umeumia tayari. Kwa hivyo ningependekeza kuwe na uchunguzi wa kutosha ndipo mtu aadhibiwe. Lakini munampiga mpaka hata pengine akifika kule, maisha yake mumeshamumalizia kabisa. Kwa hivyo ninapendekeza ichukuliwe hatua ya kuchunguzwa.

Jambo lingine, kule katika location kuna sub-location na kuna wazee wa vijiji. Ninapendekeza, watakapokuwa wamechaguliwa wawe ni wale waliosoma. Waliotoka class cha nane kuendelea mbele. (interjection) Ah, Ah! Wazee wa vijiji. Maanake hata wengine hawajui kusoma, tena ni wazee wa vijiji, sasa hiyo, na kuna vijana ambao wanaweza kuifanya kazi ile.

**Com. Lethome:** Sasa unataka iwe vijana wa vijiji na sio wazee wa vijiji?

**Moses Sofa:** Ah Ah! Hata kama ni…Yaani kuna wale wamefifuka. (interjection). Umri Kutokea arobanne na tano kuendelea mbele hata hamsini maanake kuna wengine hata kama mimi na kama mtu miaka thelathini kuendelea mbele na nimesoma mpaka class cha nane. Kwa hivyo ninafaa.

**Com. Lenaola:** Kuanzia umri gani?

**Moses Sofa:** Thelathini, arobanne kwenda juu.

**Com. Lenaola:** Sema 30 kuenda juu au 40 kwenda juu.

**Moses Sofa:** Tuseme thelathini juu. (interjection). Eh, hamsini.

**Com. Lethome:** Wazee wa miaka sabini tusiwaweke pale?

**Moses Sofa:** Pengine, tuseme waliosoma hapo juu. Na jambo jingine, katika Kenya hii tuliyo nayo, tuna mikoa minane. Sasa tunataka kila mmoja ambaye yuko kwao awe anafanya kazi kule - - ile sehemu ya kule kwao. Kwa mfano, kuna wengine wametoka Kilindini, na wanaoto kawanatoka lakini wenye kuingia hatuwajui kama wameingia. Tunakuta wazee wame-retire, lakini hatujasikia ya kwamba kijana ameandikwa. Akitoka, ametoka lakini kuingia, haingii. Sijui ni kwa nini.

**Com. Lethome:** Sasa hapo umesema kila mmoja afanye kazi kwao

**Moses Sofa:** Eeh.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo kama ni mwalimu, walimu wawe wa hapa hapa?

**Moses Sofa:** Eeh, tumesoma hata sisi. (interjection)

**Com. Lethome:** Madaktari wawe wa hapa hapa, mapolisi wawe wa hapa hapa. Kwa hivyo kama mtu wa hapa wanashikilia kazi fulani, akiondoka aje mtu wa pale pale…?

**Moses Sofa:** Pale pale. (interjection).

**Com. Lethome:** Huo ni urithi! Tuseme kwa mfano, mkuu wa Kilindini Port, akiwa ni mtu wa hapa vitengeni, akiondokaa pengine kijana wa vitengeni?

**Moses Sofa:** Hata kama si Vitengeni kama Malindi, hapa hapa. (interjection). Eeh, Mkoa huu. Ni hayo tu basi.

**Com. Lethome:** Asante jiandikishe. Tupate Fondo Kazungu.

**Fondo Kazungu:** Kwa majina naitwa Fondo Kazungu. Pendekezo la kwanza ni kwamba, ninaanza na hawa wazee wa kijiji. Kwa mfano kama kesi imeanza kwa wazee wa kijiji, au wa mitaa, ningependekeza ikitoka pale iende kwa naibu wa chief. Ikitoka kwa naibu wa chief, iende kwa chief. Kutoka hapo sasa, ndio iweze ikapelekwa mbele.

Pili, askari wawe wakitutumikia kama kawaida. Sio uje umupigie report, yeye hawezi kuondoka mpaka apewe pesa. Ma-councilors wafanye kazi yao, wasiingilie mambo ya sub-chifu wala ya chifu.

**Com. Lethome:** Unataka polisi awe mwenye kuhudumia hata bila wewe kutoa pesa?

**Fondo Kazungu:** Bila kutoa pesa.

**Com. Lethome:** Haya na ikiwa amekataa kabisa na ile ni kazi yake unataka kulalamika kwa nani?

**Fondo Kazungu:** Sasa akiwa amekataa sasa inaonekana kutakuwa hakuna usaidizi na ile ni utumishe kwa umma.

**Com. Lethome:** Na akikataa kutoa huu utumishi kwa umaa? Utalalamika kwa nani? Pendekeza, tushauriane.

**Fondo Kazungu:** Itabidi tuumie hivyo hivyo basi, na mimi ndio napendekeza tusiumie.

**Com. Lethome:** Tumekuja kuchukua maoni yenu kwa sababu hatutaki muendelee kuumia hivyo. Mutakubali tunyamaze na tuumie? Pendekeza

**Fondo Kazungu:** Mimi kitu ambacho ningependekeza, wangetuhudumia bila…(interjection)

**Com. Lethome:** Na je, wakikosa kutuhudumia? Wacha niwahakikishieni. Hii Tume ya marekebisho ya Katiba inafanya kazi chini ya sheria ambayo imepitishwa na Bunge. Katika kikao kama hiki, una uhuru wa kupendekeza jambo lolote bila kuogopa mtu yeyote. Najua wengine wameogopa, sijui kuna kachero hapa, nitashikwa. Hakuna kitu kama hicho. Sheria imekupa uhuru wa kusema utakavyo, kuna sheria ya kukulinda. Usivunje sheria lakini, sema bila uwoga. Kuna wengine waliosema jela watu wasifungiwe, watu wengine kama wamefanya makosa madogo madogo wasifungwe jela, wapewe nafasi ya kuweza kufanya kazi zao. Sasa na wewe inaonekana kuna wasiwasi ulionao. Usiogope lolote ndungu yangu. Sema wazi wazi. Ukishikwa ukitoka hapa, tambie tutachukua hatua sisi wenyewe.

**Com. Lenaola:** Ninasema hivi, nimeenda kwa polisi nikaripoti, hajachukua hatua kisheria hajakutumikia. Ungependa upeleke complain yako wapi Baada ya hapo?

**Fondo Kazungu:** Nikumurudishia sub-chief au chief. Haya, councillors. Wawe wakifanya kazi yao wasiingiliane na mambo ya chief wala sub-chief. Kwa mfano, kama kuna mhalifu amepatikana, na wewe unataka uongee na mlalamishi, ili mukikubaliana na mlalamishi, yawe mambo yatapita au yataisha. Halafu unakuta chifu anakataa au sub-chief anakataa kwa sababu anasema mkikubaliana hivyo, siku nyingine wewe mulalamishi ukienda na matatizo, hatakuhudumia.

**Com. Lethome:** Sasa unasema watu watatue malalamishi yao bila ya kuenda kwa kikao cha chifu?

**Fondo Kazungu:** Wanamaliza wenyewe kwa wenyewe ikiwezekana.

**Com. Lethome:** Wakubaliwe wamalize wenyewe kwa wenyewe?

**Fondo Kazungu:** Eh. Jambo lingine ambalo ninapendekeza, mnazi uruhusiwe kwa sababu kuna wengine wanasomesha watoto wao kupitia njia ya kuuza mnazi. Pendekezo lingine…

**Com. Lethome:** Mnazi wa mti au pombe?

**Fondo Kazungu:** Pombe. Jambo lingine, kuhusu matatizo ya watoto wa shule ya primary, shule za msingi, wasome bure. Lingine, ninapendekeza barabara itengenezwe vizuri, sio kama vile ambavyo walitengeneza wakati wa mvua itakuwa haipitiki ili tupate nauli irudi chini. Na hayo ndiyo mapendekezo yangu. Ah, sorry, nimesahau mahali pamoja. Watu wanaoajiriwa na serikali, au makampuni, wakimaliza miaka yao, wapate pesa yao ya malipo ya uzeeni bila kutatizika. Hilo ni la mwisho.

**Com. Lethome:** Asante sana, jiandikishe pale. Tupate Philip Kazungu.

**Philip K. Kazungu**: Mimi langu la kwanza nikutoa shukrani kwenyu kufika hapa kwetu. Mimi ni Philip Kazungu. Kwanza ni kutoa shukrani zetu kwa vile mkafanya kufika nyinyi hapa na kujua matatizo yanayotuhusu sisi, kama wananchi wa sehemu hii ya huku Vitengeni. Na kwanza ni kuhusu majimbo. Ningependelea serikali hii yetu ambayo kwa sasa tunayo, tujaribu tuwe na sserikali ya majimbo. Tumekaa kwa muda mrefu na serikali hii moja mpaka sasa. Na tumejua mambo yake, na tunataka tujaribu kuangalia majimbo nayo kama yatatusaidia kivipi.

Kuhusu serikali hii yetu, utakumbwa na tatizo, unaingia ofisi ya chifu au sub-chief, hicho ndicho kikao cha kwanza kabisa. Kufika na shida zako kwamba usaidiwe ama upate msaada, utakuta pengine mtu ameibiwa mbuzi. Ripoti hiyo kwanza unampelekea chief ama sub-chief, anakwambia mimi sina askari, unatoa kitu kidogo ili aende akatafute mwizi aende atafute huyo mtu. Ningependekeza kwamba, unapofika kwa sub-chief hapo huwa ni kwa serikali kamili. Anajua njia gani ya kufanya msaada kwamba wewe usaidike, bila kuitisha pesa, kwamba usaidike. Sababu huna pahali pa kwenda kupeleka shida zako, kwanza ni hapo. Utakuta yeye anasema, "Mimi sina namna kwa hivyo bila kutoa kitu kidogo, mambo yako hayatakuwa."

Sasa hakuna hatua yoyote ambayo atachukulia.

Ukiangalia sasa, huna pahali pa kwenda, ama usaidizi wako ni pale upate msaada kwa vile kile kitu ni kile ambacho kimeenda, sasa upawe ama usaidiwe, yeye anaweza kusema kwamba hana msaada, hana namna ya kufanya mpaka usaidike. Ukienda kwa chief, ambapo hapo ni juu ya huyu subchief, chief anakwambia, " Mimi sina askari.". Ukiangalia…

**Com. Lethome:** Ni kweli huwa hana askari?

**Philip K. Kazungu**: Anakwambia, "Sina askari." Sasa wewe… (interjection). Ninapendekeza pale, chief awe na maaskari ambapo sasa. kama ni msaada, upate kwa niaba ya vile report yako imeenda na imeingia kwake. Anakwambia, "Sina askari," na utashindwa utaanzia wapi, mali yako imeenda na hata, licha ya hivyo pengine mtu amekuja kwako, amekutatiza hapo bomani kwako, umeenda kwa subchief anakwambia, "Lete kitu kidogo huyu mtu afuatwe," ambapo yeye sasa ni mtu tu, anamjua. Badala ya andike barua kwamba so and so kuja kwa ofisi tutatue hayo mambo, anakwambia, "Mimi siwezi kwenda mpaka utoe kitu kidogo ili huyu mtu afuatwe". Pendekezo ni kwamba tunataka tujue, yeye ameajiriwa kama mtumishi wa umma na kazi yake ni kuangalia watu wake katika jiji lake. Ana uhaki yeye kuita mtu kwa njia yeyote. Yeye anashindwa na hiyo kazi yake kwamba hana namna. Mtu mimi nimefika kwake ananiambia hana namna, nitafanyaje? Ama nifanye kitu gani pale?

Jambo lingine, ningependekeza huyo subchief huyo, ni kuambatana na kuwa hajui kazi yake. Awe kama ni mtu anajua kazi yake, hangeniambia jambo kama hilo ambalo silijui, na ni pale nimeenda.

**Com. Lethome:** Kwa kawaida anawekwa na nani?

**Philip K. Kazungu**: Amewekwa na serikali.

**Com. Lethome:** Nyinyi mlimchagua?

**Philip K. Kazungu**: Hatuchagui sub-chief. Tunataka sasa wakati huu, ma-subchief wawe wakisimamiwa na wananchi wenyewe. Huyu anafaa, huyu hafai. Hata kama ana elimu yake, lakini wananchi wawe wamependekezwaeye kwamba wamuchague wenyewe, wajue.

**Com. Lethome:** Achaguliwe kivipi?

**Philip K. Kazungu**: Sijakupata.

**Com. Lethome:** Achaguliwe kivipi?

**Philip K. Kazungu**: Achaguliwe na wananchi wenyewe. Na wananchi wenyewe. Upande mwingine, huku kwetu michango tunayofanya ya majengo ya mashule ya kwanza ama ma-primaries, ukifika hapo unakuta jengo ni hilo hilo, ukimpata chief ama sub-chief anasema wampee pesa. Wazazi wanalalamika, wanatoa pesa lakini pesa zile haijengi shule ile ile na ni pesa tu ambazo zinaitishwa pale na hazina msimamo wote ambayo inayofanya pale,.Kwamba wazazi, kwamba waone ni wapi wangesaidia kulingana na zile pesa wametoa. Utakuta mpaka mwaka unaenda tu. Ni pesa zinaitishwa mashule, lakini hakuna kitu ambacho kinafanyika pale, mpaka wazazi wengine wamekuwa ni wavivu na kutoa pesa za ujenzi. Ukiangalia mtoto anafukuzwa shuleni kwa sababu kunasemekana mzazi hatoi pesa.

**Com. Lethome:** Haya, ungependekeza nini?

**Philip K. Kazungu**: Ningependekeza kwamba serikali ichukue hatua la jukumu kama hilo.

**Com. Lethome:** Jukumu la hizo shule kusimamiwa vizuri…

**Philip K. Kazungu**: Shule zisimamiwe vizuri, na serikali pia ijue kwamba ni pesa ngapi imeingia hapo. Ifanyie auditing kwa sababu hizi pesa nyingi ambazo zimetolewa kwa mashule, katika ma-primary, huoni shule zimefuatwa kwa auditing za vitabu kuchunguzwa na wakuu wa serikali, ambapo hata ukienda kwa huyu, ukimupata huyu yeye anakwambia "Ni huyu kitabu kina huyu", naenda tu hivi hivi mpaka zero.

Jambo jingine ni kuhusu sehemu zetu. Huko utakuta kama wale wazee ambao wanaitwa wazee wa mitaa. Kuna vitu vingi ambavyo zinaenda kinyume cha zile vijiji. Utakuta mtu mwingine ameibia mwenzake pale, ambapo ni kwamba amefika kwake na hatoi jukumu kwamba aende kwa sub-chief na chief aanze kuchukua hatua. Utaona hawa wazee wengine, pengine ni mtoto wake ama sijui ni jirani ama ni mtu anamjua. Unaenda kulalamika, na hakuna hatua ambayo yeye pia atachukua.

**Com. Lethome:** Pendekezo?

**Philip K. Kazungu**: Ninapendekeza kwamba, mtu kama huyo hafai. Hafai na hajui kazi yake wala yale ambayo anafanya. Kwa hivyo mtu kama yule atolewe nje, na chief apatiwe kibali achague yule mtu ambaye anaweza kumusaidia kwa kikazi. Si yo mtu kama huyo hafai na amemuweka hapo kwa sababu akipata shilingi mia moja kule anaenda kumupatia hamsini halafu inakuwa namna hiyo.

**Com. Lethome:** Endelea

**Philip K. Kazungu**: Kumalizia ni kwamba, upande wa mahospitali huu upande wetu una shinda nyingi sana. Utakuta mtu hapa

ana shida ambaye pengine angekuwa na hospitali hapa karibu akasaidika hapa lakini mpaka aende Kilifi. Barabara zetu nyingi ambazo hazina mwelekeo mwema ambapo ukifika hapo, kama ni mama ama ni mtu mwingine, ameshindwa na nguvu za kutibiwa anakuwa marehemu huko. Baada ya hiyo siyo transport ya kwenda hapa mpaka huko, hakupata usaidizi wa haraka kumuondoa hapo mpaka kule, ili kwamba apate msaada mapema. Ambapo kama tungefikiria kisawa, tungekuwa na hali ya huduma nzuri katika kama sehemu hizi za huku, ingekuwa ni vizuri .

Upande wa pili ni kuhusu mambo ya barabara. Barabara zetu hizi ni za wakati wa ukame lakini wakati wa mvua hazipitiki kabisa, na ukienda kwa chief ama kwa muhusika mwingine anasema mambo yetu hayo yako mbele. Yako mbele iko mbele mpaka wa leo hakuna chochote ambacho kinaendelea. Tungependa jambo hili pia serikali ijaribu kuchukua hatua. Kwa hivyo asante.

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Philip. Haya mwingine Lucina Kitao.

**Lucina Kitao:** Kwa jina naitwa Lusina Kitao kutoka hapa Vitengeni, mimi ni mwenyekiti wa Maendeleo ya wakina mama. Maoni yangu mimi ninataka Rais atawale, na hiki kifungu kiondolewe cha unafika kuwa miaka kumi uache urais. Na jambo la pili ni kuhusu haya mambo ya ma-sub-chifu, ninapendekeza ya kwamba wakina mama wakati wanapoenda kwa machiefu huwa hawatambuliwi. Na kutambuliwa ni mpaka uwe una pesa ndiyo utambuliwe. Bila hiyo, mambo yako yanaenda mrama.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo unapendekeza nini?

**Lusina Kitao**: Ninapendekeza ya kwamba, Rais aendelee kutawala, na hawa ma-sub-chifu waundiwe Tume ya kuwa ikiwa pengine kama ni mama ameenda, hajiwezi na hana chochote, awe ana mahali ambapo anaweza kuenda kuripoti, na huyu sub-chifu akachukuliwa akapelekwa pale akaenda kuhojiwa. Kwa sababu wamama sisi tunaonewa sana. Kwa hivyo sisi watu wa hapa Vitengeni tunatarajia tupate title deed ili sisi wamama tupate kujusaidia na hata wakina baba pia wapate kujisaidia kwa sababu mashamba yameandikishwa zaidi ya miaka kumi na hatuna hata title deed na utaona kwamba huwezi kupata mkopo usipokuwa na hicho kitu,. usipokuwa na title deed. Kwa hivyo napendekeza ya kwamba tupatiwe hizo title deed ili tuweze kujinufaisha na kujiinua huku mashambani.

Lengine ni kuhusu ni watoto wetu. Watoto wetu wamesoma kweli na kuna watoto ambao wamekaa mashambani zaidi ya miaka kumi kutoka wafanye mtihani na wamepata wame-pass lakini hawajapata kazi. Na kila uingiapo, hufanikiwi. Kwa hivyo tunapendekeza ya kwamba watoto ambao wamemaliza zaidi ya miaka kumi nyumbani wapatiwe makazi ili wakaweze kutuinua na sisi kwa sababu nitalima kipande mpaka mtoto nimsomeshe, nitataka apate kazi na mimi ili nipate kusaidikia. Sasa ikiwa nilifanya bidii mtoto akasoma na sina mafanikio yoyote, tunabaki sote nyumbani kulima vipande naye amesoma. Kwa hivyo serikali yetu iangalie mambo haya ili watoto wetu wapate kuajiriwa kazi ili nasi tupate kunufaika.

Lingine ni kuhusu upande wa barabara. Tunataraji barabara zetu zitengezwe kwa hali nzuri na pia hata nauli ziweze kurudi chini kwa sababu utaona ziko ghali sana kwa sababu ya barabara. Kwa hivyo tunaonelea kwamba barabara zikitengezwa zikiwa nzuri, tutaweza kujinufaisha hata mazao yetu mashambani tutaweza kuwa tunaweza kutoka na kuyauza. Ni hayo.

**Com. Lethome:** Asante bi. Luciana, jiandikishe pale. Tumpate karisa Mwambogo.

**Karisa Mwambogo**: Mimi nitaanza na jina langu ni Karisa Mwambogo. Nitaanzia na mambo ya huduma ya hospitali. Hospitali zetu wakati huu zinatutesa sana kwa sababu ya kwamba wewe unaweza kwenda kwa daktari kama Kilifi, unakwenda asubuhi. Wewe ni mgonjwa, unakaa mpaka daktari anakuja saa nane za mchana. Tena kutoka hapa mpaka huko Katangani, mimi sasa siwezi, nataka kufa, daktari simuoni, wakati nikimuona ni saa sita. Na ananiandikia ule ugonjwa wangu, kwa vile amenipima anaseme wewe utakwenda operation. Operation inataka pesa, mimi sina pesa, si nitakufa? Na mimi sitaki.

**Com. Lethome:** Pendekeza. Umeongea habari ya mambo mawili. Hosptiali kwamba uende mpaka Kilifi, halafu pia unaitishwa pesa. Pendekeza mambo haya mambo mawili.

**Karisa Mwambogo**: Nataka hospitali ziwe karibu. Jambo la pili, ninataka hospitali ziwe bure kama zamani, hata mimi ambaye sina kitu nitibiwe vile vile.

**Com. Lethome:** Umemaliza mambo yako ya hospitali na matibabu. Mambo mengine?

**Karisa Mwambogo**: Mambo mengine ni kuhusu maji ya mfereji. Maji ya mfereji, kupanda bei mwezi huu, mwezi ujao pia inapanda tena. Hivyo hivyo mpaka ndoo moja sasa ni shilingi tano. Je, mimi nikiwa sina peni ile ya shilingi tano nitakunywa maji kweli? Kwa hivyo mimi nataka maji yarudishwe, ingawa hayawezi kuwa bure kabisa, lakini ya kama ndururu kwa ndoo moja.

Kitu kingine, ni kuhusu shule. Watoto wetu wanasoma. Wanasoma watoto wa matajiri wa maskini, lakini bei ni ile ile moja ya karo. Kwa nini, mimi sina pesa mtoto wangu atasoma? Kwa sababu napendekeza hivi, kwamba shule zirudishe bei, ile karo iwe chini na mimi ambaye sina nafasi niwezeshe kusomesha mtoto wangu. Kuhusu mambo haya ya hawa wenye kututawala hawa, kama wakina Moi, basi mimi nataka yule ambaye ataendelea kwa wakati huu tuendao, atutawale kwa miaka kumi. Ikiwa tumemuona kama anaendelea vizuri, atapigiwa kura atarudi hapo. Akiwa atakuwa anaenda kombo kombo, tutamuangusha chini, apigiwe kura mwingine. Hayo ndio maoni yangu .

**Com. Lethome:** Asante sana, jiandikishe pale. Ali Yaya Gona?

**Ali Yaya Gona**: Mimi naitwa Ali Yaya Gona, wengi sana huniita Askofu Shariff kwa sababu naitwa William Njuguna vile

vile, hali ya kubadilisha kitambulisho ni taabu lakini mimi ni Muislamu muumini. Pendekezo langu la kwanza kwa Tume hii ni kwamba, watu wa Pwani ni na Jimbo la Pwani tajiri sana lakini wenyeji wa Pwani ni masikni. Kwa hivyo napendekeza majimbo ili mwenyeji aanze kuangaliwa zaidi kwanza. Aanze kuangaliwa mwanzo kuliko mkaazi, ambaye ameingia katika Jimbo. Kwa hivyo pendekezo la kwanza ni majimbo.

Pili, mashamba ya Pwani yapate haki timiliki. Haki timiliki yaani title deeds. Ijapo kuna malalamiko, ukiulizwa sana wanasema mashamba mengi yaani makesi, lakini ikichukuliwa kuwa ambaye kesi imeisha, apewe title deed, yule ambaye bado ana kesi aanze kuachwa mwanzo, kuliko kusubiri mpaka kesi ziishe. Tunavyojua, dunia haiishi maneno. Kwa hivyo yule ambaye hana kesi apewe title deed yake. Kwa hivyo iharakiswe mambo ya title deed ili watu wawezi kunufaika, wapewe mashamba.

Tatu, elimu. Elimu katika jimbo hili kweli iko haba sana. Ninaomba elimu iwe bure kutoka msingi hadi upili. Yaani shule za msingi mpaka za upili zote ziwe bure, na jimbo liwe litashughulika, kuhusika kusimamia upande wa karo zote hizo. Kwa hivyo pendekezo langu hapo zaidi ni kwamba, jimbo liwe kuna kodi la wanafanyakazi linachukuliwa ili kusimamia karo za watoto wa shule. Na elimu hii pia vile vile ifanywe lazima kwa mke na mume. Ikiwezekana ifanyiwe misako majumbani. Watu wahakikishwe kwamba wameenda shule ili nalo jimbo liinuke kielimu.

Nne, mashamba tena, lakini safari hii nasema mashamba ya Pwani yasiuzwe ili auziwe Mpwani mwenyewe. Mgeni afanye kurombeshwa au lease kwa muda mfupi, ukiisha huo, analipa tena. Mwenyewe akisema “Safari hii mimi sitakupatia lease yaani sitakukodishia”, basi atafute pahali pengine. Lakini mashamba kutoka sasa yaachwe kuuzwa. Wakaazi wasiuze mashamba mbali wafanye kukodesha. Zaidi anaweza kuuzia Mpwani mwenzake. Mtu wa nje aliyekuja hatutaki. Hata mzungu katika beach plot akodishiwe. Beach plot kama atajenga hotel iwe katika lease. Mtu anapewa kama milioni kila mwezi au kila mwaka itategemea masikizano lakini iwe si kununua. Jimbo libaki na mali zake kamili.

Tano. Kutoka upilini, kutoka msingi katika elimu mpaka upilini unakuta watu ni gharama kwenda university, yaani vyuo vikuu kwa sababu viko bara. Tikiti yenyewe inakushinda, unachangiwa mwisho wake mtoto anabakia hapo hana neno. Kwa hivyo tunaomba Pwani nayo kuwe na university yake, yaani kuwe na shule ya university, tuseme chuo kikuu.

Ni tano hiyo eh? Sita, nidhamu katika kila pahali zinapungua sana, ziko chini kwa sababu ya dini haifuatwi ya Mwenyezi Mungu arabic dialect inavyo takiwa. Kwa hivyo kutaka kusisitiza kitu cha dini kiendelee ili maadili ya binadamu yawe sawa katika kufuata mambo ya Mwenyezi Mungu katika viongozi. Kukiwa kiongozi mkubwa ni Mkristo mwananchi wake awe ni Muislamu. Kila moja aweze kusambaza dini ya Mwenyezi Mungu vile inavyotakiwa. Akibadilika akiwa Muislamu ndiye kiongozi, mwananchi ni wake anakuwa ni Mkristo, maana nikiamini vitabu vya Mwenyezi Mungu ni viwili tu. Ijapo vimekuja na ile tofauti tofauti ndiyo vikafunganywa kuwa viwili. Kuna Torati, Zaburi, Injili halafu na Koran Tukufu. Kwa hivyo hilo lichanganywe pamoja iwe ni wakristo inaendelea na hii ya Koran Waislamu. Kwa hivyo viongozi wawe wawili wawili kusaidiana hii dini pia isambae na tukielekea kwa Mwenyezi Mungu, nina hakika shida nyingi zitatuondokea. Basi, kwa hayo,

Mungu awabariki. Inshallah tuweze kufanikiwa.

**Com. Lethome:** Hayo maandishi tungependa kuyachukua. Asante, jiandikishe.Kibibi Mwanunga?

**Kabibi Mwamunga**: Kwa jina naitwa Kabibi Mwamunga. (interjection). Mapendekezo yangu ya kwanza, ninapendekeza yule waziri tutakaye mchagua hivi, aendelee kwa miaka kumi.

**Com. Lethome:** Unakusudia mbunge ama waziri?

**Kabibi Mwamunga**: Waziri yule mkubwa mwenyewe ni nani? Miaka kumi na huyo Mbunge miaka kumi. Councillor miaka mitano. Pendekezo langu lingine ni shida huko kwetu tulizonazo sisi kina mama. Tunaolewa na mabwana, tunazaa watoto wetu na yule bwana atakuwa hakuoa kitambo, ashakuwa mzee ndio aje akuoe wewe. Na wewe utazaa. Nitasomesha wale watoto wangu kuanzia nursery mpaka darasa la nane. Nikiwa sasa nataka kumuendeleza kule mbele, yeye anasema wewe basi nimekuoa umekuja. Sasa hapa kwangu niusikie mimi mwenyewe. Sasa, pendekezo langu ninapenda tuangaliwe vizuri, tena hilo jambo liangaliwe sana maanake yeye akiwa hana nguvu lakini mimi nikiwa nina nguvu ya kuweza kusomesha yule mtoto kwa sababu nilimzaa na sitaki awe maskini, ninataka niwe na mamlaka.

**Com. Lethome:** Mzee asikumpinge ukitaka kusomesha mtoto?

**Kabibi Mwamunga**: Eh.Jambo lingine ni kuhusu huku kwetu katika mahospitali. Hospitali kubwa ni Kilifi. Kutokea hapa mpaka huko, yule mzee wangu si ashakuwa mzee tayari? Ikiwa ni magonjwa, ni mimi mwenyewe niwe ninawafanyia wale watoto wangu, na kutoka hapa mpaka huko niwe nitakuwa nina pesa, sasa pesa sina na huko ni mbali.

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini? Hospitali iko mbali?

**Kabibi Mwamunga**: Iko mbali, ninapendekeza iwe hapa karibu. Jambo lingine ni kwa maendeleo ya wakina mama. Ukiwa unataka uendelee, yule bwana hataki. Anasema ukiendelea sana utakuwa hapa nyumbani kwangu wewe ndiye mtawala. Ninapendekeza nipate nafasi ya kuwa nitaendelea na maendeleo. Sina zaidi ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Asante sana, jiandikishe pale. Nyebu Kandenge?

**Nyebu Kadenge**: *(In Giriama dialect)*

**Translator**: She is called Nyebu Kadenge.

**Nyebu Kadenge**: *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Her main problem is the road.

**Nyebu Kadenge**: *(In Giriama dialect)*

**Translator**: and the hospitals.

**Nyebu Kadenge**: *(In Giriama dialect)*

**Translator**: She wants the roads constructed.

**Com. Lethome:** Anapendekeza nini kuhusu hospitali?

**Translator**: O.K. The hospitals are far away so she is suggesting that they have some hospitals built around this place and hospital fee be reduced.

**Nyebu Kadenge**: *(In Giriama dialect)*

**Translator**: That is all she has.

**Com. Lethome**: Haya asante sana, Mungu akubariki. Tumpate sasa Janet Ngala.

**Janet Ngala**: Kwa jina naitwa Janet Ngala. Mwanzo nitaongea kuhusu employment. Utakuta vijana wa kwetu wanamaliza shule, na pengine hawakupata nafasi ya kuendelea zaidi, katika pengine colleges because of money problems. Kwa hivyo ningeonelea hizi Polytechnics zijengwe, ziongezwe ili hawa vijana wasome huko kwa kuwa hizi polytechnics zikijengwa, malipo yake si kama vile ya colleges. Lingine nitaongea kuhusu title deeds. Shamba zetu nafikiri huku kote, hakuna mtu ambaye amepewa title deeds and it has become a major problem even to me. Juzi juzi nilikuwa natakikana niwe na hiyo title deed. Nilikuwa nataka ku-register company yangu, na kwetu ni huku, nikaenda Nairobi. Nilijaribu kuhangaika huku na huku mpaka nikachukuwa plot number yangu ya Kilifi. Lingine ni development of women group. Mimi naona katika huku kwetu, vikundi vya wakina mama haviendelei kama kule bara. Sijui hawa viongozi wa huku kama wanawasaidia kina mama ama wanawanyanyasa. Kwa hivyo nataka viwe vikiendelea ikiwezekana ziendelee.

Lingin**e** ni our leaders; Viongozi wa kwetu tunawachagua, lakini baadaye tukiwachagua wanaenda kukaa, wengine wanakaa Kilifi, wengine wanaenda kukaa Nairobi. Sasa hata wananchi hawajui viongozi ni wakina nani. Hawamjui councilor ni nani,

hawamjui MP wetu ni nani hata saa hii pengine akija hapa wengine hawamfahamu kwa hivyo ningetaka hawa viongozi wetu wawe wakiwasiliana vizuri na hawa wananchi.

**Com. Lethome:** Ungependekeza kama hawawezi kuwasiliana na wananchi wawachukulie hatua gani?

**Janet Ngala:** Sasa kama hawatakuwa wakitembelea wananchi na pengine kujihusisha na matakwa ya wananchi, si wanaweza kukosa hata uongozi? Kwa hivyo wajihadhari na hiyo.

**Com. Lethome:** Sasa, kama umemchagua na ameenda huko akalala, atalala miaka mingapi? Tano, ama sivyo? Je, hapa katikati ungependa wananchi wawe na uwezo wa kumuita na kumuondoa hata kama ni baada ya miaka mitatu ama tumuache tu mpaka miaka mitano halafu ndio tutamtoa?

**Janet Ngala:** Tutamuacha mpaka akimaliza hiyo miaka yake mitano, halafu tutamchagua mwingine. Tutamchagua mwingine baada ya kuwa sasa tumeona uongozi wake si nzuri. Tutakua tumeona uongozi wake si mzuri.

**Com. Lethome:** Wewe ambaye hukuridhika na hayo maoni, andika mahali ukija hapa utatuambia maoni yako, hayo ni maoni ya Janet. Haya endelea

**Janet Ngala:** La mwisho ni barabara. Barabara zetu zimetengenezwa vizuri, lakini kwingine hazikuwekwa murram. Kwa hivyo tunaomba, barabara zikiwekwa murram, huwa yaani magari yanapita kila mara, hatutakuwa na utelezi maanake barabara itakuwa ni ya all weather. Kwa hivyo tungeonelea kama ni murram inawekwa, maybe the whole road ikiwezekana. Kwa hayo, asanteni.

**Com. Lethome:** Swali moja tu, kuhusu baadhi za wakigiriama, kuna baadhi ya mila ambazo unaona pengine zipigwe marufuku na sheria ama unaona ziendelee?

**Janet Ngala:** Ziko zingine, kwa mfano haya mambo ya ufa. Mimi naona haya, kama ingewezekana, hayangeendela.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo ufa upigwe marufuku?

**Janet Ngala:** Kwa hayo, asanteni.

**Com. Lethome:** Asante, jiandikishe. Chengo Wambire? Sema mapendekezo, maana tuko na wengine wanaotaka kuongea.

**Wambire Chengo :** Kwa jina ni Chengo Wambire Ndwingi. Kwanza napendekeza majimbo. Pili madiwani, chifu, sub-chifu,

wachaguliwe na wananchi wenyewe. Tatu, diwani akichaguliwa na wananchi, tuhakikishe ana ofisi huku kwetu, tuweze kumuona hapa bila matatizo. Tuna shida kwa kumutafuta sana. Mara kwa mara yuko Kilifi, haonekani.

**Com. Lethome:** Hiyo tayari ishaingia, nyingine?

**Wambire Chengo:** Ya nne, pendekezo langu kuhusu machifu, tukifika ofisini ku-report chochote ambacho kimekupata, wanaomba pesa. Ikiwa sina, siwezi kushughulikiwa na ofisi. Pendekezo langu ni akiwa amefanya hivyo, naomba hata aondolewe kazini.

Ya tano, Rais aongoze kwa miaka mitano peke yake. Ikimalizika, awape nafasi wenzake nao waendlee.

**Com. Lethome:** Maoni yake jamani. Endelea.

**Wambire Chengo:** Ya sita ni elimu. Elimu yetu huku kwetu ina matatizo. Ninapendekeza ijapokuwa darasa la nane tunaweza tukafika lakini huko mbele tusaidiwe.

**Com. Lenaola:** Kivipi?

**Wambire Chengo:** Hiyo naweza nikasema huko mbele watuchukulie kama bure, watusaidie, serikali itusaidie. Ya saba, ni barabara. Na pendekeza barabara zetu ziwe nzuri na kusema hivyo ni kwamba, tunapata kumbukumbu kuwa zimegawanyiwa pesa na hatuzioni kwamba zimefanyika. Tunaomba Bunge liwe linaweza kutangaza moja kwa moja barabara ya sehemu fulani imegawanyiwa pesa fulani, hata mwananchi wa kawaida ajue kwamba sehemu hiyo imepata pesa ngapi na tuna haki wananchi kumu-report mbunge huyo akiwa hakufanya ile kazi ambayo pesa hizo zimewekewaa.

**Com. Lethome:** Achukuliwe hatua gani mbunge kama huyo?

**Wambire Chengo:** Hata kufutwa kabisa! Atoke, apeane nafasi mwingine afanye kazi. Ya nane, askari wetu nikifika kwa ofisi, pengine huko kwa DO, lakini naona anahusikana na ofisi ya chifu, tukijua kwamba ofisi ya chifu tunajua haina askari.

**Com. Lethome:** Pendekezo?

**Wambire Chengo:** Pendekezo langu ni ikiwa askari yuko kwa DO, uonekane mlangoni kwa DO. Ukiwa askari kwa chifu, uonekane kwa ofisi ya chifu. Sitaki mimi nilalamike na askari kwa sababu nimefika ofisi ya chief, nimepeleka report, chief ananiambia sina askari na wewe uko hapo nakuona umevaa uniform.

**Com. Lethome:** Malizia.

**Wambire Chengo:** Kumalizia kwangu, askari, chifu ahakikishe, aombe ma-askari wake. Tukipiga report tuchukuliwe bure. Kwa sababu report siku hizi ni pesa. Likiwa sina, hakuna hatua yeyote ambayo inachukuliwa. Asante, Mungu atubariki.

**Com. Lethome:** Asante, jiandikishe pale. Tumpate Roger Mwangome. Mwangome yuko? Karibu Rogers Mwangome. Karibu mzee. James Kitao yuko? James Kitao, hayuko. Kitao kama hayuko, Japeth Kisau Karisa. Haya, utamfuata mzee Rogers. Haya Mzee Rogers.

**Rogers Mwangome:** Majina yangu ni Rogers Mwangome. Nitaanza kutoa mapendekezo juu ya Constitution of Kenya. Jambo la kwanza, the Kenya Constitution has no preamble. Ilikuwa haina preamble hii Constitution of Kenya. The preamble of the Constitution of the Republic of Kenya, we need a preamble in our constitution. That is number one.

Two, our history huko nyuma has been characterized by political and constitutional instability. So, to be recognized. The sense of our Constitution is the agreement between the people, that is we here. It is the people who feel the need to live together in a society where the rule of law prevails. A good Constitution therefore must make a will of the people on the basis of a government committed to building a better future by establishing social economics, and political order through a popular and durable national Constitution, based on principles such as peace, equality, democracy, freedom, social justice and progress.

All other organs of the government are the servants of the people including the President. That is why leaders and governors are not supposed to be bosses of the people. Now, what type of government do we need? One, we need a federal government, serikali ya majimbo. That is the one we need.

Federal government; The federal government ni lazima, should have two houses. The House of Senate and the House of representatives. This House of Representatives and the House of Senate, these members must be elected by the people themselves. And then baadaye, the president, the President must be elected by the peoeple, achaguliwe na wananchi. Now, tukitoka hapo, kwamba tunataka kuwe na Prime Minister. We must have a Prime Minister. Now, huyu President, elimu yake. Elimu yake ingekuwa kama degree of Bachelor of Economics, lazima awe na degree ya Bachelor of Economics kwa sababu nchi yetu imezoroteka kwa uchumi. Kwa hivyo tukipata President ambaye anajua economics, ana degree of economics, tunatumaini ya kwamba nchi yetu itaweza kuendelea. The Prime Minister angechaguliwa na those two houses. Achaguliwe na Houses mbili, the House of representatives and the House of Senate. Ianze na house of Senate, baada ya kutoka hapo inaenda kwa house of representatives, huyo Prime Minister anachaguliwa. Not of party affiliation, tuseme kama party fulani, party fulani ah ah! Sisi tunataka the House of representatives na the house of Senate ichague the Prime Minister.

Ingine ni kwamba hawa … Kila province kuwe na majimbo majimbo haya, kila province wana Vice President. Kila jimbo liwe na Vice President au governor. Ikiwa kila jimbo litakuwa na Vice President wake, ni sawa. Dakika mbili, bado iko mingi. (interjection). O.K, O.K. lakini nilikuwa nimeandika rough notes. Hawa house of Representative na Senate, lazima wawe na elimu ya kiwango cha kutoka form four and above. Councillors, kutoka standard eight and above. President, terms zake za kuishi katika u-president ni term ya miaka 5, tunampa miaka mitano ya kwanza, halafu anachaguliwa miaka mitano ya pili ikimalizika basi. Hali kadhalika, wajumbe the same. Hatutaki mtu anachaguliwa hata miaka ishirini. Wote President na wajumbe na councillors wawe na the same terms.

Human rights, human rights; Watoto na mama yao, kama mzee ameondoka, wawe na haki ya kurithi mali ya yule aliyeondoka. Elimu; Elimu ni kwamba tungependelea kutoka standard one mpaka form four, kuwe na elimu ya bure. Free education from standard one to form four. Hali ya kugawanya pesa, kuwe na central government na hii serikali ya majimbo. Central government kwa mfano kama President awe ni mwenye kuchunga security. Yaani hali ya usalama katika Kenya na foreign affairs, ashugulikie huyu President. Na hii serikali ya majimbo, majimbo kama wanakusanya pesa zao katika jimbo, pesa zao zote zibaki kwa jimbo lakini wanaweza kutoa 75% zibaki kwa jimbo na 25% ziende kwa central government na kama kuandikwa kazi, watu wa jimbo lile wapate kuandikwa kazi. Mambo ya ardhi - unasema niende haraka - Mambo ya ardhi katika Pwani, tumekuwa na dhuluma nyingi. Kumekuwa na ma-squatter wengi katika Pwani, na kwa hivyo tungependelea kwamba yale mashamba ambayo yanamilikiwa na foreigners, na ambayo hayafanyiwi kazi, mashamba haya yainunuliwe na serikali, wagawiwe ma-squatters.

**Com. Lethome:** Haya, malizia Bwana Rogers.

**Rogers Mwangome:** Wagawiwe ma-squatters. Mahakama, judiciary, kama mtu amechukuliwa hatua kwa kosa fulani awekwe cell kwa only 24 hours, ikipita hiyo siku siku ya pili apelekwe kortini na wale wa makosa madogo madogo wafanye kazi kwao majumbani. Maduka; Maduka na mambo ya biashara, biashara tunaona ya kwamba licence, mtu anakata licence huko Kilifi, na huko Mombasa na popote pale. Halafu ile licence inakuwa sawa sawa. Kama ni shilingi elfu tatu, ni elfu tatu mpaka mashambani. Ningeona ya kwamba kuwe na tofauti kuwe na tofuati. Ikiwa yule wa town atakuwa na elfu tatu, huyu wa huku awe na elfu moja, au na elfu moja na nusu kwa sababu kule kuna mambo ya biashara. Power and communication…

**Com. Lethome:** Asante sana Bwana Mwangome lilikuwa la mwisho hilo.

**Rogers Mwangome:** Nilikuwa sijamaliza …

**Com. Lethome:** Tumpate Japeth Kisau Karisa. Haya tumpate Joseph Punda. Joseph Punda yuko karibu? Utamfuata huyu Bwana. Haya, anza kupendekeza.

**Japeth Kisau Karisa:** Haya mapendekezo yangu hasa kuhusu Rais…

**Com. Lethome:** Anza kwa jina lako tafadhali.

**Japeth Kisau Karisa**: Mimi naitwa Japeth Kisau Karisa. Mapendekezo yangu kuhusu Rais ni kwa achaguliwe kwa kipindi cha miaka kumi, tena asiwe Amri Jeshi. Upande wa jeshi uwe na yule jemedari mkuu. Upande wa ma-chief, wachaguliwe pia kwa miaka kumi. Upande wa mahari, Mzazi wakati hasa kabla ya Kenya kuwa huru, kulikuwako na utumwa, hasa Waarabu walikuwa wakitununua. Kwa hivyo hii mahari inaonekana kama utumwa moja wapo kwa vile huwezi kuoa mpaka uwe na mali. Kwa hivyo mahari iwe tu ni kwa kiwango kidogo, kwa kumufidia yule mzazi. Isiwe ni lazima ya pesa nyingi ama ng'ombe wengi kama tulivyo sisi Wamijikenda.

Barabara. Serikali ichukuwe jukumu la kutengeneza hizi barabara, badala ya kuona kama kuna labda harambee ndiyo zitengenezwe hizi barabara. Serikali ichukue hizo barabara, iwe hiyo ni kazi ambayo inahusiana na serikali peke yake.

Uraia; Raia atambuliwe kutokana na majina ya ukoo. Akiwa ni mtoto amezaliwa, ajulikane ni Mgiriama, ni Mkikuyu, hapo uraia uwe utachukuliwa kwa hali hiyo. Wafadhili; Wafadhili wasichukuliwe tu kwamba kila idara iwe inafanywa na hawa wafadhili lakini serikali ihakikishe kwamba pia nayo inachukua hatua au uwezo wa kuendeleza idara hizi badala ya kuachia wafadhili.

Kuhusu dini. Serikali ichukue hatua dhidi ya dini zingine ambazo zinakataa matibabu. Kwa mfano tuna watoto ambao wana uwezo wakielimu, wamesoma lakini wafikapo mbele masomoni? labda masomo yake yanamuruhusu kwenda kwa masomo yakidakitari dini haimuruhusu, kwa hivyo serikali ichukuwe jukumu la kuona kwa nini mtoto huyu hawezi akaendelea na masomo haya ya udaktari.

Haya, la nane, upinzani uweko kwa vile bila upinzani hatuwezi kujua serikali ina kosa gani. Ikiwa kuna upinzani, hapo tutajua kwamba jambo hili haliwezi kufanyika ama hili linastahili kufanyika. Hilo ni langu la mwisho. Asanteni.

**Com. Lethome:** Asante bwana Karisa. Jiandikishe pale na tupate Joseph Unda na afuatwe na Simon Chengo Rua. Simon Chengo yuko? Haya utafuata huyu mwenzangu. Endelea Joseph. Haraka haraka upendekeze.

**Joseph Unda:** O.K. My names are Joseph Unda, I have some few few tips, few suggestions that I would like to put across. First, in the Constitution of Kenya, we are made to understand that for somebody to be elected as a President, he or she must have attained a minimum age of 35 years old, but the Constitution doesn't state the maximum age for a presidential candidate. (interjection). So I would like the maximum age of a President to be 60 years.

Secondly, when you reach form four, there are some university forms that you have to fill. There are faculties that you select. You know you are selecting faculties but when you go out of the school, when the admission form comes, you see that the faculty which you selected is very different from what you are gramted. So I recommend that whatever you select in secondary school must be granted.

O.K. There is this issue we call remuneration. You know I want a government that fulfills its promises. For instance if it says from next year teachers will have their salaries, it do so increased. So, I want, ningetaka kama serikali itaongeza mshahara wa waalimu, ihakikishe kuwa zile phases ambazo ime-promise waalimu kuwa itaongeza mshahara, ifanye hivyo bila kudanganya danganya, si vizuri.

O.K. There is this employ sector. If you finish school unaenda college. Ukitoka college, the government ihakikishe kuwa immediately you finish your course college you are employed somewhere, you are posted somewhere, be it in a company anywhere else. Next, there are things we call public utilities. There are roads, there are hospitals and several others. FromNairobi to Nakuru there is a highway, there should also be a highway between Kilifi and Kidubwe. Another thing is what we call affirmation action. Affirmative action should be enhanced in the Kenyan government.

Next is primary education. There should be a compulsory scheme for every member, ama for every child to be educated at the primary level, whether the father or the mother likes it or not. But the government has to ensure that all children at home go to school. O.K. there is this one, when elections are to start, there are campaigns. So you know, Ngilu can come to campaign at Matanomano there, but there are these KANU aspirants, they disrupti her campaigns. I would like that to be abolished. If Ngilu comes to campaign, give her the freedom of campaigning and there should be no disruptions.

There are what we call the powers of the President. The powers of the President have to be minimized. Infact, I would like the head of the Electoral Commission to be elected by the house or the national assembly. I would also like the mayor, the civic candidates, the chiefs and the sub-chiefs to be educated. They should have taken humanities in secondary schools. (interjection). In secondary and not only in secondary schools, but they should have taken humanities even in colleges Humanities will include geography, history …

**Com. Lethome:** Please wind up.

**Japeth Kisau Karisa**: O.K. Last point. There are what we call parastatals. I want all the Parastatals in Kenya, including the Kenya Ports Authority, the Kenya Revenue Authority, the Kenya Airport Authority to be managed by the locals, but only to be controlled by the government. Thank you.

**Com. Lethome:** Asante, jiandikishe pale. Tumpate Simon Chengo.

**Simon Chengo Rua:** Haya, kwa jina mimi ni Simon Chengo Rua. Na maoni yangu ndiyo haya. Number one, Katiba mpya hii ambayo tunaiunda, iwape uwezo wananchi kumpigia kura ya kutokuwa na imani na diwani au mbunge huyu baada ya kipindi cha miaka mitatu ikiwa kwamba hafanyi lolote. Ikiwa anafaa, arudishwe. Na kama hafai, achaguliwe mwingine. Hayo ni maoni yangu.

Oni la pili, Katiba mpya iwape uwezo manaibu wa chif, kuandikwa uchifu wakati chiefu amestaafu badala ya kuandikwa mtu asiyejua kazi halafu aanze kufundishwa na sub-chief huyo, si vizuri. Ya tatu, Katiba hii mpya iwape uwezo machifu na manaibu wao, kupewa vifaa vya kusafiria, ma-honda au 'vespass' za kusafiria hapa na pale, Kufanya kazi zao kuwa rahisi.

Kuhusu elimu, Katiba mpya iwape uwezo walimu mashuleni kuwaadhibu wanafunzi wao wakati wanapokosea adhabu shuleni ili tuepukane na mizozo mashuleni. Number tano, bibi yeyote akikosana na bwanake, aende kwao siyo kwenda kwa chifu au polisi na mwisho kumfunga bwanake, labda awe amekatwa panga ama amekatwa kisu.

Ya mwisho, Rais wa Jamuhuri hii, atawale kwa miaka kumi na tano ndipo kuwe na uchaguzi mwingine. Asante.

**Com. Lethome:** Haya, bibi amegombana na mumewe, pengine amepigwa kofi, hakukatwa panga, lakini amepigwa. Hapo unasema asiende kushtaki mahali popote, aende nyumbani kwao?

**Simon Chengo Rua**: Yeye ana babake kwao, na anakosana na bwanake amepigwa. Haikosi labda amekosa kwa hivyo aendee kwa babake na sio kwa chief ama sub-chief.

**Com. Lethome**: Haya, kutoka hapo ni bibi amepigwa na mumeo kwa sababu ya makosa fulani, kawaida hupigwa akifanya makosa. Haya, na mume naye akifanya kosa? Mume amefanya kosa nyumbani, akipigwa na mkewe?

**Simon Chengo Rua:** Akipigiwa na mkewe?

**Com. Lethome:** Ndiyo. Alipigwa baada ya kufanya kosa. Si wote wawili ni…

**Simon Chengo Rua:** Ndiyo, akipigwa na mkewe, ikiwa mume amepigwa na mkewe kwa makosa, wazazi wa bwana na wazazi wa bibi, waketi kusuhulisha.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo bwana akimbie kwa wazazi wake?

**Simon Chengo Rua:** Si atakuwa amepigwa pale kwao, kwake pale, wazazi wake wako pale, basi wazazi wa bibi waitwe

washikane na wazazi wa bwana wasuluhishe matatizo kabla kwenda polisi au kwa chief.

**Com. Lethome:** Chengo Kistau Kizima, afuatwe na Karisa Kalua Tuva. Utabaki hapo, utafuatwa na Chengo Kisao. Haya utamfuata huyo. Pendekeza haraka haraka, muda naona umebaki mdogo. Na nyuma tukae kimya tuweze kusikiza tafadhalini.

**Karisa Kalua** : Mimi la kwanza … mimi ni Karisa Kalua Tuva. Kwanza ma-sub-chifu na chifu wapigiwe kura, badala ya kupewa uongozi tu, tena wapate transfer na kuondolewa kwenda kule, na mwingine kuja hapa.

Pili, kuna mila, mila zetu. Mganga wa ngoma ambayo ni mila, huja wakati kama kuna matatizo mahali fulani ameitwa, lakini huwa na kibali kutoka huko, aliandikiwa anacho. Lakini akifika hapa mpaka aingie kwa ma-sub-chifu apate kingine au kwa chifu halafu inakuwa matatizo. Pendekezo langu, akiandikiwa huko, awe hawezi kuja atafute ingine hapa, awe anaweza kufanya ile kazi.

Ingine ni hivi, kuna viosks na maduka. Kwanza kiosk ni kitu kidogo sana ambacho mtu huwa anaanza. Basi wakati akianza, huwa anataka kuingiliwa kukata karatasi kabla ya yeye hajajiendeleza. Ningependekeza hivi, kwamba aendelee mwaka mzima halafu ndio akimaliza, awe anaweza kupata licence ya shilingi mia moja tu peke yake kwa mwaka. Jambo lingine ni majimbo. Na Pendelea majimbo. Serikali iwe ya majimbo. Halafu kwa yule ambaye atashikilia kama kwa kuendesha majimbo, kama ni kura iwe ni miaka mitano ndio aondolewe, kuwe kunaweza kuingia mwingine.

Mambo mengine ni kuhusu askari. Kuna askari game, na askari MP. Ningependekeza kila mmoja ajue kazi yake, si kuingilia mwingine. Hata ikiwa yule ni wa wanyama, anawacha mambo ya wanyama anakuja kushikilia kama pombe, au mambo mengine ya vita. Kila mmoja ashike ili kazi yake. Nimemaliza.

**Com. Lethome**: Asante sana Bwana Karisa. Tupate sasa Chengo Kitsau. (interjection) Kisima? Haya Bwana Kisima njoo. Danson yuko? Danson Lugaje Masha? Utamfuata huyu bwana?

**Chengo Kitsao Kisima**: Jina langu ni Chengo Kitsao Kisima. Ningependekeza hivi, tuwe na majimbo. Hilo ni la kwanza. La pili, ma-sub-chifu, na chifu, hata DO, DC, wote wapigiwe kura maanake wale ni watu wakuweka mikutano na kusikizwa na wananchi. Basi siendelei sana. Ni hayo.

**Com. Lethome**: Asante sana. Danson ? Katana Masha Baya? Utamfuata huyu bwana.

**Danson Luganje Masha**: Kwa majina naitwa Danson Luganje Masha. Kwanza nitaanza na the side of councillors. Ningependekeza councillor yeyote altakayechaguliwa awe ana elimu ya kutosha kwa sababu … (interejction). Awe na kiwango cha kusoma kama darasa la nane na kwenda mbele. Kwa sababu wale ambao hawakusoma, wao hata ndio wanaturegesha

nyuma kabisa.

La pili ningependekeza ma-assistant chief wetu, kwa sababu ndio watu ambao wako karibu kabisa na wananchi, wawe na elimu ya kutosha, kuanzia form four, hata university. La tatu, ningependekeza tuwe na serikali ya majimbo ili kila jimbo liwe linaweza likajisimamia lenyewe. Ya nne ningependekeza Rais aweze kutawala kwa miaka kumi. Miaka mitano ya kwanza, halafu miaka mitano ya pili kisha aachie mwingine.

La tano, ningependekeza mbunge wetu achaguliwapo, awe anaweza kuwa na ofisi yake karibu na wananchi. Haitakuwa vyema uwe unafanya kumjua mbunge nyumbani kwake, unajua Jumamosi anakuja, watu wanajazana kama hivio ambvyo tuko hapa, kila mtu akipenda kumuona mbunge. Itakuwa ni vigumu kusikiza malalamishi ya watu wake.

La sita, ningependekeza DO wetu awe ni mtu ambaye anajulikana na raia. Hata kama sikosei, kwa sasa kuna wengi sana hapa hawajui hata jina la DO wao ni nani. Kwa sababu ni mtu wa kutoka sehemu zingine. Napendekeza DO awe anatoka mkoa ule . Kwa hayo machache, Asante.

**Com. Lethome:** Asante sana, jiandikishe. Katana Baya nafasi ni yako Baada ya Katana, kuna Katana mwingine lakini Katana Menza. Katana Menza upo? Haya utamfuata huyo.

**Katana Masha Baya**: Kwa jina naitwa Katana Masha Baya. Pendekezo langu la kwanza ni kuhusu wazee wa kijiji. Wapate mshahara.

**Com. Lethome:** Maoni yake, maoni yake yaheshimiwe.

**Katana Masha Baya**: Pili, ni upande wa skuli. Kutoka class cha kwanza mpaka class cha nane, iwe bure. Tatu, title deeds zitoleweshwe bure, tusitozwe. Ni hayo matatu.

**Com. Lethome**: Asante, jiandikishe pale. Katana Menza? Na afuatwe na Robert Silia. Robert Silia upo? Utamfuata huyu bwana.

**Katana Menza**: Kwa Jina mimi ni Katana Menza. Mimi pendekezo langu,

**Com. Lethome:** Anza kwa jina.

**Katana Menza:** Jina ni Katana Menza.

**Com. Lethome:** Wale wako nyuma wanafanya shingo hivi wanataka tunataka kusikia. Ongeza sauti.

**Katana Menza:** Nitasema kwa sauti ya juu. Ningependelea hivi kuhusu Katiba hii ambayo tunaiunda. Kuwe na Rais ambaye anaweza kutawala kwa miaka mitano halafu apigiwe kura tena baada ya miaka mitano. Mbunge vile vile, naye awe kama hivyo. Kuna hawa ma-sub-chief mpaka chifu, vile ambavyo wanatoka hapa hapa kwa area ya location hii hii, kuwe kuna askari ambao tunaweza tukawapata kwa chifu na kwa DO2 kwa ufupi kwa sababu DO ndio kwenye askari lakini kwa chifu hakuna.

Lengine, ni kuhusu elimu. Elimu, wazazi tunaumia na majengo tunajenga na pesa tunatoa. Kwa hivyo tungependa hiyo mambo ya pesa iondolewe kabisa, tuwe tunajenga mashule kwa uwezo wetu. Na lingine ni kuhusu barabara. Barabara zetu ni mbovu zote…

**Com. Lethome:** Jamani tukaeni kimya, tusikizeni Endelea.

**Katana Menza:** Kutoka hapa mpaka Kilifi, huwa tunasafiri kwa pesa nyingi sana na ni karibu sana. Na ukiuliza wenye magari wanasema barabara ni mbaya. Kwa hivyo langu la mwisho ni hilo.

**Com. Lethome:** Asante sana. Robert Silia. Robert karibia. Ronald Mwanzombo. Mwanzombo yuko? Haya, baada ya huyu mzee ni wewe.

**Robert Silia:** Point yangu ya kwanza… (interjection), jina ni Robert Silia. Point yangu ya kwanza ni kwamba ningependelea kwamba, katika serikali ijayo, iwe ya majimbo. Point yangu ya pili ni kuhusu mambo ya mashamba. Kwamba baada ya upimaji wa mashamba kumalizika, ile haki ya mashamba itolewe mara moja. Kumekuwa na hali kwamba - - hapo nikitaka kufafanua kumekuwa na hali ya kwamba upimaji ukiwa umeendelea na kuna kesi hapo ndani, inakuwa kwamba hata munaweza kumaliza hata miaka kumi kwa kuwa wengine hawajaelewana. Hiyo isiweko. Wale watakuwa wamepimiwa na imekubalika wapewe haki yao na wale ambao watakuwa na kesi ziendelee. Wale ambao watakuwa wao wamepimiwa, wapatiwe haki zao mara moja bila kuchelewa.

Katika serikali za wilaya, kuhusiana na mambo ya madiwani, viwango vya elimu iwe ni kutoka darasa la saba na kuendelea. Point ya nne, ni kwamba kuhusiana na ma-chief na ma-sub-chifu, iwe hawa wanachaguliwa kwa kura. Lakini iwe huyo chifu anaweza kuendelea. Kila wakati anachaguliwa anaweza kuendelea hata akastaafu ikiwezekana kama ni mzuri anaweza kuendelea mpaka akafikisha umri wake wa kustaafu.

Point nyingine ni kuhusu malipo ya uzeeni. Haya malipo ya uzeeni ni kwamba, mfanyaji yeyote yule wa serikali, vile akipewa ile barua ya kustaafu, apewe pamoja na cheque yake ya pesa zake za uzeeni. Bila hivyo, asipewe hiyo barua ya kustaafu.

Ziambatane na cheque ya yale marupurupu yake.

Point ya tano ni kwamba kumekuwa na ulegevu kuhusu hali inavyochukuliwa hawa walemavu. Walemavu kama vipofu, wale viwete na wale ambao hawawezi kuongea. Hawa watu, kuwe na mkazo ili kwamba waweze, katika kila kijiji na kila sub-location na location, waweze kujulikana watu hawa ni wangapi katika ile sehemu na serikali itenge pesa ambazo zitaweza kugharamia hawa watu ili kwamba waweze kusaidika katika ile hali yao ya ulemavu. Asanteni sana.

**Com. Lethome:** Haya, asante sana bwana Robert.

**Ronald Mwazombo**: Ronald Mwazombo ni jina langu. Napendekeza kuwa vipindi vya Rais viwe viwili vya miaka mitano mitano. Iwe hivyo mpaka ma-councillors na hata machifu na ma-sub-chifu. (interjection) Eh, kwa vipindi viwili.

Kwa upande wa ardhi, mkaaji wa pale awe anapewa nafasi ya kwanza badala ya mgeni. Kwa upande wa urithi, baba na mama wawe na haki sawa. Mali asili, wakaaji wa pale wawe ndio wanahusika. Maji yawe yatakuwa na bei kiwango kile ambacho wananchi wa mashambani wataweza kujimudu. Mambo ya license. Iwe hali inayotofautishwa kwa upande wa mjini na upande wa mashambani.

Kielimu, kuwe na - - kutoka class ya kwanza mpaka kidato cha nne, iwe itakuwa bure. Ni hayo ndiyo niko nayo. Asanteni.

**Com. Lethome:** haya, asante sana bwana Mwazombo. Kadenge (inaudible). Kazungu Kirao? Mtafuatana hivi. Kadenge mwanzo halafu Kazungu na Daniel pia akae tayari.

**Kadenge Mbuvi Chare**: Mimi naitwa Kadenge Mbuvi Chare.

**Com. Lethome:** Sauti mzee.

**Kadenge Mbuvi Chare:** Sauti ni ugonjwa. Mimi ninataka serikali ya majimbo. Serikali ya majimbo. Na sub-chief pia wachaguliwe na wananchi wenyewe. Barabara zetu zifanywe mshaada tupate kwenda Kilifi mapema. Serikali itusaidiye tutengeneze barabara. Makaratasi ya mashamba tupate mara moja. Ni hayo tu.

**Com. Lethome**: Asante sana mzee Kadenge. Haya, Daniel Keah ukae tayaru.

**Kazungu Kirao**: kwa jina naitwa Kazungu Kirao.

**Com. Lethome:** Kazungu wewe ni kijana tuoa sauti bwana.

**Kazungu Kirao**: Mimi pendekezo langu ni kwamba, ningependa kabisa serikali iwe ni ile ile ya umoja lakini chiefu sub-chiefu wachaguliwe na wananchi wenyewe. Hosptiali ziletwe hapa karibu. Barabara zetu zitengezwe, ziwe (inaudible) nauli yetu ya magari ipunguzwe. Hali ya kwenda shtaki uambiwe utoe pesa hapa kwa chiefu hiyo iondolewe. Elimu. Elimu kuanzia daras la kwanza mpaka la nane, iwe wanalipa pesa lakini kuendelea juu, kuanzia form one form two kule, serikali ichukuwe isomeshe watoto. Basi, sina mengi.

**Com. Lethome**: Asante sana bwana Kazungu. Daniel Keah?

**Daniel Keah:** Kwa jina Daniel Keah, mapendekezo yangu nasema katiba mpya hii rais anapochaguliwa, aweze kutawala miaka mitano na iwapo hata tengeneza vizur, basi anaweza kuondolewa na minister wake akashikilia wajibu wake.

Pili, serikali iwe ya majimbo. Tatu, ma-councilor haidhuru awe hana elimu ile inatakikana kama kidato cha nane kuendelea, lakini ikiwa anaendesha vizuri kazi yake, basi anaweza kuendelea. Na nne, kuhusu umilikiaji wa mashamba, tunasikitika katika kwa nchi yetu ni kwamba imerudi nyuma sana. Ukiangalia katika asilimia wanaoishi hawana vitambulisho za kumiliki katika ardhi zao kwa hivyo tunaona tunanyaganywa na hatuna uwezo maana hatuna haki kumilikia.

**Com. Lethome:** Pendekeza kuhusu vyeti.

**Daniel Keah:** Tunapendekeza kwamba serikali ifanye bidii kupatia vyeti wananchi ambao wanahusika na viwango vya mashamba. Tano, viongozi wa makanisa, ni kwamba waheshimiwa kama viongozi. Tunaona kwamba wameachwa nyuma sana, unakuta kiongozi anachukuliwa kama mtu wa kawaida na ikiwa yeye ni mtu wa kuheshimiwa katika Kenya yetu. Kwa hivyo tunahitaji viongozi wa makanisa waheshimiwe tena kiwango kile ambacho yaani, wahifadhi kuvitoa ili kusudi kusaidia makampuni, makanisa nayo ili yapate kutambulikana.

Sita, ni kwamba wakati wa mcolony, tunaona ya kwamba unga ulikuwa ni bei ya chini sana, hata hivyo tunapendekeza kwamba, urudi ule wa magunia pia mwananchi aweze kupimiwa kwa kilo ingawa nafuu ili apate kujisaidia. Saba. Barabara zinatakikana zitengenezwe, wakati serikali yetu inapochukuwa waarifu huo wa kutawala, barabara zetu zipate kutengenezwa na kutiliwa lami.

Nane, serikali yetu iwe ya muungano. Tisa, ushuru uondolewe. Ushuru uondolewe. (interjection). Sasa basi hapo undoa hapa ya muungano, sima hayo majimbo. Sima hayo majimbo.

**Com. Lethome:** Hebu tusikizeni jama, tusikizeni hapa, mambo makubwa yanatokea hapa. Haya.

**Daniel Keah:** Nane, ushuru uondolewe ili kusudi mtu wabiashara anapokwenda kunu kitu, awe anaweza kukitoa bila gharama yeyote. Tisa, kuna mila hizi ambazo ni za Kigiriama. Unakuta zinawekwa kwenye skuli, na tunakuta watoto wa skuli wanalazimishwa wengine ni Wakristo, lakini wanalazimishwa wawe watacheza katika zile mila, na mwingine anajifanya kuwa mganga, mwingine anajifanya kuwa mgonjwa halafu akitoka pale, yule mtoto wa Kikirsto, anaenda kushikwa na mapepo na anaanza kubadilika. Na pendekeza iondolewe mara moja. Katika skuli.

**Com. Lethome:** katika skuli, na nyumbani.

**Daniel Keah:** Katika manyumbani kwa yule ambaye anapendelea kufanya aendelee lakini yule ambaye hataki kupendelea aachwe hivyo hivyo, eh, awe na uhuru wake.

**Com.Lethome:** Asante mzee. Asante mzee. Ukiskiza hapa, utapata mawaidha mazuri sana. Haya tusikize Julius Tuva Konde. Yuko? Afuatwe na Rev. Jotham Obisa.

**Julius Tuva Konde:** Kwa jina ni Julius Tuva Konde. Ninapendekeza mashamba yapate vibali na serikali yetu iwe majimbo.

**Com. Lethome**: Toa sauti Bwana.

**Julisu Konde:** Majimbo!

**Com. Lethome:** Endelea, endelea.

**Julius Konde:** Na dini iendelee.

**Com. Lethome:** Uhuru wa kuabudu yaani, lakini watu waabudu Mungu si mashetani.

**Julius Konde:** Eh, Mungu si dini? Ya Kikirsto, sio ile ya mabumbumbu. Na watoto wakimaliza shule waajiriwe makazi. Na Rais wetu atawale kama miaka mitano. Na machifu na manaibu kama vile, lakini chifu na manaibu wake wachaguliwe na wananchi. Tosha hiyo.

**Com. Lethome:** Haya, Rev. Jotham Ombisa?

**Rev. Jotham Ombisa:** Majina ni Rev. Jotham Ombisa. Niendelee? Pendekezo langu ni kuhusu vyama vya kisiasa. Vyama vya kisiasa vikiwa vingi, vinaleta mambo mengine ambayo sio mazuri. Vina haribu watu. Ninapendekeza kwamba kuwe na vyama viwili au vitatu. Vyama viwili au vitatu, lakini sio kimoja, viwili au vitatu. Na vingine vifutiliwe mbali.

Jambo la pili, Rais aongoze nchi kwa muda wa miaka mitano. Kama kazi yake ni nzuri, miaka kumi. Na la tatu, Rais awe ni mtu wa makamu. Asiwe kijana.

**Com. Lethome:** Miaka, miaka, pendekeza miaka.

**Rev. Jotham Ombisa:** Miaka ya Rais? Ah, kuanzia miaka arobanne na tano (interjection)

**Com. Lethome:** Hadi miaka mingapi?

**Rev. Jotham Ombisa:** Kuendelea mbele tu

**Com. Lethome** Mpaka mia moja?

**Jotham Ombisa:** Ah Ah, akiwa mzee basi na apumzike.

**Com. Lethome:** Mzee wa miaka ngapi?

**Jotham Ombisa:** Aendelee kama mpaka miaka sitini au sitini na tano. Jambo lingine ni kwamba raia, raia wapewe mikopo bila masharti. Kama hawa ambao wanafanya kazi ndogo ndogo za biashara, wadhaminiwe na chief au na agricultural instructor. kama hao wanachukua mikopo ya ki-agriculture, wadhaminiwe na hao, halafu wapate mikopo ambayo wanataka, waendeleze biashara zao, au kazi zao ndiyo tupate kuendelea.

Na la tano, nidhamu shuleni imerudi nyuma sababu wameondoa management ya makanisa. Wakati tulikuwa na management za makanisa, hatukuwa na mchafuko katika mashule. Na hii ni kwa sababu vijana hawahubiriwi neno la Mungu ambalo litawafanya wawe watu wazuri. Kwa hivi napendekeza kwamba shule zirudishwe katika management ya makanisa. Nafikiri ni hayo tu.

**Com. Lethome:** Asante sana Rev. Haya Charles Pasi, huko? Haya karibia, nafasi ni yako. Afuatwe na Zozi Kazungu. Zozi Kazungu yuko? Kama hayuko gari linampita. Oh, yuko. Mama kaa karibu. Haya. Haya endelea Charles.

**Charles Pasi**: Kwa jina ni Charles Pasi, kutoka hapa Maganomane, Vitengeni. Kwanza ninaanzia na huku nyumbani kuhusu mambo ya ardhi. Mambo ya ardhi katika sehemu hii yetu imekuwa mbaya kwa muda mrefu, tunapimiwa mashamba, kufikia sasa tuna karibu miaka kumi na sita kutoka mashamba yale yapimwe lakini hujapata karatasi yeyote ambayo mwananchi anaweza kujisaidia nayo. Kwa hivyo ningependekeza kwamba kipengele kile ambacho kinafanya kwamba shamba zile, katika

section hiyo ikifunguliwa katika shamba zile, zikiwa zina kesi mbili au tatu, kwa watu mia nne, hawawezi kupata zile karatasi. Kwa hivyo ningesema kipengele kile kiondolewe ili kwamba ile section ikifunguliwa na ikimalizika, waorodheshe wale ambao hawana matatizo, wapatiwe vyeti vyao ili kwamba wakaweze kujisaidia manyumbani kwao. Na wale ambao wana kesi waendelee vile kuzozana mpaka wakimaliza nao watafanywa nini? Watapatiwa. Na ni (a).

(b) Hapa hapo kwa mashamba, ningependekeza kwamba, bwana na bibi wakiwa wanajiandikisha kwenye shamba, ile title deed itoke na majina mawili; ya bwana na bibi. Ili kuondoa ule mzozo ambao mara kwa mara unasikia, mara shemeji amepokonywa shamba, mara shemeji amepokonywa kiwanja cha nyumba, ile inakuwa matatizo, lakini nafikiri ikitoka na majina mawili, iwe ni bwana amekufa, mama anashikilia nafasi ile ya shamba. Ikiwa ni bibi amekufa, bwana anashikilia ile nafasi ile ya shamba ili kuondoa ule mzozo unaoendelea.

(c) Katika hapo mashambani vile vile, malipo ya mashamba vile vile, isilinganishwe na kule kwenye ma-beach. Ya huku reserve yawe yanaweza kurudishwa chini kidogo, ili kwamba hawa watu wanatoka huku nao wakaweze kujimudu kutokana na yale malipo. Kwa sababu wakilinganisha sehemu zile ma-beach, kule inaonekana hali yake iko juu sana. Kwa hivyo iwe na ipungufu yaani, iweze kurudishwa chini kidogo.

Wanyama wa pori; Mambo ya wanyama wa pori ni kwamba inasikitisha kwamba mtu anaweza kuuawa na ndovu au akaliwa na simba, lakini ukiangalia katika malipo, unakuta mtu anaweza kulipwa shilingi elfu sita, elfu tisa na amepoteza mtu. Sasa vile inaonekana ni vile ambavyo maisha ya mtu hayana maana sana. Kwa hivyo mimi ningependekeza kwamba, ikiwa kile kipengele kinaweza kikaondolewa, iwe mtu anaweza kulipwa kama laki tatu au laki nne, ili kwamba kufidia wale watoto wake pengine wanataka kusoma, hawana masomo ya kuendeleza katika zile sehemu vilivyo.

(b) Mimea pia ikiliwa siku hizi hailipwi. Kwa hivyo ningependekeza, mnyama yeyote akiharibu mimea ya wananchi, ikaweze kulipwa kulingana na vile ambavyo itafanywa assessment.

Elimu; Elimu ningependekeza kutoka zile shule za malezi mpaka darasa la nane, serikali iweze kuchukua watoto wale kusoma bure.

(b) katika elimu, ningependekeza katika mikoa hii minane, angalau kuwe na chuo kimoja kikuu katika kila mkoa, ili kwamba watu wafaidike. Maana sasa ukiangalia, vile vyuo vikuu vyote viko huko ng'ambo ya juu huko. Kwa hivyo ikiwa vile itakuwa imesaidia wananchi ambao pengine wako huku.

Malipo ya uzeeni; Hii ningependekeza kuwe na mabadiliko ambayo yangesaidia wale wazee wanaolipwa. Maana unasikia inazungumuzwa kwa mdomo kwamba wanalipwa lakini mzee anaweza kupita pita n Kilifi karibu safari kumi na tano, akifika pale hakuna pesa, hakuna pesa, hakuna pesa. Kuwe na mpango maalum ambao wazee pal wakifika pale watakuwa wanaweza

kupata malipo yao.

Kisha, (b) Yale maongezeko wanaoongezewa wale wanfanyikazi; na wale wazee pia nao waweze kuongozewa kama vile wafanyikazi wanavyofanya kazi kwa sababu walikuwa wafanyi kazi huko nyuma katika hivyo. (interjection)… Serikali, (laughing). Mbona unataka kuniharakisha? Serikali ile ambayo tungetaka iweko, tungeomba kwamba serikali hiyo itakayo kuja iwe serikali ya majimbo, iwe na Rais, na iwe na Makamu wa Rais , na pia kuwe na Waziri Mkuu ambaye ataangalia zile sehemu zile (inaudible) serikali. Na, hizi mikoa ambayo ndiyo majimbo, zipewe uwezo zaidi, kwa kuandika wafanyikazi na kufuta wafanyikazi kama vile serikali kuu ilivyokuwa ikifanya hapo nyuma. Kwa hivyo hiyo, ikifanyika hivyo, itasaidia watoto wetu wengi ambao wanakaa katika sehemu ya mikoa hii, wanaweza wakaandikishwa kazi katika mikoa yao hii.

Madiwani; Madiwani ningetaka wawe wakilipwa na serikali kuu kama vile ambayo wajumbe wanavyolipwa, na madiwani pia walipwe vile vile, na serikali. Wasilipwe na mabaraza kwa sababu mabaraza mengi hayana pesa. Kwa hivyo wakilipwa na serikali nafikiri ingekuwa ni bora kushinda mambo mengine. Shukrani. Ninge endelea zaidi lakini haya …

**Com. Lethome:** Zozi Kazungu, Sidi Karisa. Uko aribu Sidi, Sidi Karisa, atakuwa ni mama huyu? Ngoja. Esther, unakazi hapa. Ngoja mama.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Anasikitika na hawa watoto wa shule.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Hawaendi shule kwa sababu tunaambiwe tutoe mapeni.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Tutowe mapeni.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Na tunaambiwa kuna msaada.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Anasikitika na hawa watoto wa shule, kwa kuwa kwa kifupi, anasikitika na hao watoto wa shule kwa sababu mara ingine yeye hutoa pesa ambazo ni za tuition halafu baadye wale watoto wanarudishwa nyumbani.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Yeye anapendekeza kwamba elimu iwe bure.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Angependa hii elimu ya primary iwe free.

**Zozi Kazungu**: *(In giriama dialect)*

**Translator**: Basi hayo, oni lake yeye lilikuwa ni free education, ndio alikuwa anasisitiza.

**Com. Lethome:** Huyu Sidi Karisa hayuko? Tumpate Sidi. Zawadi akae tayari, Zawadi Karisa Baya. Haya endelea. Haya anza kwa majina yako, mama tuambie unaitwaje.

**Sidi Kitsao:** *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Sina mambo mengi hivi. Endelea. (*In giriama dialect*)

**Sidi Kitsao:** *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Huyu mama nafikiri ni msikizaji lakini hana maoni.

**Com. Lethome:** Haya asante mama. Zawadi?

**Zawadi Karisa Baya**: Jukumu langu mimi ni Rais aendelee kwa miaka kumi na kuendelea mbele. Barabara itengenezwe maanake tikiti ndizo ambazo zinakuwa ghali kwa barabara. Watoto wetu wasome. Wasome kuendelea kutoka class cha kwanza mpaka wamalize kabisa maanake hatutaki mtoto yeyote abaki nyumbani. Wasome mpaka wamalize.

**Com. Lethome:** Na kama hakuna pesa?

**Zawadi Karisa:** Ikiwa hakuna pesa, tunataka hapo paangaliwe hapo.

**Com. Lethome:** Masomo ya bure au vipi?

**Zawadi Karisa:** Masomo ya bure!

**Com. Lethome:** Mbona unaogopa kusema, sema.

**Zawadi Karisa:** Masomo yawe ya bure.

**Com. Lenaola:** Mpaka kiwango gani?

**Zawadi Karisa:** Mpaka wamalize form four. Akimaliza form four, akiwa anagojea majibu, asikae nyumbani. Awe na msaada kidogo wa kujusaidia, wa kujishikia shikia angojee majibu yake, kuliko kuzurura zurura humu humu.

**Com. Lethome:** Apewe msaada ama apewe kazi?

**Zawadi Karisa:** Apewe kazi, apate kazi. Ajishikie, kungojea majibu yake ya form four. Kama hivi polytechnic, kama cherahani, ama ile carpentry, kuliko kuzurura zurura humu humu, manyumbani. Nyingine ni hivi, walimu wa shule wanafunza watoto wetu, na kwa nini mwalimu akiwa ametia mtoto shule, mimba anaajiriwa? Je akiwa kama ni mtoto wa shule na ametiwa mimba na mvulana wa huko nje? Hapo tunataka tuchukuliwe hatua hapo naye.

**Com. Lethome**: Kama kijana amemtia msichana mimba?

**Zawadi Karisa:** Ametia msichana mimba, achukuliwe hatua hii, maanake huyu msichana, atakuwa ameelewana na yule mvulana, na sasa huyu bwana huyu, atakuwa anamdanganya. Atakuwa yeye yuko shule na huyu naye atakuwa hayuko shule. Sasa huyu ambaye atakuwa hayuko shule, atamtemba huyu msichana ambaye atakuwa yuko shule. Sasa tunataka achukuliwe hatua. Hatua yenyewe ni hivi; tunataka huyu mvulana naye achukuliwe hatua ile ambayo mwalimu naye achukuliwe hatua kama hiyo, ikiwa ni kufungwa, afungwe. Tusimlazimisha mtoto wa kike, ukamlazimisha kupata bwana halafu akaenda kukaa naye muda. Maanake siku hizi, msichana akitiwa mimba, kumulazimisha kupata mvulana, anaenda kukaa na yeye nyumbani. Miaka miwili au mitatu, anasema “Ah! Sitatoa kitu, tena anajua hata mimi sitampatia chochote, sitampa sabuni sitamununulia nguo. Hata akisinywa yeye, aende zake nyumbani kabisa”. Sasa hapo nataka kuchukuliwe hatua hapo kwa mzazi wa kike na mzazi wa bwana. Hapo kuwe na hatua hiyo. Hawa waungane hawa wazazi wawili hawa na watoto wao.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo huyu kijana ashikwe na ahukumiwe?

**Zawadi Karisa:** Huyu kijana, akihukumiwa mimi sitapata kitu. Lakini ni hivi, ninataka huyu bwana, huyu kijana na mzazi wake, na mimi, tuungane pamoja. Kuliko aende kule, halafu naachiwa machanga hapa nyumbani, na mtoto wangu hapa azae tena. Sasa mimi nataka hivi, huyu mvulana na babake, na mimi na msichana wangu, tuungane pamoja kwanza, tuelewane. Ikiwa hatutaungana, hatutaelewana. Hapo sasa tutakutana pale tabajane sasa. Umuchukulie hatua kali. Mimi yangu ilikuwa na hivyo. Na ni hivi tena, poleni. Ni la ngapi hilo? La tano. Nataka niongee la sita. Hilo la sita basi ni la mwisho hilo.

Kuna hivi, mimi nimeolewa na bwanangu. Nimezaa, hata nimechoka, sizae tena. Bwanangu mimi nampenda lakini hapo katikati tujetukosane. Je mimi, hapo nikiondoka tutagawana mali? Ama tuchukuliane hatua ile nzuri ambayo inafaa, ya bibi na bwana. Isije mimi nikawa nimekuwachia watoto wako wote, na mimi nilikuwa nakupenda, wewe bwanangu hatukukosana, tena mambo kidogo hivyo wasema "Haya basi nenda kwenyu, sikutaki tena! Kwanza uniachie watoto wangu." Halafu wewe unawachukua wale watoto wote, mimi nabaki pale pale. Tena narudi nyuma tena nasema, "Basi mimi boko nataka mali yangu". Hapo nataka kuwe na sheria hapo. Yachunguliwe mambo hayo. Bwana asiache bibi yake hivi hivi kabla ya hatua ambayo siyo. Sasa hapo, nataka paangaliwe hapo. Mimi nikiondoka nikiwa nimekosana na yule bwanangu nataka nikienda kwa kuwa sizai tena, hapo tena nijue hakuna chake tena kule. Si awe basi nimepewa elfu tatu, tano, na sirudi tena, watoto wake nao awachukuwe wote, eh! Hapo nataka pachukuliwe hatua sana hapo. Na nisimalize wiki….

**Com. Lethome:** Jonathan Karisa? Jonathan Karisa yuko? Raphael Watamo, kama Karisa hayuko Raphael Watano. Hayuko? Gachugu yuko? Katana Charo Jefa? Jefa? Haya njoo njoo. Afatwe na Keah Kavindo. Keah Kavindo yuko? Haya utamfuata Keah.

**Katana Charo Jefa**: Kwa jina naitwa Katana Charo Jefa, kutoka vitengeni.

**Com. Lethome:** Tusikize huku kina mama hapo wanafanya fanya mikutano yao hapo, tafadhalini. Mutapewa red card kama ile ya mpira, haya !

**Katana Charo Jefa**: Mimi sina mengi. Yangu labda ni matatu hivi. Kwanza, Rais awe na uwezo wa kuweza kuongoza jamii yake yote ya Kenya nzima hii. Pili, serikali zinafaa ziwe mbili. Majimbo, na hiyo nyingine ilioko. Hizo mbili. Tatu, ma chief waregeshewe mamlaka kama vile zamani walivyokuwa sababu wanadharaulika sana hata kukunjiwa ngumi maofisini, wanakunjiwa ngumi. Nne, barabara. Tunahitaji iwekwe lami kuanzia Kilifi mpaka Vitengeni, mambo hayo - - tumechoka kushikwa na matope hapa chini. Yangu ni hayo tu, asanteni.

**Com. Lethome:** Haya, Keah Kavindo, Keah? Dhahabu awe tayari, Dhahabu? Dhahabu yuko? Haya, tuendelana Kavinda. Lawrence Charo? Utafuata. Endelea.

**Keah Kavindo**: Mimi napendekeza kwamba serikali ya Kenya iwe ya majimbo kwa kuwa vile ile ya umoja imenyanyasa hasa

watu wa Pwani. Ya pili, watoto wetu wapatiwe kazi katika mashirika. Kuna mashirika mengi sana ambayo hakuna watoto wetu huko. Ukienda yamejaa watu kabisa. Lakini utakuta hapo, hata ile sauti utaisikia ni ya mtu ambaye humjui. Wale watu wamekuja wa kutoka bara, wajaha wakaja wakaingizwa kazini mara moja na wewe ukienda kuuliza pale unaambiwa pale pameandikwa hakuna kazi. Hicho kitu tunataka iondolewe. Watu Pwani kwanza wapatiwe nafasi wawe number one. Kazi hizi katika yale mashirika makubwa, wale watakuwa wengi wawe watoto wa Pwani. Pili, hiyo tatu.

Tatu, rasilimali zetu za Pwani ziweze kuwa na faida. Tunaona kila ikitangawa kinatangazwa kahawa tu, kahawa tu. Lakini hapa kwetu hakutangazwi chochote. Kwa hivyo hapa kuna mnazi, kuna mikorosho, iweze kuwa rasilimali, tuweze kupata wale walimu wa kututengenezea hii miti, iweze kutoa pesa kushinda ile mikahawa. Na kutoka sasa napendekeza, ile mikahawa. isitangazwe tena mpaka hii mikorosho irekebishwe. Halafu ianze kutangazwa mikorosho ndio itangazwe mikahawa.

Jambo lingine ni kwamba, kila college inajengwa Bara. Hata ile ya Utalii, Utalii uko hapa lakini ilipelekwa huko. Sijui wale watu walikuwa na akili kweli. Ningependekeza hizo college mwaka huu ziwe zemeletwa hapa. Mwaka huu usimalizike ziletwe hapa, kama ile college ya Utalii, le college ya Utalii. iletwe hapa, na zile college nyingine ambazo zinastahili kuwa Pwani ziletwe hapa. Halafu nao watoto wetu wawe hawatapata hasara.

Ingine ni kuhusu hasa college hata hizi za walimu. Utasikia shilingi sitini elfu, mtu anakwenda kusomea hiyo. Zamani hii ilikuwa ni ya bure. Hizo pesa zote zinakwenda wapi? Ninapendekeza hicho kitu kiondolewe kabisa, kisiweko. Jambo lingine ni harambee, kuhusu harambee. Hizi harambee zinafanywa na wazee wa vijiji huko, "lete shilling mia moja, lete shillingi mia moja mzee atakuwa na harambee hapa". Au tuseme councillor atakuwa na harambee. Haya, "lete tufanye fanye hii halafu tukahesabu. Hiyo harambee kutoka leo isitolewe kabisa! Kama mtu anataka harambee aweke mkutano wake hapo wa harambee, atualike tutakuja mpa kile anachotaka lakini yale mambo ya kuambiwa utocho pesa halafu zikifika huko zinakuwa zinaliwa, ningependa hata wale ambao walihusika na hio kitu, waache kutoka leo, wasiendelee. Yangu ni hayo.

**Com. Lethome**: Haya Lawrence Chai. Joseph Ngolo, Joseph Ngolo yuko? Haya fuataneni hivyo

**Lawrence Chai Sheikh**: Kwa jina naitwa Lawerence Chai Sheikh. Number ya kwanza, Rais achaguliwe kwa miaka kumi. Pili, karo za shule ziondolewe. Tatu…..

**Com. Lethome**: Karo za shule ziondolewe katika kiwango gani?

**Lawrence Chai Sheikh:** Kuanza darasa la kwanza mpaka form four. Haya, ma chief wapigiwe kura. Magari ya kubeba wagonjwa yaletwe mahospitalini. Karo za hospitali ziondolewe. Sawa. Mchawi akishikwa na ngoma za kienyeji, apelekwe kortini, ahukumiwe.

**Com. Lethome**: Maoni yake, muachie.

**Lawrence Chai Sheikh:** Maoni yangu hayo. Kuwe na majimbo Pwani.

**Com. Lethome**: Pwani peke yake? Maoni yake

**Lawrence Chai Sheikh:** Pwani! Maoni yangu hayo lakini. Mtu akiwa amekufa, kama kujitia kitanzi, na aje achukuliwe na maaskari polisi kupelekwa huko Kilifi, napendekeza akifika huko, arudishwe na hao polisi. Kuhusu wazee wa vijiji, wapatiwe mshahara. Mwisho.

**Com. Lethome**: Wewe utatuambia ukweli wewe, wewe ni mmoja wao?

**Joseph Ngolo:** Mimi kwa jina naitwa Joseph Ngolo. La kwanza na sisitiza majimbo. La pili ni mambo ya ma-councillor. Hawa ma-coucillor napendekeza si lazima mtu awe na elimu. Tunataka yule ambaye atatusaidia. Kwa hivyo si lazima wawe na elimu hawa ma councillor. Kitu kingine ni habari ya ma assistant chief na chifu. Wale wapigiwe kura na wananchi wenyewe. Na lingine ni kuhusu habari ya huu msitu. Msitu ule, mule ndani muna ndovu wengi sana. Wanakula mimea ya watu huko nje na wanaua na watu wakidai, serikali inasema kwamba haina pesa. Kwa hivyo, kupendekeza kwangu mimi, ikiwa serikali haitakuwa na pesa, waingize wire wale ndovu wasitoke nje. (Interjection)

**Com. Lethome: Na wakitoka na wamuue mtu?**

**Jospesh Ngolo:** Lingine - - Wakitoka, sasa itakuwa ni vita. Tukimuua sisi, ni sawa.

**Com. Lethome**: Na ikiwa watatoka wawaumize, wamuue?

**Jospesh Ngolo:** Wakitoka sasa itakuwa ni vita. Tukimuua sisi itakuwa ni sawa, akituua yeye pia ni sawa.

**Com. Lethome:** Na mtu akiuawa, ungependa kuwe na malipo, gharama zilipwe?

**Jospesh Ngolo:** Zilipwe.

**Com. Lethome**: Kiasi gani?

**Jospesh Ngolo:** Laki nne.

**Com. Lethome**: Maoni yake, maoni yake. Wewe ukija upendekeze zaidi au kidogo hamuna shida.

**Jospesh Ngolo:** Kitu chingine ni habari ya mahindi ya msaada yanayotoka huko ng'ambo. Yakitoka huko, yanakuja hapa yasaidie kila mmoja. Lakini yakifika hapa inasemekana watapewa hawa maskini, hawa wengine wakose. Ningependekeza hivi, mahindi yakitoka kule yakifika hapa, kila mmoja apate yale mahindi hata kama ni tajiri, pia apate ndebe mbili.

**Com. Lethome:** Kwa hiyo hata Mheshimiwa wa Bunge kama yuko huko apewe?

**Jospesh Ngolo:** Apewe, maana ile ni msaada umetoka ng'ambo.

**Com. Lethome:** Msaada wa kusaidia nani?

**Jospesh Ngolo:** Wa kusaidia Wakenya.

**Com. Lethome:** Msaada huo unapkuja, huo msaada ni wa kusaidia nani?

**Jospesh Ngolo:** Wa kusaidia sisi wananchi.

**Com. Lethome:** Haya asante. Lingine?

**Jospesh Ngolo:** Lingine ni habari ya wizi. Kuna ule wizi wa ujambazi, wa kukushika kwa nguvu. Unacho, huna, mshipi nikutoe nikimbie. Sasa mtu kama yule akipatikana yule, ana haki kule kushikwa na kwenda kunyongwa huko. Maana yule ni jambazi. Wizi wingine ni ule wa kuangalia mtu ule, na huku ukimuona kidogo anahepa kidogo unaenda kwenye muhogo unag'oa. Ukishikwa hapo, upelekwe kortini. Nafikiri hapo ingekuwa ….

**Com. Lethome:** Haya asante sana. Karisa Wambalu yuko? Haya karibia. Katana Mwaringa Ngoa? Njoo huku. Halafu na Jackson ukae tayari. Jackson Sulubu ukae tayari. Jackson Sulubu uko? Endelea, anza na jina lako.

**Karisa Wambalu:** Majina yangu Karisa Wambalu. Maoin yangu nataka makaratasi ya mashamba tupate, na mambo ya maji ya mfereji iwe rahisi kidogo, na mambo ya barabara - -

**Com. Lethome**: Endelea usiningoje mimi

**Karisa Wambalu**: Haya, nakona mpaka umalize kuandikal

**Com. Lethome**: Hapa! Kuna chombo cha kunasa pale, hich ndicho muhimu.

**Karisa Wambalu**: Na mambo ya barabara nimetaja? Iangaliwe mambo ya barabara na ninataka atakaye tuongoza awe na maendelo mzuri. Awe tutakuwa naye sawa sawa kwa hiyo yangu nisha maliza.

**Com. Lethome**: Atakua President ama atakua nani?

**Karisa Wambalu**: Atakua Rais atakua President wote sawa!

**Com. Lethome**: Haya Katana? Katana Mwaringa? Haya, Jackon Sulubu kaa hapa karibu.

**Com. Lethome**: Endelea, anza na jina lako.

**Katana Maringa Ngoa**: Niendelee?. Kwa majina naitwa Katana Maringa Ngoa, ni mkaazi wa mlima wa ndege location. Pendekezo la kwanza ama serikali ile ambayo itashika uhatamu ujao, ninaomba ama maoni yangu ninaonelea kwamba ikapate kusaidia watoto. Yaani watoto wa shule wasaidiwe kuanzia class cha kwanza mpaka form four kabisa, maana kule form four ndio ambayo tunashindwa sisi. Naona wengine wana haya kusema hivyo lakini huko ndiko kushindako, huko ni ngumu. Kwa hiyo serikali ianzishe kuanzia mwanzo mpaka mwisho, isomeshe mtoto, halafu ikiwa mtoto ameajiriwa wakati huo, atakuja kulipa, atakatiwa mshahara alipez ile pesa zake za masomo. Hayo ni maoni yangu.

Pili, ninaomba, maoni yangu, ninatoa maoni upande wa afya. Yaani upande wa matibabu, upande wa matibabu hasa ndio upande nataka serikali inagalie sana, kama vile zamani tulikuwa tukienda hospitalini na kutibiwa bure. Serikali ile ijayo, tuende kuangaliwa bure tu, tukapate madawa bure. Na tatu, nne kwa jumla ni Rais. Rais, mimi maoni yangu naona atawale kipindi cha miaka ile kumi. Hayo ni maoni yangu.

Madiwani, diwani hata kama ni mama ambaye hajui kusoma kabisa, kama hajaona number kabisa lakini ni mama ambaye hana haya na kuzungumuza na kusema ule ukweli ambao unasikika, huyo achaguliwe na akiwa amependekezwa na amependwa na wananchi, huyo awe diwani kwa sababu hata kama una elimu lakini lakini u muoga, hutatusaidia. Kwa hivyo maoni yangu, mimi naomba hata kama hajui kusoma kabisa, huyo mama, lakini ni mama ambaye hana uoga, huyo awe diwani kama tumemupenda katika ile sehemu.

Serikali; Serikali ninaomba serikali ya umoja. Ninaomba serikali ya umoja. Usimake ni maoni yangu bwana! Sikupitisha mimi.

**Com. Lethome:** Nafasi yako ikija utasema.

**Katana Maringa Ngoa**: Utasema vile utakavyo. Mimi ninaomba serikali ya umoja, na sababu hii ni kwamba hata iwapo katika mji mumeachana, kila mmoja amepika sima yake, lakini mumetoa pahali pamoja. Saa nyingine wewe ukikosa unapata kwa yule mwenzio, unakula. Lakini kama kila mmoja anakula nyungu yake basi uje ile ujue yule jirani akikosa, unalala kabisa na

njaa. Kwa hivyo mimi nataka ule umoja, serikali ya umoja. Sababu yangu ni hiyo, na sababu nyingine, maoni yangu mengine, natoa maoni, mtu anapo-shukiwa kwamba labda ameiba lakini nikushukiwa, asiuwawe. Awe anafanyiwa uchunguzi pole pole lakini siyo kukanyagwa, kukanyagwa, kupigwa mateke hata ikija ikajulikana si yeye, ameuawa na hata si yeye. Hiyo pia nayo ilegezwe hiyo. Na kitu chingine ni, maoni yangu mengine ni barabara. Barabara hata kama hatutapata lami lakini tupate murram kutoka huko Kilifi mpaka Mlimwndege huko ndani kabisa kule ambako tunakaa. Murram iingie huko. Haya, na mambo mengine ni mambo haya ya mashamba. Karatasi hizi za mashamba. Karatasi za mashamba pia ziwe zinaweza patikana mapema kwa sababu kila mtu anajivunia kitu akiwa ana haki yake. Yaani ana kile kibali chake, pale pahali unajivunia kwa sababu una kibali. Lakini kama unaketi mahali na huna kibali unasema hapa ni kwa baba, ama ni kwa babu yangu na huna chochote kinacho onyesha kwamba hapo ni kwa babu yako, wakati wowote unaweza kuondolewa. Kwa hiyo, karatasi zile za mashamba ziwe zinaweza kupatikana.

Haya, nikiingia kwa ma chief. Kwa ma chiefu maoni yangu ninaomba askari warudishwe kwa ma chief, kwa sababu yule chief sasa amekuwa kama nyani na mama mzee. Mama mzee anapotembea namna hii, sasa nyani humuona kama yule ni mwenzake, kwa hivyo hata anavyosema haja, hakimbii. Hawakimbii wale, wale mayonda huwa hawakimbii. Kwa hivyo chifu anasisitiza ama nasisitiza, lakini kwa sababu hakuna ile imetolewa moshi kidogo ile, imekuwa hata sasa maharambee mengi hayafanikiwi, mambo mengi yanaharibika sana. Kwa hivyo maaskari wa rudi kwa ma chief. Haya. Mambo mengine hapo hapo kwa ma cief, machif wachaguliwe na wananchi kwa sababu hao machiefu nao saa nyingine basi akuwa afanyaje? Akufinya na hamuna nafasi naye. Kwa hivyo ikiwa sasa kama yule munaweza kumuchagua, wakati mwingine kama anamkanyagakanyaga, munaweza kumuondoa yule mukaweka mwingine. Kwa hivyo, kumalizia malizia, ni hapa mahali kwa hawa wanyama wapori. Hawa wanyama wa pori, kweli nao tunasikia kwamba wanatuletea pesa nyingi za kigeni. Katika Kenya huwa ndio ambao wanaleta pesa nyingi za kigeni. Sasa ikiwa wanaeleta pesa nyingi za kigeni, na wamekuja kukula mimea yangu, ama hata wamemuua baba yangu, na hata baba yangu yeye alikuwa akinisomesha, imekuwa sasa hata kulipwa pesa za kuwa mimi niendelee kusoma sasa siwezi, baba yangu ameuliwa na ndovu…..

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Katana Maringa Ngoa**: Na pendekeza kuwe na malipo makubwa ili kwamba - - (Interjecttion)….kama million moja hivi. Hapo nitakomea hapo, asanteni.

**Com. Lethome:** Haya, asante sana bwana Katana, haya tumupate Jackson Nduru. Afuatwe na Karema Mulewa. Karema Mulewa? Haya endelea Jackson. Aanza kwa majina.

**Jackson Subui Charo:** Kwa jina ni Jackson Subui Charo, mimi ni mkaaji wa Mlima ndege location, sub-location Tukiri. Mapendekezo yangu, mimi ninapendekeza kwanza serikali yetu iwe, inaweza kuchukua jukumu la raia kutoka sehemu za mbali mbali, kama sehemu za mashambani, wahakikishe wamepata pipe za mfereji, wapate maji ya kutosha.

Pili, mimi napendekeza upande wa mahospitalini, tupate madaktari wa kutosha, ziwe na madaktari wa kutosha. Tatu, tupate barabara nzuri.

**Com. Lethome:** Hizo hospitali zenyewe ziko? Ziko za kutosha.

**Jackson Subui Charo:** Serikali ihakikishe tumepata hospitali za kutosha, na madaktari wa kutosha.

**Com. Lethome:** Ziko karibu au ziko mbali?

**Jackson Subui Charo:** Ziwe karibu nasi. Tatu, barabara ziwe safi, tuwe tukitembelewa katika mashambani mwetu na ma-officer wa agriculture, wawe wakitutembelea mashambani. Vile vile tuwe tunapata machifu wetu wako na maaskari karibu.

**Com. Lethome:** Machifu wachaguliwe au wasichaguliwe?

**Jackson Subui Charo:** Chief wetu tuhakikishe tumemchaguwa wenyewe. Vile vile tuwe na uwezo wa kujenga viosk bila ku-change-iwa mpaka kama baada yamwaka moja hivi ndiyo watu wawe wa licenc wanatutembelea. Hapo nafikiri si haki.

**Com. Lethome:** Asante sana. Karema Mulewa Shauri Kazungu? Shauri Kazungu? Hayuko? Haya musikizeni Karema.

**Karema Mulewa:** Jambo la kwanza serikali nataka iwe ya majimbo. Tumelemewa na mzigo katika Pwani. Watoto wetu tunasukuma hivyo hivyo lakini sasa wakienda maofisini, hakuna nafasi.

**Com. Lethome:** Kuna mama wana mazungumuzo mengi sauti zinazosikika ni za kina mama huko nyuma. Kina mama tafadhalini kaeni kimya tusikize.

**Karema Mulewa:** Kwa hivyo watoto wetu sasa wamekuwa watu wa kuiba kwa sababu hawana - - hawapati kazi wakienda kule maofisini. Kwa hivyo serikali ikiwa ya majimbo, watoto wetu watapata kazi.

Barabara; Barabara zitengezwe vizuri. Kila mmoja ajue anachangia vipi kwa , barabara hizo za kwetu. Madiwani.; Madiwani napendekeza asichaguliwe mtu ambaye hajui kusoma kabisa! Sababu ni maziwa lala!

**Com. Lethome:** Awe na elimu kiwango gani?

**Karema Mulewa:** Hata class cha nane anaweza. Sababu anaelewa.

**Com. Lethome:** Sawa endelea.

**Karema Mulewa:** Anaenda kabisa huko Kilifi, basi haukumchagua huyu. Nimemchagua mimi tena hanitaki. Nikitaka kumuona, mpaka niende Kilifi. Tikiti ya kutoka hapa mpaka huko….

**Com. Lethome:** Unapendekeza nini sasa kuhusu huyu councillor wako?

**Karema Mulewa:** Huyo councillor kama amechaguliwa, miaka ile mitano kama anafanya vizuri achaguliwe tena. Kama hafanyi kazi, hata miaka miwili yenyewe akionekana yeye hafanyi kazi, apigiwe kura mtu mwingine tuchague wenyewe, sababu tumechoka sana sisi.

**Com. Lethome:** Haya endelea.

**Karema Mulewa:** Hospitali ziongezwe vyeo, tena magari ije ya kuchukua wagonjwa wakienda nao huko Kilifi.

**Com. Lethome:** ukisema vyeo unakusudia nini?

**Karema Mulewa:** Kuwe na hospitali kubwa na ndogo, akitoka hapa aende kule ….

**Com. Lethome:** Unaona ziko mbali hospitali ama ziko karibu?

**Karema Mulewa:** Ziko mbali mbali.

**Com. Lethome:** Watakaje sasa?

**Karema Mulewa:** Nataka kila pahali pawe na dispensary.

**Com. Lethome:** Na malipo ya matibabu unasema aje?

**Karema Mulewa:** Malipo, iwe hakuna malipo. Tunaumia sana tukienda, yule karani pale ni pesa, kule kwa daktari ni pesa, sasa kama wewe huna pesa utatibiwa kweli?

**Com. Lethome:** Hauwezi.

**Karema Mulewa:** Eh?

**Com. Lethome:** Huwezi.

**Karema Mulewa:** Serikali yetu sasa ni pesa. Askari.; Askari wanatoka huko basi wanakuja kwa DO. Ukifika kwa DO kwa sababu wewe kule umekosana na mtu anataka kukuua, ukifika hapa "Lete shilingi elfu mbili" - -

**Com. Lethome:** Pendekeza, pendekezo.

**Karema Mulewa:** Kwa hivyo wale, hawakuja hapa kumulinda DO, wamekuja kulinda raia. Kwa hivyo zile pesa wanazoitisha ziondolewe kabisa.

**Com. Lethome:** Hizi pesa hazijawekwa na sheria. Ni wao wenyewe wamejiwekea. Sasa unapendekeza nini? Ile inaitwa hongo, usiogope kusema.

**Karema Mulewa:** Eh, ni hongo ile sasa ndio iondolewe.

**Com. Lethome:** Haya tumchukulie hatua gani huyu mwenye kuitisha hongo?

**Karema Mulewa:** Yule akiitisha hongo, afutwe kabisa!

**Com. Lethome:** Endelea, endelea.

**Karema Mulewa:** Kuna kiwango cha hawa watoto wakisoma, wakifika kidato cha nane, hawawezi kupata kazi. Akienda huko polisi wanaandikwa huko, anambiwa huyu mpaka awe na form four ndio apate.

**Com. Lethome:** Unataka aje? Pendekeza.

**Karema Mulewa:** Na taka yule class wa cha nane apate ile kazi ya askari vile vile si atakuwa amepata?

**Com. Lethome:** Haya endelea , na hutaki watoto wengine wafike form four.

**Karema Mulewa:** Tunataka lakini hakuna …. hakuna pesa.

**Com. Lethome:** Pendekeza.

**Karema Mulewa:** Nataka zile pesa ziondolewe asome bure.

**Com. Lethome:** Elimu ya bure mpaka secondary. Endelea

**Karema Mulewa:** Machifu wachaguliwe. Ukienda kwa chifu yeye anataka pesa na yeye. Si ameandikwa anapata mshahara? Mtu kama yule haijui ile kazi, afutwe na yeye chief. Hayo ndio maoni yangu.

**Com. Lethome:** Asante sana kajiandikishe pale. Sasa tumpate huyu …. Shauri nimesikia hayuko. Shauri Kazungu. Tumupate Chengo Chai. Afuatwe na Nyanje Ziro. Nyanje Ziro yuko? Njoo hapa Nyanze Ziro.

**Chengo Chai Sheti:** Mimi pendekezo langu kwa serikali hii ambayo inakuja, iwe ya majimbo. Ingine, chiefs, assistant chiefs wachaguliwe na wananchi wenyewe kwa muda wa miaka mitano. Akifanya makosa hapa ambayo bado hayajamalizika hiyo, aondolewe tuchague mwingine.

Tatu, huku tupate simu. Vituo vya simu vienee upande huu nao. Lingine, kuanzia form one mpaka form four, napendekeza iwe bure. Lingine, wakina mama wasiogope kugombea uchaguzi. Nao pia wachaguliwe kama diwani, kama nani, wachaguliwe nao pia. Wasiachwe wanaume peke yao. Lingine, wazee wa vijiji, wapate angalau kidogo, kamshahara. Lingine, KANU office, sehemu za mashinani, wapate kadogo nao pia.

**Com. Lethome:** Nani hao?

**Chengo Chai:** KANU office.

**Com. Lethome:** KANU office, na DP?

**Chengo Chai:** No! No!, tunataka hiki chama chetu.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo KANU offices tu zipewe. Sasa unataka tuandike katika Katiba KANU offices wapewe . Na vyama vingine vya kisiasa?

**Chengo Chai:** Hau ni shauri yao, mimi nategemea hii yetu ya majimbo.

**Com. Lethome:** O.K.

**Chengo Chai:** Lingine, upande wa barabara. Kidogo tuna shida huku, sehemu hii ya Vitengeni division. Nafikiri ni hayo tu. Asante.

**Com. Lethome:** Wewe ni mzee wa kijiji sio? Haya, Nyanje Ziro. Naomi Koi uko karibu Naomi? Karibia hapa mama. Haya Nyanze endelea.

**Nyanze Ziro**: *(in Giriama Dialect)*

**Translator**: His name is Nyanje Ziro.

**Nyanze Ziro**: *(in Giriama Dialect)*

**Translator**: His views are that the councillor, chiefs and sub-chiefs be elected by the people.

**Nyanze Ziro**: *(in Giriama Dialect)*

**Translator**: That is all he has.

**Com. Lethome:** Haya Naomi. Selina Baya? Selina Baya? Haya.

**Naomi Koi:** Kwa majina naitwa Naomi Koi, natoka Mlima wa ndege.

**Com. Lethome**: Hebu ngojea. Tumuskize huyu mama, bwana. Jamani wazee huko, kimia.

**Naomi Koi**: Kwa majina naitwa Naomi Koi kutoka Mlima wa ndege. Mimi pendekezo langu ni kwamba Rais wetu aendelee kwa miaka kumi. Lingine ni mambo ya barabara. Huku Mlima wa ndege hakuna barabara kabisa. Sasa ningependelea serikali ichukuwe hatua tupate angalau barabara kuu. Jambo lingine la tatu ni kwamba, kule kuna mahospitali lakini madaktari hawatoshi. Ukienda kwa mahospitali unakuta madaktari ni wawili ama ni watatu. Sasa hata unaweza kukosa madawa kabisa.

Lingine la nne ni kuhusu maji. Mlima wa ndege hakuna maji kabisa. Maji masafi yaani ya mfereji hakuna. Tunakuta tukifika huku tunapata maji masafi ya mfereji, lakini kwetu hakuna maji kama haya. Sasa ningependelea serikali ifikirie jambo hilo la maji mazuri huko kwetu Mlima wa ndege. Ni hayo tu.

**Com. Lethome**: Haya, Selina Baya, na afuatwe na Sidi Konde

**Selina Baya:** Kwa jina naitwa Selina Baya. Langu mimi …..

**Com. Lethome**: Hebu tumusikilizeni mama Selina.

**Selina Baya:** Langu mimi ni machifu, ma-sub-chifu wawe watapigiwa makura. Lingine ni wazee wa vijiji. Wanafanya mambo ambayo kwamba mengine si ya haki ikiwa kazi ofisi yake, akaiingilia na si ya yake, si upande wake.

**Com. Lethome**: Kwa hivyo wazee wa vijiji wanaingilia kazi ambazo si zao?

**Selina Baya:** Si zao.

**Com. Lethome**: Haya.

**Selina Baya:** Na hao nao nataka wafikiriwe.

**Com. Lethome**: Ah, wafikiriwe nani sasa atawafikiria? Wewe tuambie, pendekeza.

**Selina Baya:** Wanaweza kutolewa wakatiwa wengine, kuwa wanafanya vibaya. Lingine ni rais wetu akuwe akiendelea kama miaka kumi. Yangu ni hayo.

**Com. Lethome**: Sidi Konde, haya. Halafu akae tayari Nyankula Suleiman. Endelea Sidi.

**Sidi Konde**: Kwa jina naitwa Sidi Konde.

**Com. Lethome**: Sauti mama, sauti.

**Sidi Konde**: Sidi Konde.

**Com. Lethome**: Haya Sidi Konde, tusikizeni, tusikizeni.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Com. Lethome:** Haya, endelea mama.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: Anaitwa Sidi Konde.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: Utawala wa Pwani anataka watawaliwe na KANU.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: Jambo lingine kuhusu barabara.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: Nataka ziwekwe murram.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: Another thing is about the children going to school.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: She wants them educated free from primary level to secondary level.

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: That is all she has to say.

**Com. Lethome:** Ngoja mama, swali moja tu. Unajua Kenya kuna vyama vingine isipokuwa KANU?

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: Hajui

**Com. Lethome:** Haya, sasa nakwambia sasa. Kuna vingine vingi. Kuna vingine vingi.

**Translator:** *(in Giriama Dialect).*

**Sidi Konde**: *(In Giriama Dialect)*

**Com.Lethome:** *(In Giriama Dialect)*. Haya, Nyankula Suleiman. Hayoko, Nyankula? Hayuko, haya tumpate Zablon Mumba. Zablom Mumba yuko? Haya karibia mzee. Na Kazungu Kiti Kanu amfuate.

**Zablon Mumba**: Kwa majina langu ni Zablom Mumba.

**Com. Lethome**: Haya, endelea.

**Zablon Mumba**: Nitaanza na serikali. Serikali hii tufanywe tuwachagua wale watu, tuwachague wenyewe.

**Com. Lethome**: Unajua ukisema serekali, kuna wale viongozi sasa unataka tuanze na yupi kuchagua?

**Zablon Mumba**: Tuanze na Rais.

**Com. Lethome**: Rais achaguliwe…..

**Zablon Mumba**: Ehe, miaka ishirini. Makamu wake miaka kumi. Wale wengine waliyobakia kama ma sub-chief - -

**Com. Lethome**: Ngojeni sikizeni munapitwa na mambo makubwa, sikizeni. Haya.

**Zablon Mumba**: Machifu, assistant chifu na ma-councilor kwa miaka mitano mitano, tuwachague. Akiwa anaendelea vizuri, tutamrudisha.

**Com. Lethome**: Na hapo katikati kabla ya miako tano kuisha, ukiwa unamuona ni maziwa lala?

**Zablon Mumba**: Akiwa ni maziwa lala tumutupe nje, tuchague mwingine.

**Com. Lenaola:** Na mjumbe tumpe miaka mingapi?

**Zablon Mumba**: Mjumbe?

**Com. Lenaola**: Miaka ngapi?

**Zablon Mumba**: Miaka kumi.

**Com. Lethome**: Na mtakuwa na haki yakumurudisha ikiwa miaka hii yake haijaisha lakini hafanyi kazi?

**Zablon Mumba**: Tutamchagua mwingine.

**Com. Lethome**: Haya endelea.

**Zablon Mumba**: Serikali yetu inatambua kwamba kuna mzee wa kijiji. Inatambua?

**Com. Lethome**: Ndiyo

**Zablon Mumba**: Sasa mzee wa kijiji hapati chochote.

**Com. Lethome**: Pendekeza.

**Zablon Mumba**: Apate mshahara.

**Com. Lethome**: Lakini si kuna pesa wanatoza watu hapa?

**Zablon Mumba**: Ile ni kama bahati nasibu.

**Com. Lethome**: Halafu huenda wapi hiyo bahati nasibu?

**Zablon Mumba**: Hugawanywa.

**Com. Lethome**: O.K. Sawa, sasa kama wakilipwa mshahara, na hiyo bahati nasibu iweko ama iondolewe?

**Zablon Mumba**: Iondolewe.

**Com. Lethome**: Sawa sawa. Haya. endelea.

**Zablon Mumba**: Upande wa hospitali, hospitali za kisasa hata wewe ukiwa mgonjwa unaweza kufa ukiwa huna pesa.

**Com. Lethome**: Pendekeza.

**Zablon Mumba**: Pesa zipunguzwe tupate dawa na sisi.

**Com. Lethome**: Endelea.

**Zablon Mumba**: Upande wa elimu, kutoka standard one hadi standard eight, hata kama nikulipa tulipe kama zamani.

**Com. Lethome**: Mulilipa aje zamani?

**Zablon Mumba**: Tulikuwa tukilipa pesa kidogo kidogo.

**Com. Lethome**: Kwa hivyo ifanywe aje?

**Zablon Mumba**: Ipunguzwe. Nafikiri hapo nimetosheka.

**Com. Lethome**: Haya asante. Wewe ni mzee wa kijiji?

**Zablon Mumba**: Mimi ni mzee wa kijiji.

**Com. Lethome**: Asante tupatie Kazungu kiti. Haya endelea Kazungu. Utazungumuza Kigiriama au kizungu? Utachanganya? Haya endelea.

**Kazungu Kiti Kanu:** Upande wangu….

**Translator:** Jina, jina kwanza.

**Kazungu Kiti Kanu:** Jina langu naitwa Kazungu Kiti Kanu.

**Com. Lethome:** Haya, endelea.

**Kazungu Kiti Kanu:** Upendo wangu, nataka barabara kutoka Jila, mpaka Bamba, itengezwe vizuri, na mpaka Mlima wa ndege, mpaka Murwachakwe, mpaka Ahera, kuwekwe barabara kuanzia hapo mpaka Kilifi.
La pili, ninataka Rais, nampa mimi miaka 20. Makamu wa Rais, kumi na mitano. Kuna PC, tumpatie miaka kumi.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo PC pia ni mutu wa kuchaguliwa?

**Kazungu Kiti Kanu:** Eh, lazima achaguliwe.

**Com. Lethome:** Miaka ngapi?

**Kazungu Kiti Kanu:** Kumi.

**Com. Lethome:** O.K.

**Kazungu Kiti Kanu:** DC pia naye miaka kumi.

**Com. Lethome:** Na D.O?

**Kazungu Kiti Kanu:** Tusema hapo miaka mitano.

**Com. Lethome:** Haya, twende kwa chief.

**Kazungu Kiti Kanu:** Chifu, kwa sababu ni wa huku, tutampatia miaka kumi.

**Com. Lethome:** Sub-chifu?

**Kazungu Kiti Kanu:** Sub-Chifu mitano.

**Com. Lethome:** Haya endelea.

**Kazungu Kiti Kanu:** Diwani, Diwani miaka mitano.

**Com. Lethome:** Na Mbunge wenyu?

**Kazungu Kiti Kanu:** Mbunge wetu, tumpatie miaka kumi na mitano.

**Com. Lethome:** Haya.

**Kazungu Kiti Kanu:** Na kuna hawa wazee wa vijiji hawa. Mara nyingine wanaenda kinyume kinyume, tunataka wapigiwe

kura.  Kura kabisa. Tuangalie vizuri, nawapa miaka mitatu.

**Com. Lethome:** O.K. Wazee wa kijiji walipwe au wasilipwe.

**Kazungu Kiti Kanu:** Walipwe!

**Com. Lethome:** Na wachukue hiyo bahati nasibu au wasichukue.

**Kazungu Kiti Kanu:** Hiyo, akiwa ni mzuri, aendelee.

**Com. Lethome:** Unajua kwa sasa, hawa kuitisha watu pesa. Kabla hawajasikiza kesi, wanasema pesa zilipwe kwao kwanza.

**Kazungu Kiti Kanu:** Hiyo waachane nayo. Akishikwa, awekwe ndani.

**Com. Lethome:** Haya sawa.

**Kazungu Kiti Kanu:** Lingine la ngapi?  Saba hiyo? Nafikiri imetosha.

**Com. Lethome:** Jiandikishe pale. Asante, sasa tuna Charo Vanga.  Charo Vanga yuko?  Hayuko.  Haya Ambrose Runya? Afuatwe na Kenga Konde

**Ambrose Runya :** Kwa jina ni Ambrose Runya. Langu la kwanza ni serikali ya majimbo. Pia kuwe na serikali kuu ambapo haya majimbo yatakuwa yakijisimamia na Rais atakuwa kwa serikali kuu. Pili, barabara zetu za Kilifi zote zikaweze kutengenezwa.

Tatu kuhusu elimu,  sisi wa mapato ya chini huwa tunashindwa kuwasomesha watoto wakati wakifikia kwa vidato. Inapofika kidato cha kwanza, serikali iwe itachukua watoto hawa na kuwalipia karo. Kuhusu hospitali, wakati mtu anaenda kutibiwa na kurudi, matibabu yakaweze kufanyiwa bure. Ikiwa ni wa kulala kitandani, awe akiitishwa lakini kiwango kidogo.

Kuhusu mashamba;  Umilikaji wa mashamba uwe utapatiwa haki haraka iwezekanavyo kuliko wakati huu ambapo mtu anakuja kuandikishwa shamba yake, na hata anaweze kufariki akiwa na miaka hata mia asiweza kupata hiyo haki yake.

Sita, ni kuhusu walemavu. Walemavu, kuna wengine hata serikali haijui kuwa kuna walemavu.  Hiyo, wawe watazunguka, kila mzee wa kijiji azunguke akajue ana mlemavu wa aina gani, akaweze kutujulisha jambo hilo.

Maji; Maji huwa hayana bei kamili. Mara maji yanakatwa kwa sababu ya bill isiyoeleweka. Meter inasomwa, inasema mia moja, unaambiwa elfu kumi. Hiyo, serikali iwe itaangalia sawa sawa. Kuhusu wazee wa vijiji, wawe watapata mshahara na pia uniform kwa sababu wengine watakuwa hawaelewi ni mzee wa kijiji lakini akienda na nguo yake ya kiraia, pengine anapata hata matusi.

Kuna askari magongo, pia hawa wawe na uniform.

**Com. Lethome:** Askari magongo ni wa aina gani?

**Ambrose Runya :** Hawa ni wasaidizi wa wazee wa mtaa.

**Com. Lethome:** Hao huwa wanachaguliwa na nani?

**Ambrose Runya :** Hao huwa wanachaguliwa na kamati ya chief.

**Com. Lethome:** Ungependekeza nini sasa?

**Ambrose Runya :** Ningependekeza siku za usoni, wawe pia hawa watakuwa na kima cha mshahara pamoja na uniform.

**Com. Lethome:** Na kuchaguliwa kwao je?

**Ambrose Runya :** Kuchaguliwa kwao? Kwa vile ni kamati ya chief, hiyo moja kwa moja ni serikali.
**Com. Lethome:** Lakini wachaguliwe na nani sasa?

**Ambrose Runya :** Iwe tunachagua sisi wenyewe raia

**Com. Lethome:** Na ukiona mwingine ambaye hafai kuwa katika hiyo kamati ya wazee?

**Ambrose Runya :** Mtu kama huyu, kama haonekani katika kambi yake kwa muda wa mwezi moja, uchaguzi uwekwe, tayari aondolewe. Mimi nishamaliza.

**Com. Lethome**: Asante sana, sasa tumupate Kenga Konde, ndiye huyo? Janet Fondo amufuate. Janet Karibia.

**Kenga Konde:** Kwa jina ni Kenga Konde. Pendekezo langu la kwanza ni watoto wakisoma … Pendekezo langu la kwanza, mtoto akisoma darasa la kwanza mpaka akifika darasa la nane, akitengeza mtihani akipita sawasawa, mzee akiwa ana nguvu ya

kumpeleka mbele, ampeleke. Kama hana serikali impeleke.

Hilo ni la kwanza. Pili, serikali iwe ya majimbo. Tatu, hospitali pesa tunazotozwa zimezidi. Ukienda na mgonjwa na huna pesa, atakufa. Kwa hivyo pesa zirudishwe chini iwe nawe kidogo kidogo hata kama una shilingi ishirini, iwe unaweza kwenda atibiwe mgonjwa wako.

Nne, ma chief, na ma sub-chief, na ma-councilor, wapigiwe kura. Hayo ni maoni yangu ambayo nataka yafanyike. Sina zaidi.

**Com. Lethome:** Asante sana. Janet?

**Janet Fondo:** Kwa majina naitwa Janet Fondo. Maoni yangu: La kwanza nitaanzia kwa watoto wa kike. Watoto wa kike wanakosa haki zao kwa sababu mtoto umemzaa, mama amezaa watoto wa kike na wa kiume. Halafu pale utakuta mtoto wa kike atanyimwa haki kwamba yeye hafai kwa sababu ataolewa, ataenda huko apate haki yake. Kwa hivyo hapa hana, hawezi kupata haki hapa kwao. Mimi naonelea kwamba mtoto wa kike hata akiwa ameolewa, huko kwao pia naye apewe haki yake. Kama ni urithi, apewe kwao.

Yangu ya pili ni kuhusu wamama walioolewa. Wamama sisi pia tumeolewa na mabwana zetu ni kwamba tumeonewa. Pengine kwa bahati mbaya bwana afe, halafu yeye atakuachia urithi pale. Lakini utakuta ndugu wa yule bwana atakuingilia kwamba wewe hufai kukaa ni hiyo mali, unatakikana uende kwenyu. Wao ndio watachukua hiyo mali. Na hiyo una haki kwamba mama ukae na hiyo mali, na wale watoto uwatunze. Kwa hivyo mimi napendekeza kwamba, ikiwa ni urithi kama huo umeachiwa na bwanako, mama yule anafaa kuchukua.

**Com. Lethome:** Na ufa?

**Janet Fondo:** Ufa hakuna. Mimi napendekeza hakuna. Uondolewe huo ufa, utachukuliwa vipi? La tatu, ma-councillor; Ma-councillor, upande wa ma-councillor, mimi ninapendekeza ya kwamba, councillor achaguliwe na wananchi wenyewe. Elimu ni nyingine, na uongozi ni mwingine. Unaweza kuwa wewe umesoma mpaka form six, lakini wewe ukawa hufai kabisa, unadidimiza wengine, na yeye hakusoma lakini ana uongozi mzuri. Yule atakayependekezwa na yule atakayepitishwa na wananchi wenyewe, mimi napendekeza kwamba achaguliwe yule yule. Na achaguliwe kwa miaka mitano. Na ikiwa yule ni mzuri, ikiisha ile miaka mitano, wananchi wenyewe wakiona ya kuwa yule ni mzuri, mimi napendekeza kwamba arudishwe yule yule kama wamemuona ni sawa. Akiwa si sawa, atolewe nje.

La nne, Rais achaguliwe na wananchi wenyewe wamtakaye Rais kwa miaka mitano. Na Rais akiwa anaendelea vizuri, huyu anafaa , ikiwa wenyewe wameona huyo ni sawa aendelee, mimi napendekeza kwamba kusiwe na kiwango cha kwamba Rais basi akifikia miaka kumi ama mitano, akitolewa ni basi na aende kabisa. Kwa sababu ni miaka yake, ati imepitishwa hivi. Mimi

naikataa. Napendekeza kwamba, ikifikia hiyo miaka mitano akiwa amefanya mazuri, wananchi wenyewe wanaweza kumpitisha.

**Com. Lethome:** Na elimu? Elimu ya Rais?

**Janet Fondo:** Elimu ya Rais? Awe na elimu lakini hiyo elimu nayo sitaipendekeza kuwa ni ya kiwango kiasi gani. Maanake nimechunguza mimi hiyo elimu, kuna wengine wanaelimu sana lakini huku nimewanona ametudidimiza sana na elimu zao. Kwa hivyo hapo mimi napakataa.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo awe na elimu asiwe na elimu …

**Janet Fondo:** Awe na elimu lakini.

**Com. Lethome:** Ni kiwango gani?

**Janet Fondo:** Elimu ambayo inatosha kuongoza.

**Com. Lethome:** Standard one?

**Janet Fondo:** Ah, Ah!

**Com. Lethome:** Stanard eight, form four? Tujibu mama? Awe standard eight?

**Janet Fondo:** Anaweza kufika form four hivi.

**Com. Lethome:** Na umri wake? Ni umri gani?

**Janet Fondo:** Ah, mimi hapo kwa umri, siwezi kusema ni umri gani. Haijalishi kwamba hata kama ni mzee lakini anaongoza vizuri, atuongoze.

**Com. Lethome:** Haya tuanze na chief sasa. Awe kijana wa miaka kumi na minane?

**Janet Fondo:** Ah, Ah, kijana wa miaka kumi na minane atatupoteza njia.

**Com. Lethome:** Haya miaka ishirini na tano?

**Janet Fondo:** Bado ni kijana.

**Com. Lethome:** Arobanne?

**Janet Fondo:** Arobanne kwenda mbele.

**Com. Lethome:** Haya, mpaka wapi?

**Janet Fondo:** Ah, huko ni aende kabisa.

**Com. Lethome:** Hata miaka 100?

**Janet Fondo:** (laughing) Hayo ni maoni yangu lakini. Haya la tano, afya. La tano ni afya. Afya naona kwamba, ni heri serikali iangalie sana upande wa afya kwa sababu wakati huu umefikia sasa, hata naona kwamba watu wengi watakufa sana na magonjwa, kwa sababu bila pesa huwezi kutibiwa, na madaktari nao waangaliwe. Wale ambao hawafanyi kazi vizuri watolewe! Maoni yangu. Watolewe. Wengine wanachukua madawa na kufungua mahospitali yao ya kibinafsi, wanapeleka huko na kuuzia wengine. Mimi maoni yangu nasema akipatikana, sema daktari huyo atolewe, afutwe kazi.

**Com. Lethome:** Kwa hivyo madaktari katika mahospitali za kiserikali wasifungue mahospitali zao binafsi.

**Janet Fondo:** Kama wanafungua na pesa zao ni sawa. Lakini sasa kuna uchunguzi kwamba wengine wanachukua yale madawa kama yameletwa mahospitalini. Yeye anafanya kazi, anachukua … wale wakubwa wanachukua yale madawa na kufungua mahospitali yao ya kibinafsi wanauzia wengine madawa, na wengine huku tunaumia, tunakufa na magonjwa. Mtu kama huyo akipatikana, afutwe. Maoni yangu hayo.

**Com. Lethome:** Dakika moja sasa imebaki.

**Janet Fondo:** Ah! Ah! Hoja! Wewe unasema tutoe maoni tena unatuambia hivi? Elimu, elimu sasa. Elimu nayo iangaliwe. Upande wa walimu, nataka kusema juu ya walimu sasa. Walimu nao hawafundishi vizuri mashuleni. Watoto wetu tumegundua kwamba wanaanguka kwa sababu ya walimu. Walimu wengine ni wavivu, hawarauki mashuleni, wanalala mpaka saa nne mchana ndio wanaenda shule, anakuta watoto wanacheza. Maoni yangu ni kwamba, mwalimu akipatikana vile amechelewa, atolewe kazini! Maanake tunaambiwa kwamba watoto wetu hawasomi, kumbe ni walimu wanafanya hivyo?

**Com. Lethome**: Sikizeni, sikizeni mama anamaliza sasa.

**Janet Fondo**: La saba. Langu la saba, la saba ni wachawi. Uchawi uko, hatuwezi kusema uchawi hauko. Uko kweli uchawi, lakini utasikia serikali inasema kwamba hakuna uchawi. Na wachawi wako, hata ukijenga nyumba yako ya mabati, tayari warogwa huko! Kwa hivyo mimi mapendekezo yangu nasema wachawi, kwa mfano nataka kuwe na uwezo wa kwamba, si huwa kuna zile ngoma za kienyeji, nasikia kuna zile ngoma za kienyeji za kushika wale wachawi. Hizo nazo nasikia kwamba zinakatazwa, lakini mwishowe ikiwa umepatikana, maoni yangu ni mchawi akafungwe jela akapewa adhabu, na akitoka hapo atoe hizo ndonga zake na asirudie tena.

**Com. Lethome**: Ndonga ni nini mama?

**Janet Fondo**: La nane, la nane. La nane nazungumuza kuhusu makundi ya kina mama. Ni wamama vile vile. Makundi ya kina mama, mimi napendekeza kwamba, wanapewa vyeo vikubwa, kwa district unaambiwa huyo ni chairlady, division huyo ni chairlady, lakini halipwi chochote. Kwa hivyo mimi mapendekezo yangu ni kwamba, watu kama wale hata ikiwa ni mahali kama baraza au nini, kama ni mawaziri wamekuja, huyo mama anatakikana ajulikane lakini halipwi hata kitu kidogo. Tena yeye ndiye anatakikana azunguke kama ni divison yote aende, kama ni district atembee kwa division yote. Mimi napendekeza kwamba, mama kama huyo apewe mshahara ili naye ajisikie vizuri.

**Com. Lethome**: Apewe mshahara na nani?

**Janet Fondo**: Apewe na serikali. Serikali itoe mshahara kwa mama kama huyo. Na kiongozi yeyote ambaye anakubali hongo, mimi naona kwamba huyo hafai kabisa. Akipatikana kiongozi kama huyo, mimi kwa maoni yangu nasema, heri afutwe kazi. Kama ni chiefu kama ni nani, akipatikana afutwe. Na machief na ma sub-chief, maoni yangu ni kwamba nataka wapigiwe kura na wananchi wenyewe, maanake wanatuumiza, hata tumeumia sana. Ni hayo tu.

**Com. Lethome**: Mama unaongoza chama gani?

**Janet Fondo**: Makundi ya akina mama!

**Patrick Pondo**: Kwa majina naitwa Patrick Pondo

**Com. Lethome**: Charo Nzoa ndiye atayemfuata. Patrick endelea.

**PatrickPondo**: Kwanza ningependa kuchangia mjadala huu. Point ya kwanza ninaongea juu ya serikali yetu. Ninapendekeza serikali ya majimbo. Katika serikali hii, kuwe na governor ambaye atatoka katika mkoa wa Pwani na katika kila mkoa, atoke governor tena kutakuwa na kiongozi ambaye atakuwa ni Rais wa Kenya yote. Katika hii jimbo, zile rasilimali zote ambazo ziko

katika lile jimbo, zihifadhiwe na watu wenyewe ambao wanakaa katika lile jimbo. Kama ni kazi, asilimia themanini ya kazi zile ziwe zikipatiwa wale watu ambao wanakaa katika jimbo lile na ikiwa ni mapato, yaani revenue, ushuru unaotozwa katika jimbo lile, basi asilimia themanini zibaki katika lile jimbo, na asilimia ishirini ziende katika serikali kuu.

Point ya pili naongea kuhusu elimu. Hapa kwetu Mkoani Pwani tunahitaji university angalau moja. Maanake tumeona ule ugumu wa watoto wanapita na wanaenda juu. Ile tikiti ya kutoka hapa mpaka Nairobi ni ghali kwa mzazi na mapato yetu ni madogo. Kwa hivyo tunahitaji chuo kikuu katika mkoa wa Pwani ili tuendeleze vijana wetu.

Point ya tatu nitaongea kuhusu usawa wa jinsia. Watoto wa kiume na watoto wa kike wawe sawa, si kusomesha mtoto wa kiume peke yake kwa sababu unasema huyu ni mtoto wa kiume, ataniokoa. Yule mtoto wa kike pia ni mtoto wako. Kwa hivyo ukizaa mtoto wa kike ama mtoto wa kiume, wote uwaelimishe maanake elimu saa hii ni rasilimali yetu.

Ninaongea point ya nne. Kuhusu mawasiliano huku kwetu, tunahitaji tupate angalau telephone booth moja ama hata mbili na zienda huko ndani. Utapata pengine kumetokea mkasa, inabidii mtu akimbie, akaangalie mwenye gari, kama mtaani kuna mtu mwenye gari atoke hapa mpaka Kilifi akaripoti hiyo. Kama tungepata angalau simu, ingekuwa nafuu kwetu.

Point ya tano. Nitaongea kuhusu maji. Katika mkoa wa Pwani, kuna sehemu ambazo ziko katika hali za ukame, kama huko ndani, Mlima wa ndege, Marafa huko ndani. Tungependelea kama serikali ingeangalia na kuwapatia mifereji hawa watu ili wakapata maji mazuri kwa afya bora. Maanake tunapata magonjwa mengi yanatokana na maji, wanakunywa maji ambayo hawastahili kunywa lakini kwa vile wanakunywa na hawana lolote la kufanya, inabidii wanashikwa na magonjwa., Kwa hivyo ningeomba serikali I-supply maji katika ile mitaa ambayo iko dry.

Point nyingine ni kuhusu mahakama, judiciary. Hapa tungependelea kwamba ikiwa mtu ameshikwa, baada ya masaa ishirini na manne, aweze kupelekwa mahakamani na kuhukumiwa. Isiwe ile mtu ameshikwa anawekwa karibu miaka miwili ama mitatu ama hata zaidi anateswa kule na hata akitoka pengine hana hatia yeyote. Kwa hivyo ningependela mtu akishikwa, baada ya masaa ishirini na manne, apelekwe mahakamani ili aweze kuhukumiwa.

Kama niliyosema, vijana, kuna point ya sita nafikiri kuhusu vijana. Vijana wapatiwe majukumu ya uongozi. Unapata wale viongozi wengi wamejitolea ni wazee ambao sasa hawapati nafasi kwa vijana kuongoza na nihidhirisho ya kweli kwamba serikali ya sasa ama ile naomba ni kwamba vijana pia nao wapatiwe jukumu la kuongoza serikali yetu wakati huu. Kwa maana tumeona wengine ni wazee ambao sasa hata akili zao hazilingani na yale mazingira ya sasa. Kama sisi ambao ni watoto wa 8-4-4, tumeamkia katika muamuko mpya ambao tunaangalia serikali yetu vile iko, tunaona wazee wanachaguana wazee kwa wazee, lakini kama vijana watapatiwa jukumu la kuongoza, itakuwa ni bora.

Point ya saba; Environment. Kuna hizi misitu. Ningeomba kama itawezekana serikali yetu itunze sana hizi misitu kwa maana

tumeona misitu ni chombo muhimu ambacho kinavutia mvua katika ardhi yetu. Tunapata wale watu wengine wanakata misitu katika chemichemi za maji, yaani kule kwenye miti wanakata miti ambapo wanaleta jangwa. Na kwetu kuna sehemu nyingine kama Shangweni huko ndani haipati mvua kwa sababu ya kukata miti ilikuchoma makaa. Kwa hivyo kama ingewezekana, serikali ninaomba watunze rasilimali, zile. misitu, na ile miti mikubwa mikubwa haiwezi kutunzwa ili tupate mvua kwa wingi.

Kitu kingine ni kwamba kuna ile mitambo ambayo saa hii imesimama, mitambo ya Korosho, mitambo ya Ramisi sugar. Hizi mitambo ningependelea ziregeshwe kwa maana sasa tunaona Wapwani tulikuwa tukitegemea zile mitambo kama mitambo ya Korosho Kilifi lakini saa hii, mtambo toka uharibike mpaka saa hii, watu wengi wa kulima wamekuwa wakipata matatizo mengi kuuza mazao yao. Kwa hiyo ningeomba kama serikali ingewezesha kuendeleza hizo vituo vya hiyo mitambo. (interejction) Sawa.

Nyingine ni michezo. Michezo tumeona watu wengi ambao wamechaguliwa katika kucheza, na mchezo saa hii ni rasilimali kwa kijana kwa sababu ukiwa ni mchezaji, unapata pato jingi katika maisha yako. Lakini tutapata wale wanaochaguliwa katika michezo ni wale ambao wanafanya kazi katika makampuni makubwa makubwa. Ningependelea kama itawezekana, hawa wachaguzi wa hawa wachezaji, wawe wakiingia katika mashinani kwote huku, kuangalia wale vijana wenye vipawa, kuendeleza kile kipawa chao cha michezo, ili nao wajipatie mapato zaidi. Asanteni.

**Com. Lethome**: Ngao Charo Hayuko? Haya tukiendelea tumupate Joseph Charo? Afuatwe na Mwanyure Mbaya. Mwanyure Mbaya yuko?

**Joseph Charo**: Mimi kwa jina naitwa Joseph Charo. Napendekeza kwamba serikali inayokuja iwe ni serikali ya majimbo. Na hiyo serikali mpya inayokuja iangalie maofisi makubwa makubwa ambayo saa zote yanasumbua watu kusafiri kutoka hapa mpaka Nairobi, kila siku. Kila ofisi ambayo inahusika na matembezi namna hiyo, kama ya mashamba na kadhalika, ziwekwe katika mikoa yao, ili kupunguza gharama za wananchi kusafiri mara kwa mara kwenda kwa ofisi kubwa Nairobi.

Na habari za ma chief. Nilikuwa napendekeza kwamba, chief na sub-chief, wawe watachaguliwa na wananchi. Lakini basi wawe na umri wa kutosha wa kufahamu mambo yanavyoendelea. Pendekezo langu ni kama umri wa kutoka miaka arobanne hivi na kuendelea mpaka hamsini na tano ama sitini ama sabini. Maana hao wanajua sheria, au wanajua kuongea na watu. Lakini ma chief hawa wa sasa watakwenda watakuta mzee ana maneno, ama ana habari fulani, hajui namna ya kuifafanua ile habari. Anasikiza tu, halafu anamsikiza huyu "wewe sema, je unakubali hii?" "Je unakubali hii?" "Wewe sema, wewe unakubali hii?" Hawezi kujua hiyo. Lakini kama ni mzee, anajua huyu akisema, anajua huyu ndiye mwenye mkosa kwa sababu ya hii, na hii na hii, hiyo tu ndio napendekeza. Wazee, hata kama ame-retire, amefanya kazi ame-retire na yuko nyumbani, huyo anastahili kuchaguliwa kuwa chief ama sub-chief kwa maana anaelewa namna ya uzuri ni upi na ubaya ni upi.

Na upande wa afya, serikali inayokuja ione kwamba kila mtaa kuna hospitali karibu na wananchi. Maana safari za kutoka hapa

mpaka Kilifi ni ndefu na mgonjwa amezidiwa, akifika kule anakutana na mtu mwingine ametoka upande mwingine, na upande mwingine. Sasa hiyo inatatiza sana, inasumbua wananchi. Katika kila mtaa kuwe na hospitali kubwa ya kuwasaidia hao, yaani kila mahali.

Upande wa barabara, zitengenezwe na zitiwe lami. Nasema hivyo kwa sababu wananchi wanasumbuka kusafirisha mazao yao. Hata kuna kwingine kuna mazao mazuri lakini hayawezi kwenda mahali popote. Wanazurura zurura tu, halafu inaharibika hapo. Maziwa yanaharibika hapo hapo, wanavuna mazao hapo, yanakaa, vyakula vinakaa hapo hapo, haviendi mbele. Lakini kama kungekuwa na barabara ambayo imetengenezwa kabisa, itakuwa ni vizuri kwa watu kusafirisha mazao yao na kupata manufaa. Pesa zao wanatumia na umasikini unakuja tu kwa sababu ya hii kuwa hakuna kitu, hakuna barabara.

Elimu; Ningependa au ningependekeza serikali inayokuja iangalie sana upande wa elimu wa watoto wa aina zote, wake na waume. Kama ni elimu ya bure ijulikane ni ya bure.

**Com. Lethome**: Toa pendekezo wewe

**Joseph Charo**: Napendekeza elimu ya bure kutokea nursery mpaka Standard eight. Pia, kwa upande wa elimu, kila mkoa uwe na chuo kikuu kwa sababu watoto wengi wanasoma. Haswa hapa nawaona wanasoma, lakini wakifika form four na wanabidii kabisa wanaambiwa, "Utakwenda chuo kikuu Ruiru". Sasa Ruiru, kutoka Ruiru mpaka hapa ni mbali, pesa ya kusafiri kwenda na kurudi, mzee anashindwa. Unaona watoto wale wanakaa chini na tunapoteza watu wazuri sana. Kwa hivyo chuo kikuu, kifanywe kila jimbo, kuwe na chuo kikuu. (interjection). Basi nitawacha hapa.

**Com. Lethome**: Asante Mwanyure. Jonathan Kulola? Jonathan? Haya uko karibu wewe Nyanje Mwavuo? Haya karibu.

**Mwanyure Mbaya**: Haya, mimi jina langu naitwa Mwanyure Mbaya. Maoni yangu ni kulingana na serikali yetu. Serikali yetu inatunyanyasa sana. Sasa kwa wakati huu, wakati wa kutoa maoni vile unavyotaka, mimi maoni yangu, napendekeza serikali za mikoa na majimbo. Ninapendekeza mikoa yetu minane, kila jimbo liwe na governor wake. Tuwe na Rais mmoja, tuwe na rais moja, tuwe na Waziri Mkuu moja. Napendekeza serikali zikiwa za majimbo, za mikoa, kila mkoa utakuwa hauna taabu. Ikiwa ni misaada kutoka nchi za nje, msaada ule unalenga mkoa ule ule, kulingana na vile wakati huu, msaada ukija waja Kenya nzima, hatupa misaada yeyote kama mikoa mingine, kama mkoa wetu. Na kulingana na mkoa wetu huu, ni mkoa ambao kwamba tuna utajiri mkubwa kushinda Kenya nzima. Lakini sisi wenye mkoa huu, tumekaliwa na wenzetu ambao wanatufinya sisi, wamefanya hapa pahali petu ni colony yao, wanachukua mali zetu na kupeleka kwao halafu wanarudi hapa wanatufanya sisi ni maskini. Kwa hivyo ninapendekeza serikali ya majimbo ndio ambayo itakomboa, kila mmoja apate haki yake. Mimi sina zaidi, yangu ni hayo tu.

**Com. Lethome**: Asante, Yupate Jonathan Kulola.

**Jonathan Kulola**: Kwa majina naitwa Jonathan Maburuki Kulola, ni mzaliwa wa hapa Vitengeni location. Haya, mapendekezo yangu nitaanza na wazee wa kijiji. Wazee wa kijiji wawe wakichaguliwa kutoka katika kila sehemu za hapa kwetu nchini. Tena kuwe na mzee wa kijiji mmoja ambaye yeye atakuwa ni wa ki-location. Atakuwa ni mkubwa katika wale wazee wenzake wote. Huyu katika mahali pale, location ile, atakuwa akisaidiana na chifu kama askari wake, kama mtu wake wa karibu zaidi. Kisha kila chifu, awe akichaguliwa kwa vipindi viwili, vya miaka mitano na akifanya vizuri, kipindi kingine awe anaweza kupewa kura, akiwa hafanyi vizuri aondolewe. Sub-chief namna hiyo hiyo. Lakini huyu sub-chief, katika kila location awe ni sub-chief moja maanake nimefanya uchunguzi nikaona kwamba ma-sub-chief hawana kazi tena, wazee wa kijiji wanaweza kuchukuwa sehemu hiyo na wakalipwa mshahara kidogo wakaendelea. Kwa hivyo ma-sub-chief awe ni mmoja kila location na chief mmoja wakisaidiana na wale wengine wawe wanaweza kuachishwa kazi mara moja.

Madiwani, maoni yangu, madiwani wawe wakichaguliwa, vipindi vyao viwe ni viwili. Pia vile sawa sawa na wale machief, na ma sub-chief, wawe wanachaguliwa kwa vipindi viwili, kipindi cha kwanza cha miaka mitano na mingine mitano akiwa anafanya vizuri. Asipofanya vizuri awe anaweza kutolewa nje kwenye kipindi kingine. Tena hawa wote ambao nimewataja wasiwe na viwango vya umri mkubwa sana, wawe kama miaka ishirini na mitano hadi hamsini, wawe wanaweza kuchaguliwa hapo katikati ili wale vijana nao wawe wanaweza kupata kazi hapo ndani. Maanake sasa kazi zimepungua sana hapa kwetu nchini. Kwa hivyo ikiwa namna hiyo itakuwa wewe ukifaidika miaka kumi, mwingine naye anachukua ushukani miaka kumi, anafaidika, tunaendelea namna hiyo.

Rais awe mmoja katika nchi yetu kama vile alivyo sasa lakini serikali iwe ni ya majimbo. Kwa hivyo kuanzia Rais awe ni mmoja kama ishara ya utaifa halafu baadaye kutachaguliwa kama ma-governor wengine na wegine kuendelea. Lakini Rais achaguliwe na wananchi wenyewe. Kuhusu ma-governor inaweza kuwa hiyo ni serikali na inaweza kufanyika kama vile inavyoendelea.

Nikienda katika sehemu ile ya huyu Rais, mamlaka yake ningelipendelea awe na mamlaka makubwa kama vile alivyo nayo sasa. Kwa sababu huo ndio usalama wa nchi. Akiwa yeye hana mamlaka inawezekana kuwa kunaweza kuwa na maafa hapa na pale kama sehemu nyingine kwenye watu wanatatizika.

Tukienda katika sehemu ya ardhi, hii ardhi mimi mapendekezo yangu ningalipenda iwe yule anayepatiwa kibali cha kumiliki ardhi awe ni Mkenya ambaye amezaliwa na Wakenya wote wawili. Wazazi wote wawili wawe ni Wakenya. Na ikiwa mzazi moja sio Mkenya, hana haki awe anaweza kupatiwa kibali cha kumiliki shamba mahali hapa Kenya. Iwe vivyo hivyo. Vile ninavyopendelea, na ikiwa pengine atakuwa ni mtu katika jimbo lingine, kama vile ilivyokuwa nimependekeza majimbo, basi akiwa ni kutoka jimbo lingine awe ana uhuru tu wa kumiliki shamba la acre kumi lakini si zaidi ya hapo. Na wale wengine wote watapokuwa wanaweza kuishi, wawe wakiishi wakitoa ada kidogo kidogo. Mtu yeyote ambaye ametoka nje ya nchi hii, awe yeye analipa ushuru wakati wowote akiishi hapa mpaka akiondoka, majumba yake yote na mahoteli anaachia Wakenya wenyewe.

Langu la tisa hapa ni kuhusu elimu.  Hii elimu ningependekeza iwe ya bure kuanzia darasa la kwanza hadi la nane. Halafu kuanzia form one mpaka form four huko iwe wanalipa pesa. Na kama ni college iwe bure, hata ikiwezekana walipwe marupurupu kidogo huko.

Biashara ziwe zikitolewa license kama vile inavyoendelea sasa, wawe kuna ushuru wanatoa, wale wafanyaji biashara. Lakini iwe ni wa kiwango  fulani kama ni mashambani kuwe kuna license ya malipo kidogo, na kama ni mjini, kama ni Kilifi iwe ni kidogo. Kama ni jiji kama Mombasa, iwe imepanda kulingana na ile hali vile ilivyo maanake biashara haiko sawa.

Mapato ya jimbo yawe yakishughulikia mahitaji ya jimbo lenyewe na kama nikupeana, kiwango fulani kwa serikali kuu, iwe ni kama 30% ama asilimia thelathini peke yake, na zile sabini ziwe zinabaki kwa jimbo lenyewe likijiendelesha na mipango yako. Halafu katika kila makao ya District, kuwe kuna barabara nzuri kama ya lami, ili kwamba kuwa kuna mawasiliano mazuri.

Lingine ambalo ni langu la kumi na tatu, bibi awe ni mmoja ikiwezekana katika ile serikali inayokuja. Si zaidi ya hapo, maanake wakati mwingi watu huwa na vita namna hiyo.  Kwa hivyo,  bibi awe ni mmoja katika nyumba.

Kumi na nne, langu la kumi na nne, tusisahau mila zetu kwamba sisi ni Wafrika na Wafrika ni lazima wawe na tofautiano. Ikiwa ni mke na mume, ni lazima tuko tofauti. Kwa hivyo tusisahau kwamba sisi Wafrika hata maadili zetu ama kibibilia, tutofautiane. Kuwe kuna mavazi tofauti tofauti.  Tusiwe yule akivaa suruali na wewe unavaa suruali, hiyo isiweko katika serikali ile inayokuja.

Kingine ambacho ninacho ni kuhusu seminars za wakulima wetu.  Hawa wakulima wetu ambao tunao kama wale wakulima wa minazi wameshindwa na kujinufaisha sana kwa sababu hawajapata zile seminars za kuwafanya wajue mnazi unafaida gani. Kwa hivyo wafanyiwe ma-seminars pande ule ule, waachwe watumie ile minazi yao kwa mapato mengine kama nazi na nini na nini. Lakini  mpaka waelimishwe mwanzo, ili wajue kwamba huo mnazi sio mapato peke yake ya mnazi. Kwa hivyo wanaweza kubadilisha wakafanya mambo mengine wakajinufaisha.

Kingine ambacho nataka kumalizia, report yangu ya kumi na sita hiyo, katika mahali hapa ni kuhusu zile sehemu zingine ambazo ziko katika nchi hii ambazo pengine haziwezi kutumika sana kwa kilimo ama zina upungufu fulani, hapo pengine hakuna watu. Maanake ni maeneo makubwa makubwa na hakuna watu kama sehemu hizi za huku kwetu. Kuna maeneo mengine ambayo hayana watu ama watu wana sehemu kubwa hawawezi kuzilima. Sehemu zile serikali itoe mbegu ambazo zinaweza kupandwa katika sehemu zile, kuna msitu pia vile vile sijui ni afforestation ili kwamba kuwe na hali nyingine ambayo ni nzuri kama yule msitu ambao tunao hapa. Yangu ni hayo, asanteni.

**Com. Lethome**:  Umesema kuwa lazima tuheshimu mila za wafrika. Sasa ukiangalia katika mila zetu, utakuta kuwa mila

inakubali mtu awe na zaidi ya mke mmoja. Sawa hivyo? Hapa unasema sheria ipitishe kuwa mtu awe na mke mmoja tu peke yake, huoni hapo tukivunja mila? Kuna watu wengine sio watu wote ambao ni wakristo, kuna watu wengine ambao ni Waislamu, dini yao inakubali iwe ana wake wanne kama anaweza kuwatosheleza. Huoni kuwa umevunjia Muislamu pia haki yake ya kuabudu?

**Jonathan Kulola**: Ikiwa nitakuwa mmoja nimemukosea, atatoa maoni yake vile anavyopenda yeye, maanake nimetoa mapendekezo.

**Com. Lethome**: Nyanje Mwavuo?

**Nyanje Mwavuo**: Kwa jina naitwa Nyanje Mwavuo.

**Com. Lethome**: Tusikize Nyanje Mwavuo.

**Nyanje Mwavuo**: Kwa jina naitwa Nyanje Mwavuo. Maoni yangu, maoni yangu ninasema hivi, serikali ijao iwe ya majimbo. La kwanza hilo. La pili, ninasikitika na vijana wengi sana hapa kwetu ambao sasa wamefika wakati wa kuchukua vitambulisho na hawana. Hilo jambo linatendeka sana. Wanaenda kwa sub-chief, wanaandikiwa karatasi, wanaenda kwa DO, wakifika kwa DO wanaambiwa "Nenda Kilifi ukapimwe meno kama una miaka kumi na minane" Na huu ni wakati wa kura, vijana wanahitaji wapige kura. Sasa hao hawana vitambulisho na hawatapata.

**Com. Lethome**: Haya pendekeza jambo

**Nyanje Mwavuo**: Ninapendekeza sub-chief akiandika barua akifika kwa DO, DO achukue jukumu la kufanya hiyo kazi. Kama ni daktari wa kupima meno, aje hapa hapa. La pili, ni habari ya shule. Shule tunaona watoto wengi sana wakifika darasa la nane, wakimaliza ni basi, mbele hawaendi. Sababu ya karo ziko juu, na wazazi hawana shughuli, yaani pato la hapa ni kidogo. Kwa hivyo kwa mapendekezo yangu, ninataka kama inawezekana, ikianza hapa mwanzo, tuende mpaka mwisho. Tukienda darasa la kwanza, tuende mpaka form four. Ifanye kuchukua mtoto, yaani wasome bure mpaka form four.

La pili ni barabara. Barabara yetu hii ni ya kitambo, ni miaka na miaka na miaka na miaka. Mpaka sasa tumefikia hapa. Mambo ni yale yale ya kawaida. Gari ikiondoka hapa ikifika pale, ni kuenda kwa miguu mpaka Kilifi. Kesho utasikia itatengezwa, itatengezwa. Mvua ikinyesha hakuna kitu. Kwa hivyo tunataka hii njia kama inawezekana kwa serikali ijao, kama sasa haitatengenezwa lakini serikali ijao, mwanzo ianze barabara. Itiwe lami kuanzia Kilifi mpaka huko, Mlima wa ndege huko. Na sisi tuwe huru kama wenzetu ambao wako huru. Sababu sasa tuko huru lakini tuko huru kwa mdomo lakini hatuko huru kwa kimwili. Kimwili tunateseka.

Sasa lingine ni kuhusu askari ambao wameletwa hapa wa Do. Wamekuja wafanye kazi ile nzuri ambayo inatakikana. Leo hii imekuwa sasa mtu ametoka huko, ameenda kuleta mkambaa wa kukata msitu, amenunua vifuko vya unga viwili, ashikilia panga, atakuja shikwa njiani. Sasa hiyo panga umeshikwa unaambiwa umeshikwa barabarani, na huu unga huoni? Hakuna! Kwa DO sitaenda, nikifika njiani natoa shilingi hamsini ninampa, ninapita. Hiyo ninapendekeza kama inawezekana, askari kama yule akipatikana afutwe kazi kabisa saa hiyo.

Ingine ni hivi, kuna wakina mama wana biashara ndogo ndogo. Biashara zile, hata akitoka asubuhi jioni ni shilingi ishirini tu alipopata. Zile shilingi ishirini anunua kibiriti na mafuta ya maji, mtoto wake aende aka study. Zile zile hii, city council itaingia pale, ikate shilingi kumi karatasi. Sasa hii shilingi ishirini akitoa shilingi kumi, zinabaki ngapi? Shilingi kumi. Zitamfanyia nini? Kwa hivyo hii mambo ninataka kama inawezekana, kwa maoni yangu, iachwe kabisa, hata kama ni biashara gani afanye mpaka akapate kile atapata akajisaidia. Ni hayo tu, Mungu awabariki.

**Com. Lethome**: Asante. Tupate Florence Yaa Ngari

**Florence Yaa Ngari**: Mimi kwa majina yangu naitwa Florence Yaa Ngari. Maoni yangu ambayo nimekuja nayo hivi leo, ni kwamba katika mpango huu wa Katiba ya Kenya, Rais wa Kenya, kwa maoni yangu nataka awe mtu mwenye uwezo mwingi wa kutosha.

Pili, achaguliwe kwa miaka kumi, ili kwamba ikiwa pengine atakuwa anaenda vizuri imalizike miaka kumi, lakini ikiwa haendi vizuri, afutwe aondolewe kitini, awe atachaguliwa mwingine kabla ya ile miaka kufika.

Jingine ni kwamba wanawake, katika serikali yetu hiyo ya zamani ama ambayo bado tunaimalizia malizia, wanawake huwa wakinyanyaswa lakini kwa wakati huu naomba kwa maoni yangu unyanyasaji wa wanawake uondolewe ili wapatiwe haki zao kama wanaume vile wanavyopatiwa. Kama ni elimu, kama ni uwezo wowote, yaani wanawake wawe nao wakijulikana.

Jingine ni kwamba mwanaume yeyote, sio ati kijana ama baba, akimpa mimba mtoto wa shule, achukuliwe hatua kali ya kutosha; kufungwa miaka mingi kabisa ili kwamba wasiwe wakichezea watoto wa watu, wasichana ambao wazazi wao wanataka kusomesha watoto wao. Kwa hivyo wafungwe miaka hata kama ni zaidi ya kumi, ndio iwe ni fundisho hata wengine huku wasiwe wakichezea wasichana wenzao. Si kusema ati mtoto mvulana peke yake. Hata akiwa ni huyo mwalimu wake, ama akiwa ni mwanafunzi mwenzake, hatua ichukuliwe hivyo hivyo. Na hawa ma chief, maoni yangu yanasema hivi; Wasichaguliwe ati kwa mlolongo maana itakuwa pengine tumerudi nyuma sana. Lakini hata hivyo, hizo kazi zao wawekewe miaka fulani ili kwamba akiwa ni mtu wa kudhulumu wananchi, awe anaweza kuondolewa hata kabla ya hiyo miaka maanake sasa dhuluma ndizo ambazo zimetukalia sana ndio tumeingiwa na ule uchungu. Ingawaje chief ni mzaliwa wa hapa, lakini utaona wengine ni shangazi zake, na wengine wale ambao si shangazi zake huwa wanaumia, na wale wa ukoo wanapata faida kidogo. Kwa hivyo waweze kuwekewa miaka ili kwamba akiwa hataendelea na zile sheria za kazi, awe anaweza kuondolewa mamlakani.

**Com. Lenaola**: Umri wake uwe vipi?

**Florence Yaa Naari**: Mimi pendekezo langu ni kwamba kuanzia miaka thelathini na mitano aandikwe miaka kumi. Ikiwa hafai, yeye pia hata kabla ya kufika hiyo miaka kumi, afutwe. Na jingine ni kwamba katika serikali hii yetu, napendelea chama hicho cha umoja na ushirikiano. Hicho ndicho napendekeza mimi, kwa maoni yangu. Na jingine ni kwamba, ninataka elimu iwe ya lazima. Na nikitaka kuongezea hapo ni kwamba, ikiwa ni lazima wengi watasoma na pesa, zile za kulipishwa zirudishwe chini. Hata ikiwa si bure kabisa lakini zitarudi chini, maanake hivi kuna wengi ambao hawasomi, watoto wao hawasomi kabisa. Na sasa hapa ni kama ambaye wewe unayesomesha pia, na wewe huna moyo maanake wezi wako hapo kando kando kwa sababu ile ya lazima iliondolewa. Kwa hivyo nataka hiyo elimu ya lazima irudishwe kabisa ili kwamba kila mmoja awe atasoma. Pesa zitarudi chini zenyewe jinsi watoto wakiwa wengi, vile nafikiria maoni yangu. Kwa hivyo ikiwa ya lazima wale wezi wengi watapungua.

Kumalizia ni kwamba ukabila pia uondolewe. Tuwe tutashirikiana na hata kimila kile ambacho hakifai pia kiondolewe, tuchague kila kimila kinachofaa. Wabunge waendelee kuchaguliwa vile vile miaka mitano, na wananchi wa Kenya pia wawe watakuwa na vitambulisho vya Kenya. Yale ni maoni yangu ambayo yamenileta hapa kwa siku ya leo.

**Com. Lenaola**: Asante Sarah Kadenge, yuko? Oh, basi keti hapo utafuata yeye.

**Sylvester Junga**: Jina langu naitwa Sylvester Junga, na nina maoni kwa tume hii ya urekebishaji ya Katiba. Oni langu la kwanza ni kwamba kwa sasa tumeketi kutoka asubuhi tukisema kwamba tunarekebisha, lakini kwa maoni yangu ni kwamba hata hawa watu ambao wanarekebisha Katiba, hiyo Katiba hawaijui. Kwa hivyo pendekezo langu ni kwamba, Katiba hii mpya ambayo tunaiunda iwe na kipengele cha kwamba, watu katika mashinani waelimishwe juu ya Katiba ni nini katika mikutano ili waelewe Katiba. Ili ikija wakati wa kubadilisha Katiba, wawe wanajua Katiba ni nini, ili tubadilishe tukiwa tunajua tunafanya nini.

Ya pili ni kuhusu upande wa elimu. Mfumo wetu wa elimu ambao tuko nao sasa wa 8-4-4- ni mfumo ambao ulizaliwa kwa ghafla sana, hakukuwa na muda wowote wa kuuchunguza mfumo huu. Na ilikuwa ni kama ambao ni pendekezo la Rais wetu anayetawala kwa sasa. Kwamba kuwe na mfumo huo na bila kuchunguza vizuri, tukau-adapt ule mfumo ambao kwa kweli tumeona (mimi nikiwa muelimishaji moja wapo) tumeona mfumo huu si mzuri. Pendekezo langu ni kwamba. Katiba hii ambayo tunatazamia kuiunda sasa, iwe inapeana uwezo kwa wananchi kujadili na kukubaliana juu ya mfumo wa elimu ambao utakuweko kwa ajili ya watoto wetu.

Tatu ni kwamba, (kuhusu mambo ya elimu vile vile), ni kwamba sisi watu wa hapa Pwani nikisema tumeonewa, nafikiri nitakuwa nimetumia neno la sawa. Tumeonewa na wale wenye mamlaka zaidi katika serikali ya kwamba kila wakati

wanapopendekeza kwamba kuwe na chuo kikuu, kinapendekezwa kiwe bara. Na katika mkoa wetu, tunakosa elimu na sehemu za kufundishia watoto wetu. Utakuta unataka kumupeleka mtoto wako university, lazima aende bara, kila kitu lazima aende bara. Kwani ni nini kizuri kiko bara ambacho Pwani hakiwezi kupatikana? Kwa hivyo napendekeza kwamba, kwa vile tunavyo vyuo mbali mbali kama vile cha Bandari, cha Shanzu Teachers College, Mombasa Polytechnic, na Kilifi Institute of Agriculture, tunapendekeza kwamba, ikiwa itawezekana na haitakuwa labda rahisi kuanzisha chuo kikuu kamili, hivi vyuo ambavyo viko, baadhi zao zibadilishwe. Kuwe na sheria ya kwamba katika mkoa huu, baadhi ya vyuo vile, vibadilishwe kuwa constituency colleges za universities, ili watoto wetu nao, pamoja na sisi wenyewe, tuweze kujielimisha tukiwa hapa karibu. Mfano mzuri ni kwamba, juzi juzi tu nilipokuwa katika chuo kimoja kule juu, tuliona kwamba watu wengi kule wanasoma jioni jioni, masomo ya university, na wengi wanapata degrees. Lakini tunaona kwetu haiwezekani, mpaka mtu aende bara. Kwa hivyo napendekeza kwamba iwe sheria kwamba, iwe sheria kwamba katika kila mkoa, kuwe na angalau chuo kikuu kimoja na constituency colleges za vyuo kadha wa kadha katika sehemu yetu.

Nne napendekeza kwamba serikali ambayo tutaishika sasa ama ambayo tutaichagua, iwe serikali ya majimbo ikiwa kila jimbo liwe na governor, kuwe na Rais, kuwe na Prime Minister ambaye ataendesha serikali.

Kuhusu kiwango cha elimu cha viongozi wetu, (nataka nianze na huku chini), ya kwamba tunaelimisha watoto wetu ili watusaidie. Kwa hivyo tukisema tuchague viongozi ambao hawana elimu, tutakuwa tunatukana ile hali ya kwamba ni lazima tuelimishe watoto wetu. Kwa hivyo napendekeza kwamba, wale ambao watawania viti mbali mbali kuanzia udiwani, labda angalau wawe wamesoma kufikia kiwango cha elimu, kile cha elimu ile cha zamani cha darasa la saba au kile kipya cha darasa la nane na kuendelea. Lakini wale ambao watataka ubunge, angalau mbunge awe na cheti cha chuo kikuu ili aweze kutuongoza vizuri. Elimu tunajua ni mwangaza na ni njia. Kwa hivyo akiwa na cheo kile, itakuwa ni vizuri zaidi.

Kwa Rais, tunapendekeza kwamba, kama Rais ambaye tuko naye elimu yake iko chini sana. Na inawezekana kwamba hali ambayo tuko nayo sasa ya economy kwenda chini, haiwezi kuendelea sana, labda contribution moja, na ninasema labda ni kwa sababu hiyo. Kwa hivyo ningependekeza kwamba ikiwa yule Rais tutakae mchagua sasa, atakuwa Rais aliyesoma vizuri, kufikia chuo kikuu, na hata ikiwezekana kama tunaweza kupata ambaye amepata Masters Degree katika Economics, huyu ataweza kutuongoza vizuri. Lakini kama hatuwezi pata wa Masters, angalau awe amehitimu katika shahada ya chuo kikuu.

Kingine ni kuhusu vyama vya kuwakilisha wafanyi kazi. Tunaona kwamba nchi yetu, ama serikali yetu ambayo tuko nayo na hii inaletwa na sheria ambayo tuko nayo sasa, inahitilafu. Kwamba kuna uwezo wa Registrar of Trade Unions kukataa ku-register chama cha kuwakilisha wafanyi kazi, labda ni kwa sababu ya kibinafsi kwa upande wa serikali ambayo labda tuko nayo kwa wakati ule. Lakini pendekezo langu ni kwamba ikiwa kutakuwa na kikundi cha wafanyi kazi ambao wangependelea kuunda chama chao ili kutetea haki zao za kikazi, chama kile, iwe ni sheria na imeratibiwa katika Katiba yetu mpya kwamba, kila chama ambacho kitaonekana ni chama ambacho kina good will, kiwe registered mara moja. (Interjection).

O.K. Ni sawa. Kuhusu afya, ningependekeza kwamba serikali iwe inaangalia raia wake kiafya vizuri. Na pendekezo langu ni kwamba katika kila sub-location, kuwe na institute moja ya kiafya, angalau dispensary katika kila sub-location na katika kila division, angalau kuwe kuna health centre ili watu wawe na ukaribu na vituo vya afya.

Halafu somo la kidini. Ningependekeza kwamba, either dini ya Kiislamu au ya Kikristo iwe ni lazima katika masomo ya wanafunzi wetu katika kila kiwango cha elimu. Hata kama mtu atafanya Bachelor of Science, lakini somo moja ambalo ni afanye liwe ni la kidini, tutakuwa tuna-boost ile hali ya morals katika jamii yetu. Halafu kuhusu sheria, ni kwamba Rais ambaye tuko naye sasa, sheria inampa uwezo wa kuwa juu ya sheria hiyo. Hata leo kama ataamua kufanya kitu chochote, hatuna haki kulingana na Katiba tuliyo nayo kumshtaki. Lakini mimi napendekeza kwamba, Katiba ipeane uwezo ya kwamba ikiwa Rais ataonekana amefanya kitendo ambacho ni cha ukiukaji wa haki za binadamu, ashtakiwe katika court, ili aeleze na akiwa proved guilty, labda achukuliwe hatua zaidi.

Nikimaliza na point tatu hivi, kwanza ni kwamba pension inasumbua wazee wetu sana. Mzazi wangu alichukuwa karibu miaka mitatu kupata pension yake, anasafiri kwenda Nairobi akirudi. Lakini ningependekeza kwamba, kuwe na decentralization ya hii pension department, ili katika wilaya kuwe kuna ofisi ambayo inashughulikia mambo ya pension, isiwe ni lazima mtu asafiri kwenda bara, Nairobi, ili kutafuta pension yake, kukodesha nyumba, kula chakula, magari inakuwa ni ghali na hatimae anatumia ile pension yake huko.

Halafu kuhusu mimea yetu ningependekeza kwamba, kama vile kunavyo Tea Board of Kenya, kuna Coffee Marketing Board, ningependekeza kwamba mimea yetu pia, kama vile ilivyo mimea ya wenzetu kule bara, pia iratibiwe na iwe kuna Act of Parliament ambayo inaruhusu establishment ya Board ya Mikorosho na Mikanju, Minazi na kila mmea ambao ni wa faida katika sehemu yetu.

Harambee zinapora wananchi sana. Kwa sababu mtu ataalikwa kuwa mgeni wa heshima mahali, atakusanya pesa nyingi huko, lakini ataleta pesa kidogo katika ule mchango. Mimi ningependekeza kwamba iwe ni sheria katika Katiba yetu mpya kwamba ikiwa harambee zitafanywa, kuwe na ufuatilizaji mzuri wa pesa zile ili wale ambao wanaonekana kwamba wanaenda kinyume, wanatumia pesa zile kimakosa, waweze kushtakiwa. (interjection.)

Mwisho, ni kwamba tuna vyama vingi vya kisiasa. Wengine wamependekeza kwamba chama cha KANU kiwe pale lakini mimi ninapendekeza ya kwamba, chama chochote cha kisiasa kilichojiandikisha na kikakubaliwa na Registrar of Societies, kiwe kitapewa pesa za kuendesha kazi zake na serikali kama vile chama kinachotawala. Kwa hivyo kusiwe na ubaguzi wa chama hiki kinatawala, kile hakitawali. Kila chama kipewe haki yake ili viendeshe kazi zake sawa sawa. Hatujui serikali inayokuja itaundwa na chama gani, kwa hivyo tusiwe tunabagua aina ya chama. Halafu mwisho, serikali daganyifu ichukuliwe hatua na ikiwezekana, ilazimishwe kujiuzulu na hiyo iwe katika Katiba yetu. Kwa mfano, serikali yetu imewadanganya walimu, na ni dhahiri , imeendelea kuwadanganya na kuwadanganya mpaka sasa hatujui watoto wetu watakavyokuwa baada ya siku ishirini

na nane zijazo. Kwa hivyo ikiwa serikali itakuwa imeji-commit katika jambo fulani, mimi ningependekeza kwamba Katiba yetu ichukulie maanani kwamba, serikali ifuatilie ile commitment yake, na i-meet zile obligations zake. Na ikiwa itaendelea kudanganya na ikadhibitishwa, basi kuwe na kipengele katika sheria yetu ambacho kitawalazimisha wakuu wa serikali waondolewe mamlakani, wajiuzulu. Asante.

**Com. Lenaola:** Haya sasa Sarah Kadenge? Safari Mwambire? Safari Mwambire? Darma Ufa.

Darma Ufa? Konde? Utafuata huyu

**Sarah Kadenge**: Kwa majina yangu naitwa Sarah Kadenge kutoka Mwahera. Pendekezo langu linasema hivi….

**Com. Lethome**: Sikizeni, sikizeni mama.

**Sarah Kadenge***:* *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Ana-speak for wanawake wanaonyanyaswa.

**Sarah Kadenge***:* *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Wananyanyaswa vile mwanamke ameolewa halafu she gives birth to a daughter, when wanapatiana ule urithi, kwa vile haukuzaa a son in that place, hauwezi kupata ule urithi. So wanagandamizwa because of that.

**Sarah Kadenge***:* *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Kwa hivyo angependekeza sasa hata kama ni mtoto wa kike, kila mtu apate ule urithi wake.

**Sarah Kadenge***:* *(In Giriama dialect)*

**Translator**: Anapendekeza chama kiwe ni hicho kimoja cha KANU ndicho kinatawala. They haven't seen anything bad about it so the other parties are just there to bring trouble. So they just want one main party to continue, i.e. KANU.

**Sarah Kadenge***:* *(In Giriama dialect)*

**Translator**: They want the President, the one who is there to continue.

**Com. Lethome**: Uchaguzi unaokuja, ni lazima aondoke.

**Sarah Kadenge***: (In Giriama dialect)*

**Translator**: O.K. When another one is elected, the other one will take over but as of now, she is comfortable with the one who is there, if he is re-elected he can go back.

**Sarah Kadenge***: (In Giriama dialect)*

**Translator**: Sub-chief, madiwani na ma-chief wachaguliwe through mlolongo.

**Sarah Kadenge***: (In Giriama dialect)*

**Translator**: And if he is not performing, atolewe and they choose another one.

**Sarah Kadenge***: (In Giriama dialect)*

**Translator**: Wazee wa kijiji pia waangaliwe because KANU employ them but there is nothing they are giving them. So at least that office that elects them should be able to cater for their needs, they should get something also.

**Sarah Kadenge***: (In Giriama dialect)*

**Com. Lenaola:** Asante sana mama. Haya, Tuva Konde?

**Safari Mwambire**: Kwa jina ninaitwa Safari Mwambire. Ningependekeza serikali ile ambayo itafuata, hongo zisikubaliwe. Mfanyaji kazi yeyote wa serikali akipatikana na honyo, afutwe kazi.

Lingine, mawasiliano. Tumekuwa tukisumbuliwa sana huku na ma-shifta, na habari kule kuwa walinda salama huwa hawafiki haraka iwezekanavyo. Kwa hivyo ningependekeza kuwe na simu. Lingine ni hizi harambee. Iwe kukitangazwa mikutano, kusiwe na wale wazee wa vijiji watutembelee katika vijiji vyetu ati tunataka harambee, harambee hatutaki.

Lingine ningetaka mila na utamaduni wetu uweko. Pia ningetaka serikali itakayokuja iendelee kuhudumisha hii hukumu ya kifo, isiondolewe kwa sababu ujambazi na wizi utazidi . Vile vile, madiwani, ma-sub chief na ma-chief wawe wakichaguliwa na wananchi wenyewe.

Kuhusu mashamba, ningependekeza, kuhusu mashamba ningependekeza uandikishaji wa mashamba uwe bure. Lingine ni wachawi. Ningependekeza wachawi wachukuliwe hatua kali. Wafungwe, sababu wanatusumbua sana. Wanatuonea wivu, hawataki tuendelee. Ukijenga nyumba ya bati anakuua, anakuroga. Ningependekeza kuwe na sheria ya kuhusu wachawi. Ikipatikana ameroga mtu, afungwe. Ni hayo.

**Com. Lenaola**: Asante sana. Tuva Konde? Ngoja kidogo Kausa Luai? Karibia.

**Tuva Konde**: Mimi, mapendekezo yangu ….

**Com. Lethome**: Anza kwa majina.

**Tuva Konde**: Jina ni Tuva Konde. Napenda majimbo. Na majimbo, naona watoto wa kwetu hawana kazi kabisa. Wakifika Kilindini, watu wa bara ndio wanapata. Hapa mkoa wa Pwani ni kidogo sana. Kilindini, Bamburi… ukifika pale ni watu wa juu. Nataka kama ni majimbo basi tupate watoto wa kwetu hapa, maanake tunasomesha lakini hawana kazi. Na ningependa mtoto kama amefika kama class cha nane, mujaribu kutusaidia kule mbele maanake wengine wazee hatuwezi. Kwa sababu watu wamezeeka na kule kwenda mbele wanapenda lakini hatuwezi na tunasomesha wanawake na wanaume. Wote, wanawake hawana kazi, waume hawana kazi. Pengine nimeshindwa class cha nane au cha sita, wanakwenda kuzurura tu huku huku halafu wakija wanaambiwa wana Ukimwi kwa nini? Kwa sababu yeye hana kazi. Kwa hivyo hiyo kitu tunataka kama ni majimbo itawale lakini tukifika mlangoni kama pale, watoto wetu wapate kazi kwa sababu kazi zimefimbwa fimbwa zinapatikana huko juu. Hilo ndilo langu tu.

**Com. Lenaola**: Haya, sasa huyu ndiye Karisa Luai?

**Karisa Luai**: Jina langu ni Karisa Luai, yangu ni mawili tu. Ni kuhusu elimu. Kuhusu elimu, ningetaka au pendekezo langu ni kutoka class cha nursery mpaka cha nane, iwe ni bure tu. La pili ni kuhusu mashamba yetu. Zile karatasi zisichelewe muda mrefu sana. Zitoke hivi hivi karibuni. Asante sana.

**Com. Lenaola**: Asante sana Bwana Karisa. Katana Menza? Halafu Emmanuel Iha? Utafuata huyu. Kennedy Mwang' ombe?

**Katana Menza**: Katana Menza. Langu mimi la kwanza ni kuhusu elimu. Elimu, napendekeza kuanzia mwanzo mpaka darasa ile ya kufanya KCPE ile ya nane, serikali ichukulie jukumu pale, maanake hapo ndipo panahangaisha watu sana.

**Com. Lenaola**: Tafadhali tunyamaze

**Katana Menza**: Jambo la tatu ni kuhusu mashamba. Mashamba yetu tupimiwe. Tunapopimiwa tupate zile karatasi zetu mapema. Na ile ya tatu ni kuhusu wao ma chief. Machief tunapenda twende tukichagua baada ya miaka mitano. Ma-sub chief pia miaka hiyo mitano. Wazee wa vijiji, mwaka mmoja, asije akakaa miaka mingi. Tena, mwisho ni, kuhusu mahospitali, serikali iangalie na iyapanue. Tupanuliwe hospitali kila pembe. Tunapata matatizo kwa sababu ukienda ni mgonjwa, kwanza pesa ndiyo inatakikana sana. Akikufa, ndio kabisa; Inatakikana apelekwe nyumbani, gari inapatikana kwa pesa, ikiwa ni karibu unaweza ukachukua ukapeleka nyumbani. Sina mengi sana.

**Com. Lenaola**: Asante sana bwana Menza, jiandikishe pale. Sasa ni wakati wa Emmanuel Iha.

**Emmanuel Iha Ndelela**: Kwa majina ni Emmanuel Iha Ndelela. Napenda kuchangia katika hali ya kurekebisha Katiba ya nchi yetu. Napendekeza hivi; Katika serikali ambayo tunaitarajia, iwe elimu ya msingi ni ya bure, ni ya lazima. Na kwa kuwa mambo hayawezi kuwa bure hivyo, serikali itaangalia itatumia mbinu gani kuhakikisha kwamba itapata ushuru fulani kupitia kwa wananchi ili tuweze kuendesha mradi huu wa elimu, bila mwananchi kuona kwamba labda kila siku anafukuziwa mtoto wake ama analazimishwa kulipa. Lakini atumie mbinu zake, ionekane kwamba ni ya bure, kama vile ambavyo wazee wetu wanatuambia kwamba ilikuwa ni ya bure hapo mwanzo na walikuwa wakitoa pesa kwa njia fulani lakini hakikuwa ya direct.

Elimu ya uraia na Katiba ifunzwe shuleni na hata kwenye mabaraza. Kwa sababu hata wakati huu tunaambiwa turekebishe Katiba, wengi hatujui Katiba ni nini, na ni kama tumeghaflishwa. Kwa hivyo iwe ikiendelezwa, isingojee mpaka labda wakati wa campaign, wakati wa kupiga kura ndio serikali iingilie kati kufundisha watu kwa speedy speedy, lakini vitu ziwe zikifanywa kama sehema ya maisha yetu.

**Com. Lenaola**: Endelea.

**Emmanuel Iha Ndelela**: Serikali yenyewe ambayo ninapendekeza, iwe serikali ya majimbo. Na kila jimbo litakuwa na uwezo wake wa kujiendeleza lakini kutakuwa na Rais mmoja ambaye atakuwa amechaguliwa kutoka kwa majimbo hayo yote. Rais huyu awe amesoma vya kutosha, angalau awe amefika kiwango cha chuo kikuu, ambapo anaweza kushindana na ulimwengu wa kisasa vile ulivyo. Kwa sababu kama akienda kwa mikutano nchi za nje, wataongea vitu hawezi kuvielewa, atakuwa ni mtu wa kuchekelea, na hushuku labda ameongea mambo ya maana. Lakini awe ambaye amefuzu angalau chuo kikuu.

Upande wa ma-chief na manaibu wao, kwa kuwa hali ya ufisadi umezidi sana katika nchi yetu, basi hawa wakiweko watu wa kudumu, tutaongeza shida. Lakini wachaguliwe na wahudumu kwa vipindi vitatu vya miaka mitano mitano. Mtu atakuwa amejitayarisha kwamba anajua kama ameshinda kipindi hiki, kingine anaweza kuanguka. Kwa hivyo atakuwa na hali ya kujiandaa, kuliko mtu awe anachukuliwa kama ameandikwa kazi maisha, halafu anafanya kosa anafutwa ghafla, anakuwa frustrated na anaongeza uhalifu. Lakini mtu akijua kwamba, o.k. kuna muda atatoka baada ya miaka fulani michache,

anajiandaa, anakuwa yuko tayari kwa maisha ya baadaye.

Rais achaguliwe na ahudumu kwa vipindi vitatu vya miaka mitano mitano. Mamlaka ya Rais yapunguzwe. Tukisema yapunguzwe hatusemi kuwa Rais yuko sasa lakini Rais yeyote. Tuna-mean Rais yeyote kwa sababu mamlaka yameongezea ufisadi. Tunaposema corruption, tunafikiria labda ni kupokea hongo peke yake, lakini sasa tumeona kwamba Rais ana mamlaka mengi, nasikia kwamba anaweza kuchagua mtu ambaye hastahili mahali. Na kama amechaguliwa mahali ambapo hastahili, basi ufisadi unaendelea kwa sababu akijua kwamba Rais labda hana elimu ya kutosha, na yule mtu amepewa wizara ambayo si yake, anaweza kufanya dhambi zozote zile za kuwa uchumi haukuji, anajua kwa vyovyote atasaidiwa na Rais. Kwa hivyo mamlaka ya Rais yapunguzwe. Kwa mfano wakati huu, yeye ni Chancellor wa vyuo vikuu vyote. Kwa hivyo kama ni migomo, labda chuo kikuu cha Nairobi kimegoma, mahali fulani pia wanakosea hivyo hivyo inakuwa ni migomo all through. Lakini kama atakuwa mamlaka haya mengine si yake, hizi shida zitapunguwa.

Mawaziri na wenye viti wa mashirika mbali mbali na makampuni wateuliwe kulingana na kiwango cha elimu na ujuzi ambao wameupata. Itakuwa ni aibu kumchukuwa labda Mkuu wa Majeshi, kumuweka Mkuu wa Afya ama wizara ya afya, labda lakusomea mambo ya afya, na umemchukuwa umemuweka mahali pale, unatarajia mtu ambaye amejua kushika bunduki aende kumbembeleza mgonjwa? Inakuwa ni shida, huu pia ni corruption. Kwa hivyo mtu achaguliwe mahali ambapo amepasomea vizuri na labda pia ameonekana ana good records.

**Com. Lenaola**: Una dakika moja.

**Emmanuel Iha Ndelela**: O.K. rasilimali za majimboni, zipewe umuhimu na heshima. Kwa mfano, kama ni pombe, tuchukulie pombe ni pombe. Mradi ipimwe ihakikishwe kwamba haina maafa kwa mwanadamu, ikubaliwe. Kama ni Kenya breweries itoe pombe ili tunywe, tunywe. Kama ni mnazi pia nao, upimwe uhakikishwe kwamba huo hauna madhara kama ile 'kumi kumi' , na uhalaishwe. Na ipewe pia nafasi ya kuuzwa nje ili kuzidishia ama ku-boost uchumi.

Viwanda ambavyo vimesambaratika hasa katika sehemu ya Pwani, viwanda ambavyo vimesambaratika, viweze kuregeshwe ili kufufua hali ya uchumi, vijana wengi wapate kazi. Hata kina mama walikuwa wakifanya kazi vikoroshoni kitambo, ilikuwa uchumi si mbaya hivyo. Kwa hivyo sasa vile viwanda ambavyo vimesambaratika viweze kurekebishwe na kuhakikisha kwamba vinarudi ili kufufua uchumi.

Matibabu yafanywe kuwa bure, lakini serikali ione kwamba inafanya mpango fulani kupitia kodi fulani ambazo imekuwa ikifanya kitambo kulingana na historia ili watu waonekane kwamba wanaendelea kutibiwa vizuri bila kutoa pesa.

Lugha ya kutumika hasa bungeni, taifa letu linasema ni la Kiswahili, lakini lugha ambayo inatumika mara nyingi ni Kizungu. Mambo muhimu kama vile budget inapokuwa inasomwa, watu wanasikiza kwa hamu wajue, lakini hata walio katika darasa la

nane, wakati wengine hawaelewi. Kwa hivyo lugha ya kiswahili itumike. Kama mumesoma Kiswahili vizuri, nyinyi ambao mutakuwa mumechaguliwa Bunge, mutumie Kiswahili vizuri tuweze kuwasiliana. Kama utakuwa unaongea Kizungu peke yake, tutakuwa tunaji-enjoy kwa sababu mutasikia kwamba, wenyewe wanasikiza na wenyewe ambao wanasikiza hawaelewi.

Kila mfanyakazi akatiwe kodi fulani kusaidia uchumi wa nchi hii.

**Com. Lenaola**: La mwisho?

**Emmanuel Iha Ndelela**: Asanteni.

**Com. Lenaola**: Haya asante sana. Tupate Kennedy Mwang'ombe.

**Kennedy Mwang,ombe**: Asante. Mimi jina langu naitwa Kennedy Mwang'ombe, nami nashukuru pia kupata fursa hii ya kutoa maoni katika urekebishaji huu wa Katiba. Kwanza nitaanza na Katiba yenyewe. Katiba ni chombo ambacho hatukijui, kwa hivyo napendekeza kwamba hii Katiba ielimishwe ili sote tuijue. Sasa hivi tukiuliza mwananchi pale Katiba ni nini, hutapata jibu sahihi. Kwa hivyo tunarekebisha kitu ambacho tukijui, na ninaomba somo la Katiba ikiwezekana liwekwe hata mashule, ili watoto wetu wafundishwe Katiba.

Pia hivyo, Katiba naomba kiwe ni chombo ambacho kinaweza kupatikana hata kwa mwananchi yule wa kawaida. Sasa hivi mimi sijaona Katiba hii ambayo tunaisema ni mbaya. Siijui, hata sijaiona. Sijui iko rangi gani hiyo, Katiba ya Kenya. Mimi siijui. Sasa hii Katiba ambayo tunaiunda, ninaomba kiwe ni chombo ambacho kitafikia yule mwananchi wa kawaida. Kiwe ni kitabu ambacho kitaundwa kwa lugha ambayo inaeleweka. Kama ni Kiswahili, iwe ni lugha inayoeleweka, Kiswahili. Ikiwezekana, hata kwa lugha za kinyumbani; Katiba iundwe kwa Kinandi, Katiba iundwe kwa Kigiriama, Katiba iundwe kwa Kijaluo, Katiba iundwe kwa Kiswahili. Kiwe ni chombo ambacho mwananchi wa kawaida anaweza kuishika na akaisoma, na ikiwezekana afikiye kila mmoja wetu, aijue. Tumeiunda, isibaki Nairobi. Siku nyingine nje, tuione huku kwetu Vitengeni hiyo Katiba.

Na mapendekezo yangu ni kwamba serikali hii iwe ya majimbo, na napendekeza kwamba Rais asiwe Amri Jeshi Mkuu. Rais awe na mamlaka yake ya Kiraisi. Lakini kuwe na mtu atakaye chaguliwa kuwa juu ya majeshi yetu yote. Pia, hali za U-judge. Judiciary, hiyo isiwe nayo iko chini ya Rais. Judiciary isiwe chini ya mamlaka ya Rais. Nafikiri hapo nimeeleweka.

**Com. Lethome**: Sawa sawa. Yaani ikuwe huru. Mahakama ziwe huru?

**Kennedy Mwangome**: Mahakama ziwe huru. Na upande wa usalama, hatuko na uhuru wa usalama. Unakuta unatembea kama ni town, umeshika begi yako, askari anakuvamia pale, na anakupiga piga Waswahili wa sasa wanaita "Tero". Kukupekesheni, na huna chochote ulicho beba, lakini atakupekesheni, ata wanaopita njia wanakushuku, "Huyu anabeba nini?

Mbona askari wamemuvamia?" Na baadaye hawataona chochote pale. Kwa hivyo hawa askari nao wana mamlaka mengine. Hasa polisi wanamamlaka mengine ambayo ni ya kutisha wananchi sana. Kwa hivyo ningeomba Katiba yetu ya sasa, hicho kipengele kiwe kitawekwa. Umekuta mtu amekufa mahali, pengine ni mtoni, pengine amejitia tanzi, lakini hata unaogopa kutoa ile report. Kwa sababu ukitoa report "nimeona mtu amekufa", wewe ndio unaitwa first suspect. Sasa hata kama ni wachungaji wameona mtu amejitia tanzi, mtu anaweza kuozea pale. Lakini kila mtu atakayemuona anaogopa kutoa riport. Polisi wetu wamekuwa ni watu wa kutisha raia sana. Kwa hivyo hiyo nayo, mimi ningeomba ukitoa report yeyote, uwe unasaidia polisi, unasaidia serikali lakini usiwe wewe ndiye unadhaniwa kwamba umefanya huo uhalifu.

Lingine ni upande wa PC, DC, DO. Ningependelea watu hawa waajiriwe kutokana kwa mikoa wanayotoka. Wawe wametoka kwa mikoa wanayotoka, wale wanaoajiriwa kama PC, kama DC, kama DO. Mambo ya maji, tunasema maji ni uhai, lakini Kenya maji kupata debe moja la maji ni gharama kubwa sana. Wengi wetu hawawezi ku-afford debe moja ya maji. Maji yamekuwa ghali kuliko hata chakula. Kwa hivyo ningeomba serikali yetu inayokuja, maji yawekwe kwa kiwango ambacho kila mtu ataweza kukigharamia. Na mawasiliano, barabara ziwe nzuri, hospitali ziwe… huduma hii ya hospitali iwe inagharamiwa na serikali na hata mawasiliano kama simu yaweze kusambazwa katika sehemu hizi za kimashambani.

Labda kwa kumalizia, nitasema kwa upande wa mambo ya mashamba. Ningemomba serikali inayokuja, kusiwe na mambo ya u-squatter kabisa katika Kenya. Kila mtu apewe kibali cha mahali anapoishi. Kila Mkenya apewe kibali cha mahali anapoishi, free, bure. Kibali hicho kisilipiwe chochote. Kusiwe na mtu ati anaitwa squatter ama anakaa mahali huko akilipa. Anamlipa mtu fulani kwa kukaa pale na yeye ni Mkenya amezaliwa hapa Kenya lakini mahali anapoishi anapalipia? Ningeomba Katiba yetu kusiwe na kulipa kodi, labda uwe umepangisha nyumba ya mtu, lakini si kulipa mahali umejenga nyumba upalipie. Mahali unaishi na jamii yako pengine miaka kumi au zaidi unapalipia? Mimi ningeomba Katiba yetu ya Kenya, iwe kila Mkenya anaweza kukaa mahali na kuwe na cheti cha kumiliki pale mahali. Asanteni.

**Com. Lenaola**: Asante sana. Emanuel Kiti?

**Emanuel Kiti**: Kwa majina yangu naitwa Emmanuel Kiti. Maoni yangu ni kwamba wamama wapate haki yao kutoka kwa wazazi wao. Oni la pili, wazee wa vijiji wapate mishahara. Tatu, maoni yangu ni kwamba baada ya Katiba kuundwa, tuletewe vitabu tuelezwe ama tujue ni nini, ama maoni yetu yamo katika kitabu. Ni hayo tu, Mungu awabariki.

**Com. Lenaola**: Asante. Tupate Robinson Mweri.

**Robinson Mweri**: Kwa majina, naitwa Robinson Mweri. Robinson Mweri. Mimi napendekeza hivi, vile ambayo tunaendelea, Rais kuchaguliwa na raia ni sawa sawa, lakini kuna ….

**Com. Lenaola**: Jamani kukae kimya tumsikize huyu jamaa

**Robinson Mweri**: … Kuna kitu kimoja, kwamba yeye yuko juu ya sheria. Kifungu kile kingeondolewa, ili akifanya kitu chochote, awe anaweza kupelekwa popote kama raia wa kawaida. Kitu chingine, Mjumbe awe na elimu, ili awe anaweza kuwapangia wale watu wake ambao anawatawala. Kiwango kama cha chuo kikuu.

Napendekeza hivi, chief, sub-chief na councilor wachaguliwe na raia wenyewe ili wanapofanya mambo ambayo hayafai, wawe hawana wa kumlaumu. Lakini sasa utakuta unaletewa mtu halafu baadaye anaanza kutusi mtu "Mulifanya kuniona hivi, hamukunichagua". Sasa, ukiangalia hivi, huna pa kwenda, unatatizika kiakili.

Hati za mashamba ziharakishwe ili watu wawe wanaweza kwenda pahali popote wakasaidika na angalau mikopo ili waweze kujimudu kimaendeleo. Watoto kutoka standard one mpaka standard eight, elimu yao iwe ya bure. Na mtumishi yeyote ambaye ni wa serikali, sio wote ati kuwa ni wabaya, lakini kuna baadhi yao mambo yao si mazuri. Sasa mtumishi kama yule akipatikana, na yale makosa kama ufisadi, ashtakiwe moja kwa moja. Sio kungojea kibali kutoka kwa mkuu wa sheria halafu munaona mambo yanaenda hivi hivi mwishoni munaona amerudi tena kazini. Hamuna pa kwenda. Lakini ashtakiwe direct moja kwa moja pale alipotenda ule uhalifu.

Kitu chingine ni wazee wa vijiji. Wazee wa vijiji wanafanya kazi kubwa lakini hawasulumiwi na pendekezo langu ni walipe angalau kitu kidogo ili nao waweze kujiskia. Sasa utamkuta karibu, kama vile anayofanya kazi sub-chief, ni yeye ndiye anaifanya pale kijijini na ana watu kama mia tano. Sub chief anangojea report, halafu ukienda huko pengine uaambiwa huyu ameanza kuzunguka zunguka kutafuta pesa. Sasa ninaomba, mapendekezo yangu, wawe wakifikiriwa. Kwa hivyo mimi sina mengi ni hayo.

**Com. Lenaola**: Asante. Tupate Juma wa Magogo

**Juma Magogo**: Kwa jina mimi ni Juma wa Magogo kutoka Vitengeni.

**Com. Lethome**: Sauti Bwana!

**Juma Magogo**: Kitu cha kwanza mimi napendekeza ni upande wa ma-chief na sub-chief, wawe wanachaguliwa kwa miaka mitano. Pili Rais awe anaweza kuchaguliwa kwa miaka kumi. Upande wa land, napendekeza kuwe hizi title deed ziwe zinaweza kutoka kama umepimiwa shamba yako na hakuna kesi yeyote na shamba yako. Uwe unaweza kupewa kama miezi mitatu upate title deed yako, kusudi ufanyie mambo yako ya kimaendeleo.

Kilimo; Katika Pwani hapa tumezoroteka sana upande wa kilimo. Kwanza kwa upande wa Korosho, tunaona korosho kwa

wakati huu haina faida yoyote. Kwa nazi, pia nazi nazo hazina faida.  Kwa hivyo napendekeza kwa hayo mambo tuwe tunaweza kupata kiwanda kizuri kama ile ya korosho iregeshwe, na pia upande wa mnazi sasa, nataka ifanywe kama breweries. Tuseme hapa Pwani, kuwe kuna hicho kiwanda. Iwe hii pombe inaweza kusafirishwa mpaka ng'ambo kusudi tupate pesa, faida ya mnazi tujue ni nini ili tuweze kujiendeleza.

Upande wa madiwani, hawa watu wawe wamesoma mpaka kiwango kama form four. Kitu kingine ni upande wa serikali za wilaya. Tunaweza kusema hii arghi yako inachukuliwa na county council.  Sasa council ile inachukua pale kwako, wewe mwenyewe unafukuzwa na hupewi kitu. Ili sasa  council inachukuwa zile pesa za kila mwake pale. Kwa hivyo hata hawa kuingia kwa upande huo nasema wao wanunue, yule mwenye pale pia ajue amefaidika.

Nyingine ni upande wa kustaafu.  Hii miaka ipunguzwe sababu watu wamekuwa wengi hawana kazi. Miaka arobanne na tano iwe mwisho, atoke  ….

**Com. Lethome**:  Ngapi?

**Juma Magogo**:  Arobanne na tano.

**Com. Lethome**:  Una miaka mingapi?

**Juma Magogo**:  Mimi?  Thelathini na nane.

**Com. Lenaola**:  Itakuwa una miaka misaba ndio utoke?

**Juma Magogo**:  Ndiyo watoke waingie wengine ambao hawana kazi.  Sio kukaa mpaka hamsini na tano. Hiyo iwachwe wazi. Upande wa elimu, elimu iwe ni ya bure kutoka nursery mpaka standard eight.  Na afya pia, upande wa madawa, upande wa hospitali matibabu yawe ya bure. Na upande wa jela, mtu kama ameshikwa, awe anaweza kuwekwa cell kwa masaa ishirini na nne, si akae hapo miaka na miaka.  Yangu yameisha, asanteni sana.

**Com. Lenaola**:  Asante sana Bwana Magogo, sasa Mama Dalma.

**Mama Dalma**:  *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: She has a child who is in secondary and the husband is sick what will she do and she doesn't have the money?

**Com. Lenaola**:  What does she suggest?

**Mama Dalma**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: O.K. She want, free education for that child so that she can finish her education.

**Mama Dalma**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: The other problem is about the road, She wants, the road constructed so that transport can be easy.
**Mama Dalma**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: She has said they are traditional dancers and they have come to entertain and they want to be given that chance.

**Mama Dalma**: *(In Giriama Dialect)*

**Translator**: She doesn't have any more.

**Com. Lenaola**: Margaret Keah? Leonard Baya?

**Leonard Baya**: Kwa majina naitwa Leonard Baya, nashukuru kuwa pamoja nanyi kwa kutoa maoni yangu kwenyu. Maoni yangu ni kwamba serikali ijayo, mimi naomba iwe ya. majimbo. Na katika majimbe ile ambaye ninaomba ni kwamba, hatutaweza kuondoa kabila lolote kwa jimbo lile au pale. Njia ambao tunataka ni kwamba, kila kabila iweze kuwa inakuwa hapo, lakini mapato katika lile jimbo lile, yaweze kutumika kama sabini na tano za mia, ziweze kutumika pale pale kwa lile jimbo. Baadaye ishirini na tano za mia, ziweze kuenda kwa serikali kuu ambapo wakati zikifika huko, jimbo lile ambalo litakuwa haliwezi, ama halijimudu kabisa, liweze kusaidika na hii ishirini na tano kama ambavyo inafanyika katika cost sharing mahospitalini. Hiyo itaweza kusaida kwa sababu tumeona wakati ambao umepita, wakati mwingine mapato yote yalikuwa yakienda kwa serikali kuu, baadaye kumekuwa kwamba mapeni haya yanaweza kuwa yanatengwa kupelekwa pande fulani fulani, kwingine kuna kosa. Na wakati huu, serikali ijayo tunataka kila mwananchi aweze kufaidika na pato lile ambalo liko katika jimbo lake.

Kuhusu ardhi; Ardhi ni jambo lingine ambalo linakasirisha kabisa hapa kwetu Pwani. Kwanza tukifikiria tangu sheria ile ya mkoloni ambayo walikuwa wanaweka kwamba beach plots, na front plots kutoka baharini, tunaziona ya kwamba hazina wenyeji. Zote zimekuwa kwamba zinapangwa kutoka juu huko, na ni ajabu kama bahari ile ilipokuwa, haikuwa na wenyeji. Tungeomba serikali ijayo iweze kuona kwamba, katika hizi beach plots, ziweze pia kupatiwa wananchi wenyewe kwa sababu gani? Kuna uwezekano miaka ijayo, kama mtu amefika Kilifi pale bridge, aangalie kwa ile beach plots ambazo ziko pale, wale jamaa wameanza kuweka kuta katika beach huko, na ni kalango tu. Baadaye unaona “Mbwa Kali”. Kama baadhi ya miaka

mia tatu au mia moja hamsini ijayo, hakuna watoto kutoka huku kwetu wataweza kufikia hata yale maji. Tukipata kama kwingine kama Amsterdam au Rotterdam kule ambako watu wanaishi kwa bahari na meli, nchi imejaa. Basi utakuta watoto wetu hata hawataweza kufika kabisa kufika pale chini. Kwa hivyo napendekeza serikali ijayo iweze kuona katika zile beach plots ambazo ziko mikononi mwa serikali, ziweze kupatiwa wenyeji ambao waweza. Na kama mtu amepata, wasiweze kuweka, wapatiwe nafasi, watu waweze kuteremuka hata kupata ile maji, au kuona yale maji. Isije ikawa mpaka kuteremuka ni tuende tukatoe pesa kama museum.

Chingine ni kile cha ardhi, title deeds. Hii ninasema ikiwezekana, serikali ijayo itusaidie. Kama pahali pamepimwa na pamemalizika, na baadaye kuna kesi kama mia mbili, na watu mia nane wameandikishiwa wale ambao hawana kesi wapatiwe vibali. Kwa hivyo natoa maoni kwamba, wale watu wote mia sita hawana shida yeyote, wapewe title deeds. Na mia mbili au ni mia moja ndio wenye kusumbuana pale, wamalizane wenyewe bila kufanya watu wasipate hizi titles kwa miaka mingine kama kumi na mitano hivi. Tuweze kuzipata mapema. Ili wabaki wale wale ambao wana hizo kesi.

Maendeleo; Maoni yangu nafikiria maendeleo wakati huu, yaweze kufika kwenye kijiji kabisa ili mwananchi wa kawaida, chochote ambacho kinatengenezeka, kisifikiriwe kwamba kimetengenezwa na serikali ijayo. Kama ni hospitali ikijengwa, wajue ni yao wanaijenga. Na hii ni kwamba serikali kama imesaidia, badala ya kama ni cheque, (kama wakati ule mwingine kulikuwa na RDFs kutoka kwa districts) badala iwe kwa DC hapo, ijaribu kupelekwa kwa account ya development kwenye kijiji ili waweze kuangalia wenyewe kwamba ile miradi wanaendelea namna gani, na utaendelea kwa hali nzuri bila mambo ya corruption. Hayo ndio ambayo nilikuwa nayo.

**Com. Lenaola**: Una dakika moja kumalizia.

**Leonard Baya**: Nikichukua upande wa ma-chief, mimi naomba ma-chief waweze, kama serikali ijayo, wanaweza kuwa pia wapatiwe transfers. Upande mwingine, two, ma-sub-chiefs…

**Com. Lethome**: Usizungumuzie juu ya serikali ya ijayo, zungumuzia juu ya Katiba ijayo.

**Leonard Baya**: Katiba ijayo, oh! Asante sana. Katiba ijayo, ma-chief waweze kupigwa transfer, waende kufanya kazi kwingine. Wabaki tu ma-sub-chiefs ambao hao ndio wanasimamia miji au vijiji vile ambavyo viko. Kwa hayo naweza shukuru. Asanteni.

**Com. Lethome**: Hao machiefu watakuwa ni watu wa kuchaguliwa au wa kuteuliwa?

**Leonard Baya**: Vyovyote vile ambavyo hata kama wangekuwa, bora ni wawekwe transfers. Kwa sababu kama ni kuchaguliwa, itabidi sasa, kule atakoenda, wanaweza kumkataa.

**Com. Lenaola**: Asante. Justin Kapombe?

**Justin Kapombe**: Kwa majina naitwa Justin Karisa Kapombe. Mapendekezo yangu ya kuhusu Katiba, kwamba serikali ile ambayo inakuja - - katiba ile ambayo inakuja, napendekeza tupate serikali ya majimbo. Na Rais asiwe Amri Jeshi na atawale kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Wabunge, pia vile vile. PC, DC, DO's wawe pia wanatoka mkoani. Ma-chief na manaibu wao, wachaguliwe na wananchi, pia wawe na elimu kufikia kidato cha nne.

Elimu ya msingi iwe bure na mfumo ule wa zamani wa kuanzia darasa la saba, form four na form six mpaka university, ubaki ule ule. Kuhusu mashamba, haki za kumiliki mashamba zipatikane haraka iwezekanavyo, unadikishaji utakapo malizika kwa sehemu ile ambayo itakuwa imeandikishwa. Wananchi wenye viwango vya chini vya elimu kuanzia darasa la nane wawe wanaweza pia kufikiriwa na kupatiwa nafasi za kazi katika mashirika nchini. Kila raia wa Kenya lazima awe mzaliwa wa hapa na awe na kitambulisho cha kitaifa.

Madiwani wawe na elimu kuanzia darasa la nane, hadi kidato cha nne, na umri wa miaka ishirini na mitano, hadi arobanne na mitano. Serikali iwe ina control price ya vyombo na vyakula vinavyouzwa nchini.

Kumi na moja, suspects au washukiwa wasiteswe na askari kabla uchunguzi haujafanywa. Hospitali za kiserikali zihudumie raia bure. Asante

**Com. Lenaola**: Asante sana. Malevu Mabira?

**Malevu Mabira**: Kwa jina naitwa Malevu Mabira. Mimi yangu nataka serikali ijayo iweze kutoa vibali vya mashamba. Ya pili, angalau hapa Pwani chuo kikuu kijengwe hapa. La tatu, nataka elimu ya wazee, yaani gumbaru iletwe. Basi yangu ni hayo tu.

**Com. Lenaola**: Asante. Benjamin Saha Jefa?

**Benjamin Jefa**: Naitwa Benjamin Saha Jefa, nina maoni yafuatayo. Serikali ijayo …

**Com. Lethome**: Ongeza sauti.

**Benjamin Jefa**: Katiba, nataka au nina maoni ya kwamba iwe ya majimbo. Rais awe na waziri mkuu. Katika kila jimbo au mikoa, iwe na ma-governors na wafanya kazi wa kiserikali, lakini wale watenda kazi wa kiserikali ma-DC na ma-PC wawe wanatoka katika mkoa huo, wawe ni wenyeji. Na watenda kazi wa serikali wengine ambao wanafanya kazi katika mikoa

ambako hawatoki hapo, kuwe na ushuru fulani ambao watatozwa, mapato yote yaende katika jimbo hilo.

Sehemu ya wabunge, au katika hapo kwa urais, nina maoni ya kwamba Rais awe amefuzu katika chuo kikuu, tena awe na miaka arobanne na tano mpaka sitini na tano. Tukienda sehemu za wabunge, nina maoni ya kwamba wabunge wawe na vipindi viwili vya miaka mitano mitano. Hata upande wa Rais, pia hapo kuna vipindi viwili vya miaka mitano mitano, na mbunge akiwa amepata miaka mitano ya kwanza na miaka mitano ya pili, akiwa na miaka kumi, anaweza kupigania urais lakini hakuwezi kuundwa kikundi cha chama halafu apiganie tayari urais na hajakuwa mbunge. Hii tunaona ya kwamba hana ujuzi kuwa mbunge au kutawala. Kwa hivyo lazima awe mbunge mwanzo ndio awe Rais.

Na wabunge wawe na elimu angalau ya kufikia form four. Wawe na miaka arobanne na tano, mpaka sitini na tano. Madiwani, pia nao wawe ni wasomi, wawe angalau wana cheti cha darasa la nane. Wawe wamekomaa kidogo kiasi cha miaka thelathini mpaka sitini na tano. Na Madiwani pia wapigiwe kura kwa vipindi viwili vya miaka mitano mitano.

Tukienda kwa upande wa ma-sub-chief na ma-chief, hao pia wawe wa kupigiwa kura. Nao waweze kuwa katika wadhifha huo kwa miaka hiyo kumi, yaani vipindi viwili. Na pia hawa wote; Rais na madiwani na wabunge na ma-sub-chief na chifu. Na kipengele chingine hapa chini cha wazee wa kijiji, pia nao waweze kuwa katika sehemu za vijiji kuchaguliwa kwa kura na wanakijiji kwa miaka miwili. Lakini kukiweko na sababu yeyote ya kutosha, ya pengine udanganyifu au mahongo au sababu za kutosha, tunaweza tukafanya vote of no confidence na hata rais au mbunge au diwani au subchiefu au chiefu au mzee wa kijiji kabla miaka yake haijaisha, tunaweza tukamtoa katika kile kipindi hakijaisha na tukamchaguwa mwingine, siyo kwamba kuchaguliwa miaka mitano mpaka iishe. Ukifanya makosa ya kutosha unaweza tu kutolewa.

Sehemu nyingine ni sehemu ya mashamba, ardhi. Tunaona kwamba kipengele kile cha kuziba sehemu moja ikiwa imetamukwa ya kwamba iandikishwe, ikiandikishwa na kuwe na kesi fulani fulani hata kesi moja itazuia vyeti vyote. Hiyo mimi nasema katika katiba ijayo, kila atakayekuwa ameandikisha shamba yake, ikimaliza miezi mitatu ikiwa bado haijashtakiwa hiyo number yake, apewe cheti chake. Wale ambao wanazozana waendelee kuzozana mpaka wapate suluhisho lakini wale wengine wapate vyeti ili waendelee na maendeleo.

Katika sehemu nyingine ya kortini, tunaona kwamba hawa wazee wa kijiji ambao wametusaidia sana, hatutaki pia tuwafute, lakini ningetaka wawe kama kila kijiji watano watano. Na pia kuwe na karani kutoka kortini ambapo atakuwa posted katika kila sub-location ashikamane na hawa wazee wa kijiji ili katika kuamuwa kwao cases za kinyumbani, yeye awe anaweza kuwa msaada katika uamuzi, na kama pengine ni jambo ambalo litakuwako limeelekea kwamba hatua itachukuliwa ya mbele, basi karani wa kortini aandamane naye aende naye.

Kuhusu elimu, elimu ninapendekeza kwamba wanawake kwa wanaume, watoto wetu iwe ni elimu ya bure ya primary mpaka secondary. Wanawake hasa watiliwe maanane sana ya kwamba wapewe nafasi ya mbele za kupewa kazi au kupewa msukumo

hata kama ni msaada hao wasome kwa wingi ili wapatikane katika sehemu nyingi ambazo wanawake wamekosekana. Na katika hiyo serikali kwa sababu za elimu hii ambayo nimependekeza ya bure, nina maoni ya kwamba hata hiyo serikali nayo iwe na mpango wa uzazi. Kwa sababu kama tutasema watoto wote wasomeshwa bure na hawajui kama ni watoto wangapi ambao tunawazaaa sisi wananchi kwa mwaka, inakosa magisio na inakosa kuwapangia fee au gharama za hawa watoto. Kwa hivyo kama ni wazazi, waelimishwe habari ya upangaji wa uzazi, na kama kila mzazi apewe kama ni watoto fulani ili serikali ijue miaka mitano hii, tunatarajia tupate watoto fulani ambao applicants wameapply ya kwamba wanataka watoto. Ihidhimishwe wasizae bila kuhidhimishwe.

**Com. Lethome**: Unapendekeza kila familia iwe na watoto wangapi? Pendekeza iwe na watoto wangapi.

**Benjamin Jefa**: Watoto watano, iwe ndio mwisho, hio ndio hatuwa ya juu zaidi.

**Com. Lethome**: Akipitisha hapo?

**Benjamin Jefa**: Akipitsha hapo - - mwanzo hawezi kukua na mimba Bibi yake mpaka aidhinishwe mwanzo kwamba yeye ana uwezo ya kwamba… Lakini si uzae tu uzae tu, na hakuna uwezo. Unaletea serikali gharama! Na upande wa afya, upande wa afya ningependekeza ya kwamba kila location kuwe na dispensary ambayo itakuweko. Hiyo inatoa huduma za bure kwa wagonjwa wanatibu magonjwa madogo madogo au kutoa huduma za uzazi , hata mambo ya kutahiri yawe katika hospitali. Iwe bure, lakini ile ya clinic na health centres kuwe na gharama kidogo ya cost sharing.

**Com. Lethome**: Jambo la mwisho?

**Benjamin Jefa**: Asante nafikiri nimefika mwisho.

**Com. Lenaola**: Asante. Samuel Ngumbao?

**Samuel Ngumbao**: Asante mimi kwa majina ni Samuel Ngumbao. Nataka kuchangia Katiba yetu itakayokuja. Ya kwanza, Rais awe anachaguliwa na wananchi na asiwe mbunge. Awe anachaguliwa na Kenya nzima yaani. Pili, iwe uchaguzi wa rais usishikamane au kuwa pamoja na wabunge. Rais achaguliwe, iwe ni race ya watu wawili au watatu marais peke yao, tuchague marais halafu ndiyo tuingie mambo ya wabunge, wachanganyikane na madiwani, na rais asiwe akiteua wale ambao anawateuwa kwenye ma-parastatals au wale ambao ni nominated MPs. Wasiwe akiteuwa yeye ni basi, iwe pia wanaidhinishwa na Bunge.

Na tukirudi upande wa mahakama yetu. Ichukuliwe kwamba judiciary iwe independent. Iwe haiwezi kuwa interfered na President ili wahakikishe wanatoa haki kwa wale wahusika ambao ni washtakiwa. Kusiwe na interference, ndiyo nataka kuwaeleza hapa. Halafu tukirudi upande wa elimu, mimi nataka kusema kwamba elimu iwe ya bure kutoka nursery mpaka

standard seven. Halafu kutoka kidato cha kwanza mpaka cha sita-yaani tunataka kurudia ule mfumo wetu wa zamani-kufikia hapo, kuwe na cost sharing kidogo hapo lakini nilikuwa na propose kwamba, ikiwezekana serikali ianzie kutoa loan kutoka hicho kidato cha kwanza mpaka university. Itoe loan. Wale watoto wahakikishiwe kwamba watapata kazi na walipe pole pole mpaka watakapomaliza. Wao ni wananchi wa Kenya kwa hivyo hata kama wataenda kufanya kazi nga'mbo, walipe hiyo. Lakini isiwe mzigo wa mzazi jamani. Hiyo napendekeza.

Halafu tukirudi upande wa afya, tukirudi upande wa afya, ninapendekeza kwamba, tuwe na mfumo kama ule wa Wingereza. Kuwe na shirika kama hili letu, tunaliitaje lile la afya? Mtu ukilazwa unalipiwa? (interjection). Basi iwe ni kwa mwananchi yeyote hata kama wewe ni mkulima ni nani, uwe una-contribute kidogo. Lakini ukiwa mgonjwa uwe unaenda hospitali unatibiwa bila wewe kuwa na hela. Kwa sababu wakati wa ugonjwa haubishi hodi. Ngonjwa unakuja wakati wowote, sasa ukienda kule unaulizwa maelfu ya pesa, si nikusema tu yule mgonjwa afe? Basi kuwe na taratibu kwenye Katiba yetu kwamba kuwe na hilo shirika la kuwahamasisha watu wote, waingie katika hilo shirika, ili mtu akiwa ni mgonjwa, aende hospitali na apate matibabu wakati huo. Ni upande wa hospitali.

Upande wa ardhi, ninataka kusema hivi, wageni wanokuja hapa, wasichukue ardhi yetu ati wakaambiwa amenunua. Wawe wata-lease tu, lakini ardhi yote iwe iko chini ya serikali. Mwananchi anaweza kupatiwa sehemu, eh, akapatiwa na title deed lakini mgeni yeyote anayekuja kujenga manyumba yake na nini, awe ana-lease kwa muda halafu ile ardhi yote ni ya serikali. Isiwe wananunua. Wanatufanya sisi ambao ni wananchi tunakosa haki zetu. Ma-beach plot, mtu anakuja, anakuwa allocated anauza. Na sisi wananchi tunabaki hatuna lolote. Kwa hivyo ninaomba, Katiba yetu ionyeshe haki ya ardhi yetu, tupatiwe vile vyeti kama wenzangu walivyosema, tupatiwe vyeti, lakini sehemu nyingine iwe ni ardhi ambayo ni ya serikali. Kama wewe ume-lease, na huwezi ku-utilize ile ardhi, yaani huwezi kuifanyia kazi, iwe unaweza kupokonywa na ikapewa mtu ambaye anaweza kuzalisha kwa sababu haina maana kama hutaweza lisha chochote. Kwa hivyo iwe inaweza kupewa mtu mwingine na akazalisha ili uchumi uweze kuendelea. Huo ni upande wa ardhi.

Halafu upande wa usalama, nafikiria Rais, kwa vile atakuwa anachaguliwa moja kwa moja, awe pia ana Waziri Mkuu ambaye atakuwa mkubwa wa serikali. Rais awe ni ceremonial ikiwezekana, na wengi wetu hapa tume-propose juu ya majimbo. Mimi nafikiria hayo majimbo, hatujafikia hapo kwa sababu ya hali ya rasilimali zetu. Pengine tukiambiwa tuweke mapolisi wetu hapa na jeshi letu hapa, au tuseme jeshi litakuwa ni serikali kuu lakini police, tunaweza shindwa hata kuwalipa mishahara yao ili watulinde katika lile jimbo.

**Com. Lethome:** Toa pendekezo.

**Samuel Ngumbao**: Mimi napendekeza serikali moja, lakini yaani zile sehemu za utawala, ziwe zitalindwa sawa sawa. Kusiweko na mambo ya ufisadi na kila chombo kiwe kinaweza kuwa checked na chombo chengine. Kwa mfano ikiwa ni ofisi ya Rais haiwezi kufanya jambo lolote bila kuwa checked, iwe bunge inaweza kucheck. Ikiwa ni judiciary, inataka kwenda

upande wa ufisadi na nini, iwe kuna chombo chingine kinaweza ku-check. Sasa hapo itakuwa mambo yetu yote yetu yanaenda sawa sawa. Kwa hivyo nafikiri ni hayo tu.

**Com. Lenaola**: Asante. Hamisi Kazungu?

**Hamisi Nyanje**: Mimi naitwa Hamisi Kazungu Nyanje. Maoni yangu ni serikali iwe ya majimbo, tupate vyuo vikuu huku. Pili, madiwani nao wachaguliwe kwa hiyo miaka mitano pia. Na wakusoma au asiyesoma achaguliwe, bora maendeleo iwe inaonekana. Tatu, machifu wachaguliwe kwa mlolongo. Ma-sub-chief nao wachaguliwe lakini hapa hawa ma-sub-chief hawana kazi. Kazi yao ni kufanyisha punda hawa wazee wa vijiji tu, kukaa ofisini bure.

**Com. Lethome**: Unapendekeza nini?

**Hamisi Nyanje**: Waondolewe hawa .

**Com. Lethome**: Tusiwe na cheo cha ma-sub-chief?

**Hamisi Nyanje**: Eh, kuwe na hawa wazee wa kijiji wapate mishahara kidogo. Nafikiri chief atapata kazi kubwa.

**Com. Lethome**: Endelea

**Hamisi Nyanje**: Mambo ya kuhusu minazi, tembo haitakikani. Sisi tunataka hii ifunguliwe iwe wazi. Kama miraa vile, yote ni ulevi ule. Ihalalishwe. Ma-license yakatwe sawa sawa. Mambo mengine ya wasichana, wasichana wanatakikana, wengine wanasema wapate haki kwa wazazi wao, kama shamba. Hakukuwa amezaa pale, apatiwe sehemu kidogo. Hiyo italeta fujo. Napendekeza isiweko hiyo. Mtu akiwa amezaa pale, aende huko huko. Maanake akipendekeza tukimpatia kitu kidogo pale, ataleta jamaa mwingine, tutatiana visu huko maanake hana pahali pa kukaa.

**Com. Lethome**: Hebu ngoja, msichana hajaolewa.

**Hamisi Nyanje**: Hajaolewa

**Com. Lethome**: Halafu atiwe mimba, babake amekufa.

**Hamisi Nyanje**: Babake amekufa?

**Com. Lethome**: Ndungu zake wamepewa urithi yeye apewe pia ama asipewe?

**Hamisi Nyanje**: Asipewe! Kwa nini, hatapata Bwana yeye? Hata wa bure yuko, bwana ako. Maoni yangu asipewe, maanake atafanya kusudi ya kuzaa hapa, sasa mashamba yatamalizwa na hawa wa huko msituni! Na yule mtoto akitiwa mimba, akikubali kutiwa mimba, achukuliwe hatua ya kufungwa kama hata miaka kumi kwa sababu mlango hauwezi kufunguka kabla kufungua mwenyewe. Mtu anabisha basi mlango ufunguke.

**Com. Lethome**: Sasa nani aadhibiwe?

**Hamisi Nyanje**: Msichana. Msichana ndiye aadhibiwe.

**Com. Lethome**: Na mvulana, yule mwanamume?

**Hamisi Nyanje**: Ataadhibiwa kama miaka mitano! Maanake yule matani; ni matani ule anakubali tayari. Yaani akipata mimba atapata urithi pale; kwa hivyo hajali. Na haya maandishi ya watoto wamezaliwa; unaandikisha mtoto, halafu unataka karatasi ya kuzaliwa; pengine anatakikana shule; inasumbua watu kutafuta kule na kule na kule ni gharama kubwa. Ingeandikishwa kwa chief, akitakikana karatase ile ipatikane huko kwa chief tena. Na mambo ya mila nyingine ya uchawi hii kwanza. Uchawi uko, tunataka hii Katiba mpya, sasa iangalie hao wachawi. Wachawi, kesi zao ziregeshwe kwa wazee. Ukiangalia kutakuwa kuna haki yule mtu atachukuliwa hatua, lakini sasa kwa wakati huu, ukisema mtu mchawi, anasema, "Mimi nimeokoka, mimi hata mambo hayo siyawezi haya." Sasa anakusumbua jioni, mchana anakusumbua na yeye ameokoka na ni mchawi kweli.
Kuna mila nyingine ile ya mvua. Wako hapo na wameikoka. Sasa njaa imejaa kabisa kwa sababu ya hawa waokovu hawa. Wameokoka na mila zao wako nazo. Kwa hivyo tunataka hiyo iregeshwe kwa wazee watatue, ule utamaduni uendelee. Akiwa ameua, ashtakiwe kuua yule mchawi. Akiwa yule amesingiziwa kama kawaida, yule wa kukuua na panga awe kama yule mchawi.

**Com. Lethome**: Haya, jambo lingine.

**Hamisi Nyanje**: Jambo lingine? Sasa hata nikiwa nimemalizia pia niendelee?

**Com. Lethome:** Umetosheka?

**Hamisi Nyanje**: Haya, nimetosheka, ni mengi lakini yamesemwa tayari.

**Com. Lethome**: Asante. Tupate Joseph Kambire.

**Joseph Kambire**: Kwa majina yangu naitwa Joseph Kambire. Kwa kurekebisha ile Katiba yetu ambayo inakuja,

ningelipenda kusema juu ya hizi, nazungumuza kuhusu hospitali. Hospitali, watu wanatibiwa. Ningependa watibiwe ingawaje si bure lakini watibiwe kulingana na vile walivyo kwa sababu utakuta mtu hana pesa nyingi. Mtu pengine mapato yake ni kama pengine kwa kutwa anapata mia mbili na akienda hospitali inaitishwa kama elfu kumi. Hii, ningependa upande wa hospitali, Katiba yetu inayokufa, tunayorekebisha, watu watibiwe kulingana na uwezo wako.

Vile vile pia kwa upande wa Rais wa nchi, Mimi ningependelea kwa maoni yangu awe atatawala miaka minne. Miaka menne ile, akipagiwa kura, hata pengine ikiwa amekaa pale, amepigiwa kura na ako pale anatawala, kuna maadui zake. Maanake rais akiwa na maadui zake, sisi raia tunaumia. Wengine wanasema wataficha majunga, wanasema sisi tumeficha unga, basi huyu Raisi wenyu awape kitu kama vile. Sasa akiwa na miaka mingi pale, sisi raia huwa tunumia, lakini akdiwa na miaka michache hata kama wale adui zake wanampiga vita pale, baada ya ``miaka michache hata kama wale adui wanampiga vita pale, baada ya miaka michache utakuta ule uchaguzi unakuja na hapo itakuwa ni nafuu kwa wananchi. Hayo ni mapendekezo yangu, napenda iwe vile. Kwa hivyo, sitaongezea sana kwa sababu sikuandika.

**Com. Lenaola**: Asante. Emmanuel Masha.

**Emmanuel Masha**: Jina langu naitwa Emmanuel Masha. Sehemu ya kwanza ni ma-sub-chief. Ma-sub-chief na chief wawe wakichaguliwa na wananchi kwa sababu wametunyanyasa siku nyingi sana. Wewe umeibiwa ukifika pale unasema, " Mimi nimeibiwa," Anakwambia, " Nenda kule kwa askari ukaelewane nao". Ukifika kule unaambiwa "Mzee una elfu moja?" Na wewe huna. "Ikiwa huna basi nenda!" Huta pata msaada wowote hata leo ukaibiwa, hutapata msaada wowote, maanake lazima uwe na pesa. Basi yule askari abebe bunduki yake akufuate lakini bila hivyo, hakufuati. Sijui kwamba huyo askari analipwa na serikali au tunamlipa sisi wananchi.

**Com. Lethome**: Pendekeza

**Emmanuel Masha**: Kwa hivyo nataka ma-sub-chief wapigiwe kura kwa muda wa miaka mitano tu, na chief pia apigiwe kura kwa muda wa miaka mitano peke yake. Jambo la pili, Rais, tunataka awe ni mbunge. Kwa sababu akiwa si mbunge, hajui kawaida ya pale bunge kabisa. Anaenda basi tumempigia kura, amepita, ni mgeni kabisa, hajui lolote! Kwa hivyo tukimpata ni mbunge, atakuwa na usawa kabisa maanake anajua hali za pale vizuri sana na anaweza kutusaidia, na tukimpitisha, awe na kipindi cha miaka ishirini ili tujue huyo Rais, akipita awe akichukua kipindi cha miaka ishirini angalau tupate angaa zile pesa zake lakini tukisema miaka mitano, hata pesa zake hatutazipata, Maanake miaka mitano akiwa hatafanya vizuri, anatolewa. Miaka mitano hatafanya vizuri, anatolewa, hata pesa zake hatutaziona kabisa! Lakini akiwa miaka ishirini huyo Rais, hatimae hata pesa zake tutaziona.

Jambo la tatu ni hivi, kuhusu mambo ya lands. Mambo ya lands nimeona tukio moja huko Kilifi. Rais anatoa title deeds kwa shamba zilizotolewa huko Gede kwa muda wa miaka kama arobanne na tano ilivyopita. Isiwe hivyo, ni muda mchache tu,

wakisha kuandikiwa shamba zao, wapate title deed kwa njia ya haraka. Tena wajue kwamba huku ni mashambani, hakuna mapato yale sawa sawa na huko sehemu za Malindi, Pwani huko. Huko ni sehemu zingine. Mtu anaweza kukaa miezi mitatu, asipate kibarua chochote. Kwa hivyo mambo ya lands, title deeds zije kwa njia ya haraka sana.

Nimefurahia kitu kimoja kama elimu. Mtu ana watoto kama kumi, na hatimae wote wanataka kisomo. Wanataka wale, wanataka wavae, wanataka mambo ya hospitalini, yeye peke yake. Ikiwa katika mashule, wale ni bure, itakuwa ni vizuri sana. Itakuwa wazee sisi tunasaidika sana sana sana.

**Com. Lethome**: Iwe elimu ya bure katika kiwango gani.

**Emmanuel Masha**: Iwe elimu ya bure kutoka standard one mpaka standard four!

**Com. Lethome**: Maoni yake hao, maoni yake. Standard four ama form four?

**Emmanuel Masha**: Form four, ya form four. Poleni nimetafalika kidogo. Kutoka standard one, mpaka form four iwe ni ya bure, na jambo lingine tena ni jambo la mahospitalini. Watu wanaumia na magojwa nyumbani kwa sababu hawana pesa. Upendekezo wangu, nataka hizo hospitali zote ziwe ni za bure, kua matibabu yote yawe ni ya bure. Na jambo lingine ni hivi, Kuna jambo kama urithi. Urithi, ikiwa mtoto wangu wa kike amezaa pale, inanipasa mimi kumpatia urithi. Akiwa ameolewa na bwana mwingine, hiyo sasa amekatiza urithi, atajua yeye na bwanake huko. Lakini akiwa amezaa pale, itanibidi yeye apate urithi kutokana na shamba hilo kwa sababu nitawagawanyia wale watoto wangu na yeye apate urithi kwa sababu sina mahali pa kumpeleka kwa sababu ni mtoto wangu na yuko pale pale. Nikimkosesha urithi, sijui ataenda wapi.

**Com. Lethome**: Na ikiwa hajazaa na hajaolewa?

**Emmanuel Masha**: Sasa akiwa hajazaa na hajaolewa na ako pale pale, urithi atapata vile vile, baada akiolewa tu, basi awe amekatiza. Atajua yeye na bwanake. Lakini akiwa pale pale hajaolewa, ni sawa sawa tumpatie urithi maanake wote ni watoto wangu.

**Com. Lenaola**: Haya jambo la mwisho?

**Emmanuel Masha**: Jambo la mwisho, mimi ni Mchungaji. Wachungaji hawatiwi maanani na serikali. Hawapewi heshima. Unaweza kuta kwamba ukifika kwa sub-chifu, wanasema tumekataza mikutano ya usiku isendelee na ukiangalia hivi, ma-disco yanaendelea. Hiyo ni nini? Sasa tunakatazwa sisi tusifanye hivyo, kule wanakesha ma-bar! Na ma-disco, u siku wa siku kuu, wanakesha. Lakini sisi tunakatazwa. Ikiwa ni mkatazo ya kwamba kusikeshwe usiku, ni wote wasikeshe! Lakini ikiwa ni Wakristo peke yake, hivyo si sawa sawa. Kwa hivyo nataka Wakristo watiwe maanani sana. Waheshimiwe kama ilivyo inastahili, lakini ikiwa hatuheshimiwi, itakuwa ni jambo la aibu, na sisi tunamtukuza Mungu. Kwa Hayo, Mungu awabariki.

**Com. Lethome**: Asante. Samson Kitani Mele.

**Samson Kitani Mele**: Asante sana kwa sababu ya kufika katika mkutano huu mkubwa, ambao bado hatujawasili katika wakati unaokuja hata sasa. Tunashukuru serikali yetu kwa sababu kututia maanani sisi watu wa mashinani. Mimi ninaitwa Samson Kitani Mele, nakaa Vitengeni, ni mkaaji wa hapa. Kwa hivyo sasa, kuchangia kwangu ni kwamba, la kwanza haswa, serikali yetu nataka iwe ya majimbo. Hiyo ni mara ya kwanza. Serikali yetu iwe ya majimbo. Na pili, fees za watoto wetu wa kidato cha kwanza, wasome bure mpaka wafike darasa la nane. Wakifika darasa la nane, wataingia sasa kidato cha kwanza, wanaendelea form four. Sasa kule, fee ya kule sasa ipunguzwe. Ipunguzwe sana ili kusudi walio mashinani nao, wawe waweze kulipia wanaweza fee kwa watoto wao walio ma-secondary. Lakini kuanzia mashinani huku, wawe wanasoma tu mpaka wakifika kidato hicho, basi, fee iwe chini ili wapate nafasi ya kuingia na kwenda mbele. Hilo ni la pili.

La tatu, barabara zetu zitengenezwe. Katiba hiyo ambayo tunaiweka, kipengele hicho kiwe kimeandikwa, barabara zetu ziwekwe vizuri mpaka mashambani kusudi bibi zetu ambao ni wajawazito, wapatapo shida, wapate nafasi ya kubebwa na magari iliyo yanayoendeshwa kwa njia nzuri na kupelekwa matibabuni bila shida.

La nne, nataka baada ya kuwa serikali ya majimbo, sasa Rais wetu asiwe kijana zaidi.

**Com. Lethome**: Pendekeza, umri wake uwe ngapi?

**Samson Kitanimele**: Umri wake awe kama thelathini na tano au arobanne kwenda mbele. Huyo amekuwa na akili timamu.

**Com. Lethome**: Na kiwango cha juu?

**Samson Kitanimele**: Kiwangu cha juu kabisa kitakuwa kitakwenda mpaka makamu wako wa maisha yake ya hapa ulimwenguni hata kama ataishi kwa miaka mingapi. Lakini ukimtia kijana, kisha hana bibi, ai! Atavunja ndoa za watu. Haya, la tano. Katika sisi sote tulioko huku, kuna roho ambazo zinapita. Kila mtu ana roho yake hapa. Sasa roho ni kama hizi sharti. Mimi yangu ina mistari, na ya huyu ni nyeupe kabisa, na mwingine ni nyekundu. Mtu hupatwa na maafa ya kujinyonga. Anaweza kupanda yeye mwenyewe hapo kwa hasira zake za mjini kwake, haeshimiwi ni wananwake wake au watoto wake, akajifunga akajinyonga. Baada ya kujinyonga hivyo, sisi huenda kule kwa mkuu wa polisi tukamwambia," Casa kule tumepata kisanga hiki." Wanakuja, wanafika hapo, wanamwangalia wanapima vizuri. Wakimaliza wanamchukua wamtia garini, wanaenda. Tena wanamwambia yule amefiliwa, "Changa pesa ndio uchukue maiti yako." Napendelea sasa, akimbeba akienda naye, tena wamrudishe. Ndio mapendekezo yangu.

**Com. Lethome**: La kumalizia?

**Samson Kitanimele**: Kumalizia ni kwamba, sita, mashamba yetu. Tupate vile vyeti vya kumiliki, ili sisi nasi tuwe watu. Mwisho.

**Com. Lethome**: Asante sana. Daniel Baya.

**Daniel Baya**: Mimi nazungumuza kwa niaba ya kamati iliyochaguliwa kwa mambo ya marekehisho ya Katiba katika sehemu ya wakilishi bungeni ya Ganze, Jina langu ni Daniel Baya, na wanakamati ni kama wafuatao. Mheshimiwa Noah Katana Ngala, ambaye ni Mbunge wa eneo hili. Bwana Daniel Mwaringa ambaye ni District Co-ordinator, Alfred Masha, Susan Biria, William Mpola, Ruth Muramba.

**Com. Lethome**: Kama kunao walio hapa, tungelipenda wasimame. Tunamjua mheshima, tunamjua Daniel, wale wengine kama wako hapa wasimame tuwaone.

**Daniel Baya**: Kuna wengine tumewaacha Ganze, wanashughulikia huko.

**Com. Lethome**: Walioapa wasimame tuwaone.

**Daniel Baya**: Alfred Masha, Ruth Muramba, Joseph Mwaru, wao ndio wako hapa. Na mapendekezo ni kama yafuatayo; Muundo wa serikali, kwanza hilo ndilo kwanza. Wanataka serikali ya kiungo cha kati, ambapo kutakuwa na Rais aliyechaguliwa na watu, Rais huyu ahudumu kwa vipindi viwili vya miaka mitano, Kama wananchi bado wanampenda, aongezewe miaka mitano mingine zaidi.

Rais awe na makamu wake na awe amechaguliwa kutoka kila mkoa. La tatu, katika hicho kipengele cha kwanza, akuwe na Prime Minster, ambaye ni Waziri Mkuu, atachaguliwa na wale wabunge walioko bungeni. Huyu ndiye atakayekuwa anafanya shughuli zote za serikali. Mapendekezo zaidi, awe na watu wawili wa kumusaidia. Huyu Prime Minister awe na watu wa kumusaidia, wawili ambao watachaguliwa na watu.

Baraza la mawaziri; wateuliwe na Rais. Pendekezo la pili, mabaraza ya miji yawe na nguvu zaidi kwa kuhudumia wananchi. La kwanza, mayor, elimu yake angalau iwe ya form four, O'level. Councillors, elimu yao ya chini kabisa iwe ni darasa la nane, kama itawezekana kwa sababu watu wengine wanapendekezwa ni watu elimu yao huwa iko chini lakini watu wanawapenda. Muda wao wa kufanya kazi katika ofisi; awe akichaguliwa hiyo miaka mitano.

Kipengele cha tatu ni vyama vya kisiasa. Kuwe na vyama vingi vya kisiasa kama ilivyo sasa. Vyama ambavyo havina muelekeo mzuri, vina malengo ya kufanya ghasia visiruhusiwe kabisa, visiwe registered kabisa.

Sehemu ya nne ni Tume ya uchaguzi yenyewe (au niko mbiyo sana? Ni sawa?) Tume ya uchaguzi yenyewe, muundo ulioko sasa uendelee kuwa huo. Isipokuwa siku ya kupiga kura iwe public holiday ambayo watu wote wanaofanya kazi watakuwa na haki ya kwenda na kupiga kura.

Usalama wakati wa kupiga kura uimarishwe, kusiwe na ghasia ambao hatimae watu hupoteza maisha yao wakati wa shuguli za uchaguzi. Kipengele cha tano ni kuhusu ardhi. Ardhi zote za nchi hii kwenye Katiba hiyo ijayo wanapendekeza ziwe chini ya uongozi wa mabaraza, ambayo mabaraza hayo ndiyo yatakayohusika pia na kutoa title deed, vibali vya hiyo ardhi katika sehemu inayohusika. Pendekezo zaidi ninasema mtu aliyekaa kwa ardhi kwa muda wa miaka mitatu na zaidi apewe kitambulisho cha kumiliki ardhi hiyo au title deed.

Sehemu ya sita ni elimu. Kila mkoa uwe na university moja ya kitaifa, chuo kikuu cha kitaifa katika kila mkoa kimoja. Si vile vyuo vikuu vingi vinakuwa Nairobi lakini katika kila mkoa kuwe na chuo kikuu kimoja. Pendekezo hilo linasema pia elimu ya msingi iwe ya lazima na bure. Si iwe bure peke yake lakini watu ambao hawataki kuwapeleka watoto wao shule, kuwe na kipengele cha kuwalazimisha kuwapeleka watoto wao shule, ili angalau mtu mdogo katika jamii awe amefika darasa la nane.

Sehemu ya saba ni uajiri. Mashirika ya serikali na mashirika binafsi, katika kila jimbo au katika baraza, yawaajiri asilimia themanini na tano ya watu wanaotoka sehemu ile. Halafu ile sehemu itakayobakia wachukue watu kutoka mahali pengine. Naendelea kusema pia viongozi wa mashirika ya serikali na viongozi wa serikali wenyewe kutoka sehemu ile, wawe ni watu wa kutoka sehemu ile. Si watu wa kutoka mahali pengine.

Sehemu ya nane ni dini na mila. Dini zozote ambazo hali zao haziridhishi au zinahitilafiana na maisha ya watu kama vile kuna dini zingine zinasema, “Yesu anakuja mwaka ujao kwa hivyo watu wasisome, na wasiende shule.” Dini kama hizo zisiruhusiwe kabisa kwenye jamii zetu. Kuna dini zingine pia au kuna mila zingine ambazo zinahadharisha maisha ya wananchi, kama vile dini zingine zile ambazo zinafanya ghasia kama hizi za Mungiki na vitu kama hivi visikubaliwe.

Sehemu ya tisa ni habari ya afya. Mabaraza haya ya miji ambayo tutakuwa tumeyapatia nguvu katika ile Katiba mpya inayokuja, mapendekezo yetu ni kwamba yawe yanahusika na kutoa haya matibabu kwa wananchi. Kwa hivyo, karibu baada ya kilometre tano au kumi kulingana na population ilioko katika sehemu fulani, kuwe na zahanati moja, with a full maternity wing, well equipped. Kwa sababu wamama wetu wanashindwa kufika hospitali wakiwa na shida kama hizi za uzazi wanakufa njiani kabla ya kupata usaidizi. Kwa hivyo tunapendekeza haya mazahanati yawe karibu karibu kuwasaidia watu wetu pamoja na full maternity wing.

La pili ni kwamba kama kuna watu ambao wanafanya kazi katika hizo hospitali za umma, wasifungue clinic zao. Na kama mtu anataka kufungua clinic yake, a-resign huko kwanza, halafu aende kule afungue yake. Kwa sababu mara nyingi tumeona

madawa ambayo yanatolewa na serikali yetu yanapotea kabla ya kumfikia mwananchi, na ni sababu yanatolewa huku yakipelekwa kule.

Sehemu ya kumi ni kuhusu maji. Haya mabaraza kama yamepewa nguvu, pia yashuguliki upande wa maji kwa wananchi, angalau kila baada ya kilometre tano, kuwe na maji ya mrefeji ambayo mwananchi wa kawaida anaweza kujikinga kutokana na magonjwa mengine madogo madogo kama tyhpoid, na pia wakina mama wasipate ile shida ya kusafiri kwenda mbali kutafuta maji, huwa wanapoteza wakati wao mwingi. Asanteni.

**Com. Lenaola**: Asante sana Bwana Baya. Tumkaribishe Hon. Katana Ngala aweze kusema machache.

**Hon. Katana Ngala**: Asante Bwana Lenaola pamoja na wenzako ambao mumekuja, na wananchi ambao muko hapa. Mimi nitatoa maoni machache na maoni yangu, kama alivyosema Bwana Baya sisi tuko katika kamati ambayo tulikuwa tumechaguliwa tuweze kushugulikia mambo haya ya Katiba. Kwa hivyo tukaona ya kwamba pia na sisi tuwe na machache ya kusema. Kwanza ni kwamba tunashukuru sana serikali, tunashukuru sana Tume, kwamba imetupa nafasi raia na viongozi waweze kuchangia mambo ya Katiba itakayokuja, na ya kwamba imeweka maanani raia wa nchi ya Kenya kwamba wapewe nafasi na wao waweze kuchangia ili waweze kuona muundo wa katiba ijayo kwa wakati itakapokuwa imepitishwa. Kwa hivyo nataka niseme kwamba, muundo wa serikali ambao tunaona kwamba unaweza kufaa, ni muundo wa kiungo cha kati, lakini kama ilivyosemekana katika karatasi tuliyoandika, nguvu nyingi za muundo wa serikali hii, ziweze kupelekwa katika mikoa, na katika serikali ya mitaa. Hiyo tunaona inaweza kusaidia katika uendeshaji na usimamizi wa serikali zile ambazo zitakuja.

Pia tunafikiria kwamba katika hali hii ambayo tunaipendekeza hivi sasa, ikiwa imekubalika, kutakuwa kuna uwezekano ya kwamba tumetoa mamlaka zaidi katika maeneo yetu na kwa hivyo itakuwa inawezekana kusimamia mambo yetu kwa njia ambayo ni ya manufaa. Tunaamini tukifanya hivyo, ile hali ya utumishi na utoaji wa zile hali za yale matumizi au zile kazi za delivery services zitakuwa ziko karibu na watu wetu na tunaweza kuzisimamia vizuri kwa sababu tutakuwa tuko karibu nazo. Kwa hivyo delivery services zitakuwa ni muhimu, na pia tunaona ya kwamba, katika hali hiyo ya Katiba, kwa vile ni kiungo muhimu sana katika maendeleo ya raia, ni vizuri sisi sote ambao tuko hapa tuweze kuwa na njia ya kuweza kusimamia maisha yetu ya public kwa sababu tutakuwa katika hali hii ya Katiba tunayofanya ni kama ambayo tunajipangia namna tutakavyoweza kusimamia maisha yetu wenyewe katika siku hizo zinazokuja. Kwa hivyo tunaweza kuwa na uwezo wa kusimamia maisha yetu wenyewe katika siku hizo ambazo zitakuwa ziko mbele yetu. Kwa hivyo tunaona kwamba ni vizuri katika hali hii, serikali muundo wake uwe vile ambavyo tumetangaza.

Yale mengine ambayo yamezungumuzwa katika kutilia mkazo ni juu ya mambo ya ardhi. Na mimi nataka niseme tu kwamba mambo ya ardhi ni muhimu katika mkoa huu na nilazima yasikike kutoka kwetu na tuweze kusema muundo wake vile ambavyo tunautaka na mimi nafikiri vile ambavyo wengi mumezungumuza ni kwamba, mambo ya haki na mambo ya maonevu, mambo ya kutolewa na kuwekwa watu wengine, haya yameonekana kwamba yameleta taabu kabisa. Na ikiwa tumefanya hivyo katika

muundo wa serikali ambao tumesema, tunafikiri kwamba kitu muhimu ni usimamizi wa rasilimali. Rasilimali za watu wenyewe zinaweza kuwa na usimamiaji bora. Rasilimali ni mambo mengi ambayo yanaingia chini ya msemo wa rasilimali, mambo ambayo ni ya miti, pesa, mambo ya pahali ambapo ni kama Kilindini, na mambo ya hoteli, na mambo mengine; hizi rasilimali ambazo ziko katika eneo linalozungumuziwa. Kwa hivyo tunaweza kuwa na nafasi ya kuweza kusimamia vizuri ili tukaweza kuangalia mambo vile yanavyoendelea. Kwa hivyo katika upande wa kiserikali na katika mambo ya kusimamia rasilimali, tutakuwa tunafaidika katika hali zile ambazo tutaweza kuzisimamia.

Kwa hivyo mimi ni mmoja kati ya wale walichangia lile karatasi ambalo limesomwa na Daniel Baya hapa. Lakini katika kuongeza ningesema katika hii Katiba ijayo, mambo ya mazingira, mambo ya mazingira nafikiri ni muhimu kwa maisha ya binadamu wa sasa na binadamu wanaokuja. Hicho ni kifungu ambacho mimi mwenyewe najisemea. Mazingira yetu yamechafuliwa sana. Yameharibwa na tuko katika hali ya wasiwasi katika siku zijazo, kwa hivyo katiba inayokuja iichukuwe na itilie maanani mambo ya mazingara. Mazingara tusipoyatunza, yanaweza kutuweka sisi katika hali ya shida na mazingara ni kama hivyo ambavyo sote tunayafahamu, mambo ya miti, mambo ya mito na mambo mengine ambayo yanahusinana na mazingara. Ni vizuri Katiba inayokuja yaweze kuichangia vizuri. Yanaanza kuzungumzwa hivi katika vifungo vifungo lakini Katiba yenyewe pia iweze kuweka kabisa kwa mipaka ya kwamba mambo haya ya mazingira pia tungeweza kuyasimamia vilivyo.

Kwa hivyo, sitaki kuchukua wakati wenye mwingi sisi wenyewe tutapata wakati mwingine kuzungumuza kama wabunge, lakini nilikuwa na unga mkono tu karatasi tuliopitia na tukaifikiria na haizungumuzi kwa niaba yenu, ni maoni ya wana-committee, nyinyi wenyewe bado mutaendelea kutoa maoni yenu. Kwa hivyo ile ni kama karatasi ya kusaidia ule muelekeo na mwenendo wa hii kazi ya Katiba. Kwa hivyo kwangu mimi ni kutoa shukrani kwa wale ambao wamepata nafsi ya kuja hapa, na kuwashukuru hata nyinyi raia ambao mumepata nafasi ya kuja hapa, ili kuja kujizungumuzia wenyewe, bila kusemewa na mtu. Na vile ambayo mulipata matangazo na mukaona ni vyema mufike hapa kwa wingi, sisi kwetu tunasema shukrani, maana mumeonyesha kwamba muna hamu ya hii Katiba ijao, iwe munaweza kuichangia. Kwa sababu ile Katiba ambayo tumeitumia, imekuwa na sisi miaka arobanne, na sasa miaka arobanne imefika na tunataka kugeuza tupate Katiba nyingine ambayo itakuwa inatusaidia zaidi katika maisha yajayo. Kwa hivyo ni vizuri mumefanya kitendo hiki cha kuja hapa, na ningependa kila mmoja wenyu atoe maoni yake, ili tuwape nafasi hawa, ambao wamekuja kuandikisha waone kwamba tuna kiu ya hii Katiba, kwamba si kitu ambacho kinazungumuziwa na watu wengine.

Kwa hivyo tungependa tuweze kuzungumuza hata kama ni usiku, tuzungumuze bila uoga. Na nafikiri wamewahakikishia kwamba hakuna uoga wowote na vile munavyoona kwamba unaachiwa useme vile unavyotaka katika hali hii. Kwa hivyo ni shukrani kwamba serikali imetupa uhuru huu na tuutumie vile ambavyo inatosha. Kwa hivyo kwangu mimi ni kusema asanteni kwa kunipa nafasi, na nyinyi raia pia tunawashukuru kwa kuja, ili muje na nyinyi muchangie. Kwa hivyo huu ndio mwenendo mzuri ambao tunajitengenezea mambo ya kesho. Kwa sababu tusipofanya leo, na miaka arobanne nyingine kama ndio siku za kugeuza makatiba, tutakuwa wengine pengine hamuko wakati huo, lakini mimi nimewashukuru vile mumewacha mambo mengi ya kufanya hivi leo na kuona ni vizuri muje hapa. Kwa hivyo mimi naachia hapo nikisema asanteni.

**Com. Lenaola**: Asante sana Hon. Katana. Sasa tuendelee na Susan Kahindi.

**Susan Kahindi**: Asante sana, kawa majina naitwa Susan Kahindi, nitazungumuza kwa niaba ya chama cha walimu. Kwanza nitaanza na elimu. Nataka Katiba yetu ijayo, iwe itapatia mtoto wa Kenya elimu ya bure, kuanzia nursery mpaka form four. Elimu ya bure na ya lazima. Katiba yetu ijayo, tungependa kuwe na uhuru wa shule kuchagua muundo wa elimu kama wanatala 8-4-4, iwe inaweza kupewa hii nafasi. Na kama shule itakuwa inapenda kuendelea na ule mfumo wa zamani wa 7-4-2-3, kuwe na uhuru wa namna hiyo kwa sababu tumeona ni kwamba kuna hinderances wakati tunaweka mfumo mmoja wa elimu.

Nataka kuzungumuzia kuhusu uongozi wa serikali. Katiba yetu ijayo, hatungependa iwe inampatia Rais uwezo wa kufuta watu kazi ovyo ovyo. Nataka mtu akijiliwa kazi awe na tenure of office. Yes, security of tenure. Si leo niamuke ni-seme fulani ametoka hapa ameenda pale, kuwe kutakuwa na muongozo mzuri. Kisha ikiwa itawezekana kwa Katiba yetu ijayo, katika hawa ministers ambao ni watu watakuwa na experience in the ministries wanazi-run. Si mtu amekuwa kwa jeshi amepelekwa kwa land, ama amekuwa kwa lands anapelekwa kwa water. Tunataka ministers wetu wapewe ministries ambazo wana-exeprience nazo.

Security; Katiba yetu ijayo tunataka iangalie sana haya majeshi kwa sababu tunaona ni wengi, na pesa nyingi sana zinatumika kuwalipa na wanakaa tu maofisini especially kama Mtongwe. Vita vya maji vimepigwa sijui imepita miaka mingapi. Kwa hivyo kama itakuwa inawezekana, wakati hakuna vita, hawa vijana wetu ama majeshi wetu wawe wanaweza kuwa mahali wakafanya kazi, kama watavishwa kwa mabarabara, kufanya vitu vidogo vidogo, kuliko mtu akae pale anapandishwa daraja hadi lingine, na mwajiriwa wa Kenya mwingine yuko pale pale, analipwa pesa kidogo na anafanya kazi, saa kumi na mbili asubuhi mpaka jioni kama mwalimu.

Mfanyikazi wa Kenya afanye kazi masaa yale yanatakikana kama mfanyi kazi mwingine. Kuhusu land, iwe chini ya mabaraza, na title deeds ziwe za kutolewa na hizo baraza.

Tunataka serikali yetu ya Kenya iheshimu Katiba hii tunayoiunda leo. Hatutaki Katiba yetu ambayo tunayoiunda sasa iwe inaweza ikavunjwa na serikali yenyewe. Kila mwananchi wa Kenya ambaye atakuwa yuko katika ofisi ama ni raia, aweze kuheshimu Katiba yetu. Ndio nataka kusema kuwe na preamble ya waziwazi. Wakati ikiwa kuna agreement ifuatwe vizuri. Asanteni.

**Com. Lenaola**: Johnson Ndogo Masha? Karisa Charo? Karisa Charo? Patrick Kuloba. Patrick Kuloba? Kanzu Karisa? Kanzu Karisa? Haya endelea.

**Johnson Masha**: Mimi naitwa Johnson Ndogo Masha. Mimi nazungumuza kuhusu serikali. Serikali napenda hiyo...

**Com. Lethome**: Hebu nyamazeni jamani. Kuna makelele huko nyuma.

**Johnson Masha**: Serikali iwe ya majimbo. Na pendeleo langu ni kwamba Rais awe mmoja na kuwe na governors katika kila mkoa. Na Rais atakuwa akisaidiwa na Prime Minister ambaye atakuwa ndiye kiongozi wa serikali.

Kuhusu elimu, katika mkoa wa Pwani, ningependekeza kila mkoa uwe na university moja, na kwa sababu ya umaskini, ambao uko katika hii jamuhuri yetu ya Kenya, ninaomba elimu ya bure ianze kutoka … yaani napendekeza elimu ya bure ianze kutoka nursery mpaka mwisho.

Kuhusu hali ya hospitali, napendekeza ya kwamba cost sharing iondolewe kabisa na hizi hospital charges zipunguzwe. Kuhusu ardhi, title deeds ziwe chini ya mabaraza. Administration, yaani utawala, ma-chiefs na wazee wa vijiji wachaguliwe. Na napendekeza kwamba kila location kuwe na angalau ma-assistant chiefs wawili kwa sababu naona wa ma- assistant chiefs, wengine hawafanyi kazi vizuri. Siyo wengine wanaofanya kazi, lakini angalau usichokeshe mmoja, iwe ni assistant chiefs wawili, hatutaki huyo chief. Na vile vile askari warudishwe kama vile zamani, kusaidia yule chief.

Kuhusu hali ya usalama, kama vile ambavyo tumekuwa tukisumbuliwa na mambo ya ma-shiftas na vile, tungeliomba askari wazidi kufanya nini? Wazidi kuajiriwa na hata kiwango kiwe angalau class cha saba, class nane, maana inasemekana mpaka form four lakini angalau class cha nane. Akiwa amepimwa na ameonekana ni sawa, aajiriwe na kuwe na radio calls kila upande kwa sababu ya hali ya simu vile ambavyo hakuna katika sehemu nyingi za jamhuri. Tukiwa na radio calls vile vile huwa zitasaidia upande wa sarafu.

Kuhusu wanyama wa pori, watu wengi sana wanauawa na wanayama wa porini, na hata mimea vile vile kuharibiwa na wanayama wa porini. Ningelipenda kuwe na fidia kwa serikali. Ikiwa ni mtu ambaye ameuawa pengine kwa mfano ndovu, ama mnyama yeyote vile, alipwe milioni mbili zenyewe, na ikiwa ni mimea, jukumu hili litachukuliwa na mtu wa agriculture ndiye ambaye atakwenda pima pahali pale aone ya kwamba inapasa alipwe kiasi gani Ni hayo tu.

**Com. Lenaola**: Asante sana Bwana Masha, Jonathan Katana Wanje? Jonathan Wanja? Esther Muramba? Esther Muramba? Samuel Kadenge? Lawerence Kingi?

**Samuel Kadenge Wanje**: Mimi kwa jina naitwa Samuel Kadenge Wanje. Mimi, katika hii Katiba, ninataka iwe serikali ya majimbo. Iwe majimbo, na watoto wa hapa kwetu, hawana kazi, Kwa hivyo mapendekezo yangu, ninataka kuanzia watoto wa standard eight ambao walishindwa, wazazi walishindwa na kuwaendesha mbele, walibakia kwenye standard eight, hao, katika hii Katiba, nina mapendekezo kwamba, wanatosha kusimamia mambo ya ulinzi kama asakari. Sababu kuna watoto wengi ambao hawana kazi wanazurura tu hivi hivi, na kusoma wanajua. Kwa hivyo, mapendekezo yangu, hatupendi watu wa elimu ya juu zaidi ambao watatoka mbali na kuja kuwanyanyasa watu hapa. Sababu kuna mambo ambayo yanafanyika ambayo ni kama matusi. Mtu awe ana shida, kama ameibiwa, amepata shida yeyote ambayo anataka askari. Akifika kambini anataka askari,

anaitishwa elfu, ikiwa ni askari mmoja. Ikiwa ni askari wawili, atoe elfu mbili. Hilo ni jambo ambalo linatesa watu.

**Com. Lenaola:** Toa mapendekezo.

**Samuel Kadenge Wanje:** Mapendekezo, ninataka wafanye kazi watu wa hapa kwetu, sio watu wa kutoka mbali na kuja kunyanyasa watu kinamna hiyo. Kutokana na mambo ya masomo, napendekeza watoto kuanzia class cha nursery, waachwe waendelee kusoma bure wakisaidiwa angalau kufikia hapo standard eight. Huko mbele, hata ikiwa ataitishwa pesa, lakini watakuwa angalao wamepata mwangaza. Na tena hapo, serikali itawasaidia wazazi, wawe watatoa chochote, lakini wawe wamepata mwangaza. Kwa hivyo mimi ninaonelea majimbo yaweko, kila mmoja afurahie mahali pake. Sio watu wa hapa kuwa hawana kazi. Hicho kitu hakipendezi. Kwa hivyo natumaini naweza kuachia kwa hayo machache.

**Com. Lenaola**: Asante sana. Tupate Lwrence Kingi.

**Lawerence Kingi**: Ya, kwa jina naitwa Lawerence Kingi. Maoni yangu kwa Katiba ijayo, nataka serikali ya majimbo na President achaguliwe na raia kwanza kabla ya wabunge. Madiwani wawe na elimu isiyopungua darasa la nane. Mbunge, asipofanya kazi vizuri, au diwani asipofanya kazi vizuri, kwanza hawa wawe watakuwa kwa muda wa miaka kumi, lakini wakiwa hao hawawezi fanya kazi vizuri, warudishwe kwa raia, tuwapigie kura wengine, yule awe amefuwa. Sio akae mpaka miaka kumi, na hafai. Tukishamuona mwaka moja ambaye hafai, mara moja tuwe na kura ya maoni kwamba hatutakuwa na imani naye, na tuwe tunaweza kuchagua mbunge mwingine au diwani mwingine.

Mkurugenzi yeyote wa shirika, akosapo nidhamu, na kuvuja pesa za umma, napenda Katiba iseme kwamba asipewe wadhifa nyingine, afutwe na afungwe. Siyo ameharibu hapa, halafu anaenda kufanya kazi mahali pengine. Afutwe kabisa. Machifu na wadogo wao wapigiwe kura. Ma-DO hadi PC wasikae pahali pamoja kwa zaidi ya miaka kumi. Elimu iwe ya bure na ya lazima, na pesa zote ambazo zimekadiriwa … (interjection)

**Com. Lenaola**: Elimu ya bure iwe kutoka kiwango gani cha elimu mpaka gani?

**Lawerence Kingi**: Pimary mpaka secondary level. Na pesa ambazo zimekadiriwa zifanye kazi kwa mfano, kunaweza kuwa kuna pesa ambazo zinatakikana zifanye kazi huku, na kwamba hazifanyi zirudishwe kwa treasury. Tunataka hao wakubwa ambao wanasimamia hii, wawe watu wa Pwani kwa sababu hao ndio wataweza kujua matatizo ya jimbo lao.

Ardhi; Mtu akiwa amekaa hapo kwa muda wa miaka kama kumi, naomba Katiba imuidhinishe mara moja, apewe kibali cha kukaa pale, kusudi kuondoa ma-squatter. Vyama vya siasa visiwe vingi, viwe kama vitano peke yake, sio zaidi. Na mahakama yawe ya kijitegemea. Asante.

**Com. Lenaola**: Asante. Tupate James Kitzau Leso.

**James Kitzao Leso**: Kwa jina naitwa James Kitzao Leso. Mimi mchango wangu wa maoni kuhusu Katiba ijayo, ninapenda nguvu za Rais ziwe nyingi tena za dhati zenye uwezo wa kutunza nchi hii ya Kenya. Na Rais, mbunge na diwani wachaguliwe kwa viwango, kwa kupendwa na wananchi. Si kwa viwango vya kwamba alisoma zaidi, ama ana elimu ya … aweze kuchaguliwa ikiwa watu wanampenda.

Na viwango vya kuchaguliwa viwe vitafanywa na wanaochagua wenyewe. Wawe wanachaguliwa na watu wenyewe kwa kupenda, kwa kadri ya uwezo wa kufanya ile kazi aliyochaguliwa naye kufanya; awe Rais, awe mbunge, na hata diwani kama mimi. Kwani kusoma ni lugha ya kazi lakini si kwa uongozi. Uongozi ni kitu kingine na kusoma ni lugha ya kutafsiri maneno, lakini si kwamba ndio kuweza kuongoza maneno. Kwa hivyo tusichukulie kama mtu aliye hakusoma hawezi kutunza wananchi ama watu wakijiji kile anachoongoza. Hapo itakuwa tunafanya kitu kinachoitwa . Katiba ijayo nataka itambue mambo haya kwa dhati.

Na mapendekezo yangu mengine ni kwamba, kuna wizara zetu za elimu, zifanye kazi kwa dhati na zinapopata viwango vya pesa, iwe mambo yanarudi kwa wizara. Si kwa mambo yale ya kufanya tender, hivi na hivi. Ndiyo yanaleta umaskini wa nchi ama ukora wa watu wetu. Maana kama wizara ya barabara, kama ikitenga pesa za barabara, kama barabara yetu italimwa kama Vitengeni, watu wa Vitengeni waandikwe kazi. Katika Katiba ijayo, iwe na uhifadhi wa nanma hiyo. Lakini pesa za-toka Nairobi kisha twaziregesha Nairobi. Watu wetu watakuwa wezi na mambo kama hayo. Mimi Leso nasema mambo hayo yasiwe katika Katiba ijayo.

Mambo ya wizara, itambuliwe na kazi zote zirudi kwa wizara kusudi watu wetu waweze kupata kazi. Lakini hii mambo ya kufanya fulani ana majongoo, basi pesa zarudi kule na sisi watoto wetu wanaweza kufanya kazi na mikono yao, wanaksoa kazi. Tunataka mambo hayo yasifanyike katika Katiba ijayo na mambo ya ardhi yatiliwe nguvu na muhimu sana kwamba title deeds ziweze kupatikana kwa haraka kama inavyotakikana, kama sehemu zingine za nchi hii yetu ya Kenya. Na mapendekezo yangu mengine, ninapenda kama watu wa wizara kadhaa, wakiwa wameonekana kwamba wanafanya mambo ambayo hayahalisi, ni sawa na kufutwa na waandikwe wengine. Kwani wasomaji ni wengi siku hizi, wasije wakachezea chezea kazi kisha wengine wakakosa kazi, ana-ondolewa hapa ana enda mbele, mwizi mwingine analetwa. Mambo kama haya Katiba Katika ijayo, ifanyiwe uchunguzi na watu kama hawa wasiwekwe katika kazi hizi ambazo ni za serikali. Na machifu, wawe na nidhamu njema ya kujua kwamba, kama si wananchi, hangeandikwa yeye. Na askari wetu, wawe ni walinda sheria na walinda wananchi, wasiwe ma-judge. Katika Katiba ijayo tunapenda askari asiwe judge! Na askari, akiwa amejulikana kwamba amechukuwa pesa kwa ajili ya kwenda kufanya kazi, report ikifika kwa mkubwa, afutwe mara moja. Asiwekwe. Kwa Katiba ijayo, hilo lichangiwe.

Na maombi yangu mengine, ninataka hata hii wizara, mambo ya serikali ijayo, yatazame sana vipengele vya makanisa na watu

wa dini. Watunzwe na walindwe, maana hao wanaombea serikali yetu kila kukicha. Kwa hivyo, hata ningependa, katika serikali ijayo, kuwe na waziri wa dini za nchi hii ya Kenya, kusudi mambo ya dini yahifadhiwe vizuri. Asante.

**Com. Lenaola**: Asante. Tupate Ambrose Thoyaya.

**Ambrose**: Kwa majina naitwa Ambrose Thoyaya Kulingana na Katiba mpya hii ambayo tunaizungumuzia hapa, kwa maoni yangu, kwanza naanza na mambo ya uwajiri. Pendekezo langu ni kwamba katika uajiri wa kazi, yaani ningependekeza kwamba katika mkoa, yale mashirika na kampuni zozote ambazo ziko, wanapoajiri watu, waanze kuchukua watu wa pale sehemu za mkoa, watu kama percentage ya themanini kwa mia. Halafu baadaye wawe wanaweza kuchukua kama 20% kutoka nje. Wale wa mkoa ule wapewe nafasi ya kwanza.

Mapendekezo yangu mengine kwa upande wa kikazi na mambo ya college ni kwamba, hasa kwa upande wa mahoteli, tunaona kwamba mahoteli mengi yako upande wa Pwani. Mapendekezo yangu ningesema kwamba hii college ya Utalii ingejengwa pale mahali ambapo mahoteli yana wingi zaidi. (Hayo ni maoni yangu) ili kwamba watu wakapate kufaidika kwa ajili ya sehemu hiyo ya kazi.

Jambo lingine, ninarudia upande wa university. Mapendekezo yangu ni kwamba katika Pwani au Mikoa, kila Mkoa ukaweze kuwa na University angalau moja kwa kuanzia. Kwa sababu tunaona ya kwamba universities zinaonekana mahali pamoja, mikoa mingi haina university. Hiyo ni jambo ambalo linatutatiza kielimu kwa watoto wetu.

Jambo la tatu ni mabarabara. Tumeona kwamba barabara ni mbaya sana hata kwa upande wetu na sehemu zingine. Kwa hivyo tunaona kwamba mambo hata kama ya usafirisaji, usafiri una shida. Kwa mfano kama kwetu hapa tunatoka hapa mpaka Kilifi, hapa hapa tu tunatoa shilingi mia moja kwa sababu barabara ni mbaya. Na kutoka Mombasa mpaka Malinidi, shilingi mia moja. Hiyo ni sababu ya barabara kwamba ni chafu. Napendekeza kwamba zitengezwe barabara zetu.

Jambo lingine. Machifu na ma-sub-chief wao, na wazee wa vijiji wafanyiwe kuchaguliwa na wananchi wenyewe. Hilo ni pendekezo langu. Jambo lingine ni kwamba Ma-mayor wa miji yetu kama Mombasa, Malindi hata Kilifi, watu kama hawa wachaguliwe na wananchi wenyewe. Hilo ni mapendekezo yangu. Tunarudi upande wa elimu; Elimu tumeona kwamba kuna shida fulani katika mashuleni ambayo inawapata wazazi na hata pia vijana, na pia naona hata walimu pia, hiyo inachangia. Ni jambo ambalo linaonekana kama kidogo sana lakini mimi linanisumbuwa akili yangu sana, ni kwa upande wa hizi text books. Unakuta kwamba kuna vitabu vinakuja kwa mwaka mmoja, vinafundishwa halafu mwaka mwingine haviwezi msaidia mtoto mwingine. Kuna Professor mwingine ametunga vitabu vyake na yeye anapendekeza kwamba vitabu vyake vinunuliwe. Inasemekana sasa kwamba vitabu hivi havifai tena, nunueni vitabu vingine. Ningependekeza kwamba kama kuna vitabu vya elimu ambavyo vimenunuliwa kwa ajili ya mafundisho kwa watoto viendelee kwa muda wa miaka. Kama vile zamani tulikuwa tunasoma Caney Francies Owen, hiyo ilichukuwa muda halafu ikaja ikabadilishwa. Mimi mapendekezo yangu ni kwamba

ingekuwa hivyo. Sio kitabu mwaka huu, mwaka mwingine kitabu kingine kinabadilishwa.

Upande mwingine nikuhusu walimu. Wafikiriwe pia upande wa mishahara kwa sababu ni kazi ambayo si rahisi. Elimu ndio chanzo cha kila jambo. Pili, upande wa maskuli, tungetaka tupate misaada pia kwa majengo. Jambo lingine, ni kwamba tungependekeza serikali isaidie wazazi kwa ajili ya watoto, kwamba wasome bure kuanzia class cha kwanza mpaka form four.

**Com. Lenaola**: Endelea.

**Ambrose**: Jambo lingine ni kuhusu wa afya. Mapendekezo yangu ni kwamba, tuna hospitali ya Coast General, hiyo inawakilisha Coast, kwa district kuna dispensary za districts. Ningependa kwamba kuwe kuna hospitali ambazo zitakuwa zinawakilisha divisions, katika kila mikoa, hayo ni mapendekezo yangu. Kwa sababu kuna shida ya matibabu.

**Com. Lenaola**: La mwisho?

**Ambrose**: La mwisho ni upande wa mambo ya Katiba hii na serikali yetu ambayo itakuja. Mimi ningependa kwamba serikali yetu ikaweze kuwa na Prime Minister na Ma-governor katika provinces. Na katika mapato yetu, mapato ya province yawe yanaweza kuhifadhiwa mahali pale na yakaweze kuhudumia wananchi wa pale katika province yao. Hayo ndio mapendekezo yangu. Kwa hivyo, ni hayo tu.

**Com. Lenaola**: Asante. Tumpate Kazungu Karisa Kiti

**Kazungu Karisa Kiti**: Kwa jina naitwa Kazungu karisa Kiti. Kuchangia Katiba ijayo. Kwanza ni mashamba. Mashamba yetu baada ya kupimwa inahitajika tupate vyeti haraka iwezekanavyo. Kuhusu elimu; Elimu iwe bure kutoka nursery mpaka form four. Na elimu hii labda watoto wetu watakapo maliza form four, na hali ya ukame wa kibarua kama tujuavyo katika nchi hii yetu ya Kenya, tuweze kutilia maanani vyuo vya ufundi kama village polytechnic ambavyo wakati huu vimeachwa kabisa kwa sababu havina nguvu. Elimu hii ya ufundi ambayo ni ya village polytechnic isichukuliwe ni ya watoto ambao wameanguka darasa la nane peke yake. Inahitajika hata wale ambao wanatoka vyuo vikuu kwa sababu bila elimu ya ujuzi katika Kenya hii inakuwa shida kupata kazi. Na walimu ambao wanafundisha katika vyuo hivi vya polytechnic, waweze kutambulika na kupewa mishahara yao vilivyo. Na management ambazo zitakuwa kwa vyuo hivi vya ufundi, viweze kuchunguzwa. Ikiwa kazi inayofanyika katika offici ya manager au manageress, ikiwa kazi hii haiendi vizuri, haraka iwezekanavyo, management hiyo inaweza ikabadilishwa.

Tukienda kwa machifu; Machifu waweze kuchaguliwa kwa kura. Kwa maoni yangu, haina haja kuwa na assistant chief. Kwa sababu wazee wa vijiji wamechaguliwa kila sehemu zote za Kenya hii na wana kazi ngumu ambayo hiyo inatosha kupeleka

moja kwa moja malalamiko ya wananchi kutoka kwa vijiji mpaka kwa chifu moja kwa moja. Kwa hivyo inaonekana kwamba assitant chief hapa hana kazi. Kwa hivyo awe ni chief peke yake na aweze kuchaguliwa kwa kura kwa muda wa miaka mitano.

Turudi kwa madiwani; Madiwani pia waweze kuchaguliwa kwa kura kwa kipindi cha miaka mitano, na diwani huyu awe amesoma angalau darasa la saba, na darasa la nane mpaka form four. Tukienda kwa mbunge, mbunge awe ana elimu ya form four kuendelea. Tukirudi kwa vyuo vikuu. Vyuo vikuu viwe katika kila mkoa, wa Kenya hii yetu. Kila mkoa uweze kupata chuo kikuu angalau kimoja kuendelea.

Malipo ya hospitalini. Zahanati za serikali ziweze kutoa matibabu ya bure katika Kenya nzima. Kwa sababu ugonjwa huwezi kujua ni lini unakuja na mtu hawezi kujitayarisha kuwa na pesa akijua kwamba kesho anaweza kuumwa.

**Com. Lenaola**: Malizia malizia

**Kazungu Karisa Kiti**: Serikali iwe ya majimbo. Rais wetu awe na mamlakha ya serikali kuu lakini kila mkoa uweze kujitegemea wenyewe. Na Rais huyo achaguliwe, awe ana uwezo kuwa tajiri, asiwe maskini, asije akapora serikali na awe na umri wa miaka thelathini, kutoka miaka thelathini mpaka miaka sitini. Ikiwa amefikisha miaka sitini, anaweza kuachishwa kazi kwa sababu ukiwa mzee akili yako inarudi kama mtoto. Anaweza kusema jambo lolote na lisionekane kuwa la maana na watu waweze kulishika kwa sababu yeye ni Rais. Miaka sitini awe anaweza kutolewa nje.

Mwananchi wa hali ya chini aweze kuruhusiwa kufanya biashara ndogo ndogo, bila kulipishwa chochote kwa sababu umaikini unazidi kuenea katika nchi. Mwananchi wa hali ya chini akianzisha kazi kama ya viatu, kama ya kushona, analipishwa mambo ya license kiasi cha kwamba anaweza kushindwa kulipa na umaskini unaendelea kuenea katika mitaa yetu ya nchi hii ya Kenya.

**Com. Lenaola**: Asante. Tupate Angelica Mwang'ombe.

**Angelica Mwang'ombe**: Kwa majina yangu naitwa Angelica Mwang'ombe. Mimi ningetaka Katiba ya wakati ujao iweze kuangalia wananchi. Zaidi tukirudi kwa upande wa mahospitalini, tunakuta mwananchi ambaye ni wa kawaida anateseka sana. Wakati anapoenda hospitalini na ikiwa hana pesa, basi anatatizika sana, hawezi pata matibabu kwa njia inayofaa. Tunahitaji hospitalini zirudishwe kama ilivyokuwako mwanzoni. Ziwe bure ili hata yule ambaye hajiwezi, aweze kupata matibabu.

Nikirudi kwa upande wa watoto, tunaona ya kwamba watoto wetu wanasoma lakini kazi zinakuwa ni shida. Pengine itakuwa kazi zimetangazwa, na watoto wataenda pengine kwa interview, tunaona ya kwamba wanaenda kufanya interview lakini kuna watu waliopitishwa tayari watapata kazi,na hao watoto watarudi bila kazi.

Pendekezo langu ningependa ya kwamba, wakati watoto wanapoenda, wasije wakawa wanaitwa kwa interview kutupoteza,

na huku washatengeneza mambo yao huko juu. Tunataka na sisi tulio upande wa huku Pwani tuweze kufikiriwa kwa watoto wetu maana nao wamesoma kama watoto wa nchi nyingine.

Tukienda kwa upande wa elimu, elimu ningependa kuanzia nursery mpaka form four iwe ya bure na walimu wa nursery wafikiriwe na serikali waweze kulipwa na serikali. Hapo elimu inaweza kutimia bure. Na tukiangalia upande wa elimu, watoto wanasoma ni sawa. Na walimu nao wanahitaji watoto wawafundishe vizuri, wanafundisha vizuri. Lakini hata hivyo, tungependa Katiba yetu iweze kuwaruhusu watoto pamoja, wazazi na waalimu wazidi kuwa kitu kimoja, kusaidia hawa watoto wapate elimu ya juu kama watoto wa nchi nyingine za huko nje nje. Nikiendelea tena kwa upande wa elimu, nikiangalia kwa upande wetu wa hapa Pwani, ma-college tuko nayo, lakini tukiangalia university, hatuna hata moja. Watoto wetu ni kwamba wakitaka kwenda university, mpaka waende mbali. Hata ikiwa kama amepata karo ama amechangiwa, lakini huwa hata tikiti yenyewe inawatatiza wazazi kwa kupeleka watoto kupata elimu.

Nikirudi kwa upande wa vitambulisho, vitambulisho ni kama zina shida kwa upande mwingine kwa watoto. Kuna watoto wanaweza kwenda, wanataka vitambulisho, na ikiwa mtoto amezaliwa hapa, kwa miaka yote ako hapa, amesoma primary hapa, secondary amesoma hapa, akifika kwa kitambulisho anaambiwa mpaka arudi sehemu za chief wa kwao. Upande wa Pwani na watoto wanapata taabu kupata vitambulisho. Utakuta mtoto anapita, amemaliza form four, kitambulisho hawezi kupata na akitaka pengine aende college, inakuwa ni tatizo maanake huwa akitoka sehemu ya huko na ameshakuwa sasa ni mtu mzima, akiwa anaenda college anatakikana apate kitambulisho. Tena mtoto akitaka kutetea haki yake, anashindwa kupata kitambulisho, hawezi kumchagua mbunge ama diwani anayempenda kwa sababu amekosa kitambulisho. Kwa hivyo ningetaka Katiba hii inayokuja ama kwa wakati huu iweze kuangalia watoto kwa upande wa vitambulisho, wapate vitambulisho na waweze kutetea haki zao wao wenyewe kwa sababu mtoto anataka yule wake anayetaka kumchagua na wazazi nao watachagua wale wanataka. Maana mtu akimaliza shule si mtoto tena.

Kwa upande wa viongozi, tunataka viongozi waheshimiwe na viongozi nao waheshimu raia kisawa sawa. Na tukiangalia kwa upande wa madaktari, hasa ukiwa na mgonjwa, unaweza ukafika hospitalini, ukaketi kwa muda mrefu kwenye ubao. Na ikiwa hospitali kama hizi kubwa kubwa, pengine zina milango nyingine ya nyuma, utakuta wale wanaojulikana wanaingia na hapo nyuma. Tunataka hayo yaweze kufikiriwa kwa sababu wagonjwa wengine huweza kupoteza maisha yao kabla hawajafika kwa daktari. Ikiwa kama daktari anangojea anaangalia anachukua yule anayemjua na wewe usiojulikana, basi utazidi kupata matatizo.

**Com. Lenaola**: Malizia

**Angelica Mwang'ombe**: Nikimalizia ninaenda kwa Rais. Rais apewe uwezo wa kutosha. Akipata uwezo wa kutosha, hata hizi bei zinazopanda mara kwa mara, ziwekwe kisawa maana kuna wengine hawajiwezi. Ikiwa kuna wengine wanafanya kazi na wengi wetu ni wale ambao hatuna kazi, utakuta sasa, yule mtoto wa wazazi ambao wanafanya kazi wanaweza pata chakula,

lakini wizi unaongezeka kwa sababu vyakula vimekuwa vya bei ya juu, kuliko mahitaji mengine ya mwanadamu. Tunahitaji hizi bei zibaguliwe vizuri, hata Rais awe na uwezo wa kutosha wa kuweza kutetea hizi bei. Asanteni.

**Com. Lenaola:** Asante. Sasa hapa Ganze giza limeingia. Wamezungumuza watu 108. Tangu tuanze kazi hakuna mahali watu wengi wamezungumuza kama nyinyi. Area nyingi ni watu sabini, watu themanini. Kwa hivyo kwa hii panel, tumevunja record tangu tuanze kazi Central Province. Kwa hivyo nyinyi ndio muna kikombe cha waliyotoa maoni sana. Lakini ninaona mikono miwili, hii ni demokrasia, hebu ni wasikize.

**Speaker:** Niko na memorandum nimeandika nataka niwape.

**Com. Lenaola:** Uko na memorandum? Karibu, leta hapa Itachukuliwa, tutaisoma na tutaichukua. Tumeshukuru sana. Yes, ndungu yangu.

**Speaker:** Mimi nilijiandikisha lakini sijaitwa nitoe maoni yangu

**Com. Lenaola:** Ndio nasema sasa, ndio nasema kwamba kuna watu karibu hamsini bado sijawaita, ni vigumu sana kuwafikia nyinyi nyote. Ndio nasema kwamba munaona giza limeingia, maoni tumeyachukua, hatutawafikia nyinyi wote. Kwa hivyo mutatuuia radhi kwa sababu hiyo tu, otherwise nafikir tumeelewana.

**Com. Lethome:** Nafikiri kuna jambo ningetaka kuzungumuzia. Tafadhalini tusione kuwa leo ndio siku ya mwisho ya kuchukua maoni. Baada ya sisi kuondoka, ikiwa una maoni na ungependa hayo maoni yachukuliwe na yawekwe katika Katiba mpya, una nafasi bado. Tafadhali kaa chini yaandike hayo maoni yako. Kuna mwakilishi na pia kuna kamati ile ya watu kumi katika kila sehemu ya uakilishi bungeni. Hapa sehemu ya Ganze muna watu kumi. Kupitia kwa hao watu, munaweza kuwakilisha hayo maoni. Kwa hivyo siyo mwisho. Na maoni yenu tunawahakikishia yatafika na wakati report itakaporudi tena kwenyu nyinyi kuzunguka, mtaona kuwa maoni yenu yamechukuliwa. Kwa hivyo kuondoka kwetu leo, siyo maana kuwa ndiyo tumefunga mlango wa kuota maoni. Munaweza kuyawasilisha kupitia kwa mwakilishi wenyu wa Wilaya, na pia kamati ya wale watu kumi katika sehemu ya uwakilishi bungeni.

**Speaker:** Mimi nimekaa sana hapa na sijapewa nafasi kutoa maoni yangu. Nipe angalau dakika tatu niseme.

**Com. Lenaola:** Munajua sasa tukifungulia moja, tutafungulia wote. Kwa hivyo tunasema kwamba ni vizuri lakini hatuwezi kusema wewe usikizwe na hawa wengine waachwe. Kwa maana niko na watu hamsini sasa ambao wangependa kuzungumuza. Nafikiri tusameheane kwa hayo. Andika maneno yako vizuri, patia Co-ordinator wa Kilifi, ama mpe mtu yeyote wa committee, itafika. Tumeagana vizuri tufanye hivyo? Ni sawa sawa? Asante sana. Sasa nitamuita Co-ordinator aseme machache halafu tufunge kikao kwa maombi. Karibu Co-ordinator.

**Daniel Mwaringa:** Asante sana ma-commisioners, Mheshimiwa Waziri, langu ni kutoa shukrani kwa vile kama alivyotangulia kusema Mheshimiwa, vile ambavyo mumejitolea, mkaja tukamaliza vizuri, hata ingawa pengine wengine wachache wenyu hawakutoa maoni. Musiwe na wasiwasi, ofisi yetu iko wazi kuanzia Jumatatu mpaka Ijumaa, tunafanya kazi mpaka saa kumi na nusu jioni. Kwa hivyo mkija pale mkileta maoni yenu, tuta-file na tutawasilisha wajibu ule. Kwa hivyo musiwe na wasiwasi. Kusema kweli tumefurahi vile mumejitokeza kwa wingi na hamujachelewa. Kwa hivyo wakati wowote pia mkiweza, andikeni kwenye karatasi, lete, na ujumbe huo utawafikia hawa. Na kwa hivyo sasa ningetaka kumuomba moja wetu atufungie kwa maombi. Tafadhali Eunice tufungie kwa maombi tafadhali.

**Prayer:** (Inaudible)

Meeting closed at 6.15 p.m.

**&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&&**